SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**KAMPUNI** mabasi ya Kilimanjaro yaamriwa kulipa faini ya mil. 300/-


ama
AFYA NA MAZINGIRA
WASICHANA MORO & UKATILI JINSIA ... Mwenyekiti aja juu kuoza binti, Ofisa Ustawi ang'aka sumu ngoma ya Mkole
SAFARI YA KIJINSIA MIKOA SABA... Kote alikopita waziri ameibua 'madudu' yamuweka rehani mama na afya yake
Wataalamu wa Jakaya Kikwete: Wenye shida moyo 60% hufika wamechelewa

UKURASA 13

Nipashe

Alhamisi Desemba 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581167

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mkataba TPA, TICTS tamati Desemba 31

UKURASA 2



Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari, Juma Kijavala.

## Maridhiano kisiasa yalivyotikisa 2022, yakaendelea kuwa kiporo

UKURASA 2

## Wakala mtandao auawa kwa risasi kwenye jaribio la kuporwa fedha

UKURASA 3

MICHEZO NABI NA MTIHANI KWA KAMBOLE, YACOUBA UK. 32

KATUNI UK. 6

HABARI KITAIFA

# Mkataba TPA, TICTS kumalizika Des. 31

**Na Mwandishi Wetu,**
BAGAMOYO

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imetangaza kuwa mkataba wa uendeshaji wa Kitengo cha Upakuaji na Upakiaji Mizigo uliokuwa ukifanywa na Kampuni ya Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) utamalizika Desemba 31, mwaka huu.

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Juma Kijavala, alisema kuanzia Januari mwaka 2023, Bandari itachukua eneo lake na serikali itaamua nani aendelee kutoa huduma zilizokuwa zinatolewa kwenye eneo hilo.

Hata hivyo, mamlaka hiyo imesema wafanyakazi wote waliokuwa wanafanya kazi katika kitengo hicho cha TICTS, ajira zao zitabaki pale pale na maslahi yao yataendelea kuwa salama.

Akizungumza katika kikao kazi cha waandishi wa habari, mjini Bagamoyo jana, mkoani Pwani, Kijavala alisema ni wakati sahihi jamii ikafahamu na kueleweka kwa Watanzania wote kuhusu mkataba wake na TICTS.

"Mkataba wa TICTS haujavunjwa bali umekwisha muda wake, hivyo TPA inachukua eneo hilo kwa ajili ya kuliendesha. Niwahakikishie huduma zetu zitakuwa bora kuliko ilivyokuwa awali na haki zote za wafanyakazi zitaendelea kama ilivyokuwa awali," alisema Kajivala. Akifafanua alisema, mwenye nyumba anapoamua kumpangisha mpangaji ana hiari kuamua aendelee na mpangaji wake baada ya mkataba kumaliza au la, kutokana na TICTS kumaliza mkataba wake eneo hilo litakuwa chini ya Bandari na serikali itaamua apewe nani kuliendeleza.

Kadhalika, alisema pamoja na TICTS kuwa chini ya Bandari ajira za wafanyakazi wote ziko salama huku akisisitiza hata maslahi yao yako kama kawaida na walioko eneo la upakuaji na upakiaji mizigo wataendelea na majukumu yao.

Kijavala alisema makubaliano kuhusu vifaa na miundombinu yote ya TICTS yameshafanyika kwamba vitanunuliwa na kuendelea kutumika na TPA.

Naibu Mkurugenzi huyo alisema mamlaka hiyo pia inatarajia kuzindua Masta kadi ya malipo mapema Desemba 30, 2022 kwa ajili ya kufanya malipo.

Alisema ulipaji kwa kutumia kadi utarahisha shughuli za malipo na kupunguza mlolongo wa foleni hasa benki wateja wanapotaka kulipia huduma.

TICTS ilikuwa na mkataba wa miaka mitano ambao uliisha muda wake Septemba 30, mwaka huu.

Mkataba huo uliongezwa tena muda wa miezi mitatu ili kutoa fursa kwa pande mbili kujadili uwezekazo wa kuongezewa mkataba.

Septemba 2017, Hayati Rais John Magufuli, aliiagiza TPA kupitia upya mkataba na TICTS baada ya aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (SAG), Prof. Musa Assad, kubaini kuwapo na tatizo kwenye mkataba huo.

Baada ya kupitiwa upya mkataba huo mwaka 2017, serikali iliiongezea kodi TICTS malipo kwa mwaka kutoka Dola milioni saba hadi Dola milioni 14.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, dira ya mamlaka hiyo ni kuona inakuwa kinara, kuongoza, kuwa lango la biashara ya kitaifa na kimataifa.



Abiria wakisubiri usafiri wa kuelekea Mwanza na Bukoba baada ya kukwama kutokana na mabasi kuwa machache kipindi hiki cha kuelekea sikukuu katika kituo cha Magufuli, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maridhiano kisiasa yalivyotikisa 2022, yakaendelea kuwa kiporo

**Na Waandishi Wetu**

NI mwaka uliojengwa kwenye maridhiano baina ya serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vya upinzani juu ya kuendesha siasa za nchi huku kukiwa na kikosi kazi kilichotumia hadidu za rejea tisa kuzungumza na Watanzania ambao walieleza matakwa muhimu kuwa ni Katiba Mpya na Mabadiliko ya Sheria za Vyama vya Siasa.

Jitihada za maridhiano zilianza kwa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, kuitisha mkutano wa itifaki wa haki, amani na maridhiano wa wadau na vyama vya siasa Desemba 15 hadi 1, 2022 ukiwa mkutano wa kwanza wa aina hiyo tangu kumalizika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Jaji Mutungi alisema Tanzania haitajengwa na chama kimoja au mtu mmoja na kwamba kila mmoja ana wajibu wa kuijenga nchi katika misingi yenye usawa.

Katika mkutano huo ambao mgeni rasmi alikuwa Rais Samia Suluhu Hassan, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alitaka kuwapo maridhiano ya kisiasa ili kuondoa hali ya kutokuelewana iliyoko. Pia alitaka kuachiwa kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ambaye alikuwa akikabiliwa na kesi ya ugaidi wakati huo.

"Tunaomba sana kwa mujibu wa sheria na kufuata taratibu zote za kisheria, tusaidie mwenzetu tuwe naye ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja, tuunganishe nchi yetu, tufanye siasa kwa tija kwa maslahi ya nchi yetu," alisema.

Baada ya muda, hatimaye Mbowe alikuwa huru baada ya Jamhuri kudai kuwa haina nia ya kuendelea na kesi hiyo ambayo ilikuwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Baada ya kuachiwa, Mei 10, mwaka huu, Mbowe alialikwa na Rais na kufanya mazungumzo naye Ikulu, Dar es Salaam.

"Kitu kikubwa tulichojadiliana ni kuwa Tanzania ni yetu sote na tunapaswa kufanya kazi pamoja, kuijenga lakini hili linawezekana tu iwapo tutajenga uaminifu na kudai haki, pamoja na kuheshimiana. Hii itatusaidia kupata nafasi ya kuijenga nchi yetu," ilikuwa kauli ya Rais Samia baada ya mazungumzo yake na Mbowe.

Baada ya mazungumzo hayo, Mbowe alisema: "Tumekubaliana njia nzuri ya kuwa na maridhiano ni wakati kuna haki. Tumepitia madhila mengi, hakuna haja ya kuyarudia mara kwa mara badala yake tunapaswa kusonga mbele na kuwa na siasa safi na kuiunga mkono serikali. Tunatumai kuwa itatuunga mkono kwenye shughuli zetu ili kila mtu afurahi."

Katika hotuba yake ya kwanza Aprili 22, 2021, juu ya mwelekeo wa serikali yake ndani ya Bunge jijini Dodoma, Rais Samia aliyeingia madarakani Machi 18, 2021, baada ya kifo cha Dk. John Magufuli, alieleza nia yake ya kutaka kukutana na kuzunguma na vyama vya siasa nchini.

Nuru ya kufikiwa maridhiano ilianza kuonekana Mei 20, mwaka huu, baada ya timu ya viongozi wa CHADEMA, CCM na serikali kukutana Ikulu na kufanya mazungumzo ambayo umma ulielezwa yatakuwa endelevu.

Juni, mwaka huu, CCM iliishauri serikali kuangalia namna bora ya kufufua mchakato wa Katiba mpya kwa kile kilichoelezwa ni maslahi mapana ya nchi.

Aidha, Septemba 15, mwaka huu, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani, Rais Samia alitoa taarifa kwa umma akigusia moja ya mambo ambayo kikosi kazi kilichokuwa kinaendelea na kazi kimeyakusanya kama ndiyo kiu ya wadau wa siasa ni kutolewa kwa ruhusa ya kuendesha mikutano ya vyama vya siasa lakini ilionyesha wasiwasi kwenye sheria na kanuni zinazosimamia suala hilo.

**RIPOTI KIKOSI KAZI**

Oktoba 15, mwaka huu, kikosi kazi kilikabidhi ripoti yake na kueleza maoni ya Watanzania waliokutana nao kuwa hitaji lao ni katiba mpya, mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa ili mikutano ya siasa irejee.

Mbowe alikaririwa mara kadhaa kuwa chama hicho hakitajitoa kwenye mazungumzo na CCM, huku Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia, akisisitiza kuendelea kusimamia maridhiano hayo katika kuendesha siasa za nchi.

Baada ya hapo, CHADEMA ambayo ni chama kikuu cha upinzani nchini, ilisusia mkutano wa wadau wa siasa. Pia NCCR-Mageuzi kiliweka msimamo kama huo.

Wiki hii pia CHADEMA ilitoa taarifa kuwa wataendelea na mikutano ya hadhara kuanzia Januari, mwakani, ikiwa Rais Samia ataendelea kuwa kimya kwenye ruhusa ya vyama kuendelea na shughuli hizo.

**KAULI ZA WACHAMBUZI**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Dk. George Kahangwa, alisema kuna haja ya vyama hivyo vya siasa kuongeza nguvu na msukumo zaidi katika mazungumzo hayo ya maridhiano ili yafikie muafaka.

"Hali ya siasa iliharibika zaidi kuanzia awamu iliyopita na baadhi ya waliopo sasa walikuwapo kipindi hicho na wanaendelea kunufaika na hali hiyo, kwa hiyo bila vyama hivyo kuongeza msukumo siyo rahisi kufikia muafaka,"alisema Dk. Kahangwa ambaye mwaka 2015 aliwahi kutangaza kugombea urais katika moja ya chama cha siasa cha upinzani.

"Ni kweli hali ya demokrasia nchini bado si ya kuridhisha sana kwa sababu miongoni mwa vitu vilivyoko kwenye Katiba ya nchi ni pamoja na hiyo ya vyama vya siasa kufanya siasa kwa uhuru ikiwamo kupitia mikutano ya hadhara ambayo haifanyiki. Maana ya kuruhusu vyama vingi ilikuwa ni kuruhusu kupata mawazo mbadala kutoka sehemu tofauti za vyama vya siasa."

"Kwa hiyo kunapokuwa hakufanyiki mikutano ya hadhara au vyama vya siasa havifanyi shughuli zake kwa uhuru basi hapo hakuna uhuru wa kidemokrasia na hakuna mawazo mbadala na maana ya kuruhusu vyama vingi haipo," alisema.

Pia alisema vyama vya siasa kwa ujumla wake vinatakiwa viweke kikomo cha mazungumzo hayo badala ya kuendelea pasipokufahamu mwisho wake.

Mwanaharakati na mdau wa siasa, Selemani Bishangazi, alisema haoni sababu ya kukataza vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara kwa sababu Katiba ya nchi inaruhusu mikutano hiyo.

"Kwanza hata hayo mazungumzo ya maridhiano kwa ajili ya kuruhusu vyama kufanya mikutano ya siasa yapo kinyume kwa sababu kama Katiba inaruhusu mikutano hiyo, kwa nini vizuiliwe na kuanzishwe mazungumzo ya kudai kitu ambavyo kipo kihalali kufanyika," alisema Bishangazi.

HABARI KITAIFA

# Wakala auawa kwa risasi jaribio la kuporwa fedha

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAKALA wa fedha mtandaoni, Richard Nzumbe, mkazi wa Mtaa wa Butengwa, Kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, ameuawa kwa kupigwa risasi na watu wanaosadikiwa kuwa ni majambazi.

Nzumbe alikutwa na mkasa huo juzi saa 1:00 jioni wakati akiwa getini anaingia nyumbani kwake katika mtaa wa Butengwa mjini Shinyanga.

Mwenyekiti wa mtaa wa Butengwa, Onesmo Mayeba, akisimulia tukio hilo kwa waandishi wa habari jana, alisema alipopata taarifa alifika nyumbani kwa marehemu na kukuta tayari majambazi wametoweka huku Richard akiwa ameanguka chini.

Alisema Nzumbe alikuwa anajishughulisha na uwakala wa fedha na kwamba taarifa za awali zinaeleza majambazi hao walimpora fedha. Alisema inaonekana watu hao walimfuatilia muda mrefu na wamempigia risasi getini wakati akiingia ndani.

"Tukio hili ni la kikatili na tunalilaani kwa sababu majambazi hawa wametoa uhai wa mtu na ni kosa la jinai, tunaliomba jeshi la polisi kuwabaini wote waliohusika kutenda mauaji haya ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria," alisema Mayeba.

Shemeji wa marehemu, Salome Dady, alisema majira ya saa 1:00 jioni, alikuwa ndani yeye na watoto wa dada yake, ndipo wakasikia gari la shemeji yake getini, akatoka mtoto kwenda kufungua, akasukumwa na majambazi na kufyatuliwa risasi baba yake.

Alisema baada ya kusikia mlio wa risasi, alitoka nje akakuta shemeji yake amepigwa risasi kifuani na majambazi, ndipo akarudi ndani kuchukua kigoda akampiga nacho jambazi mmoja akaanguka chini, kisha akamchoma na kisu begani.

Wakati akiendelea na mapambano hayo ili kumwokoa shemeji yake, aliwasikia majambazi hao wakisema wanataka hela, ndipo akazichukua hela na kuzikimbiza ndani na baada ya majambazi hao kukimbia, walimpelaka hospitalini lakini alifariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa majambazi hao walimpiga risasi Nzumbe kwa lengo la kumpora fedha.

Alisema mbinu iliyotumika ni kumvizia akiwa anarudi kutoka kazini kwake na kipindi anaingia ndani ya geti la nyumba yake, walimpiga risasi kwa lengo la kumpora fedha zake lakini hawakufanikiwa kuzichukua.

Kamanda Magomi alisema polisi wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo huku akiwataka wafanyabiashara kuacha kutembea na fedha au kuweka nyumbani bali wahifadhi kwenye taasisi za fedha.

## Usajili vitambulisho NIDA sasa kidijitali

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imezindua mfumo mpya wa usajili kwa njia ya mtandao, utakaowezesha wananchi kutuma maombi popote walipo, ndani na nje ya nchi, bila kulazimika kwenda ofisi za mamlaka.

Msemaji wa NIDA, Geofrey Tengeneza, aliyasema hayo jana, Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari. Alisema hatua hiyo imeanzishwa baada ya mfumo uliotumika awali kuwa na malalamiko ikiwamo taarifa kukosewa, wananchi kukaa saa nyingi katika foleni na gharama kubwa.

Alisema mfumo huo unatarajiwa kuongeza kasi ya wananchi kujiandikisha na kuandika majina yao na taarifa zingine kwa usahihi, ikilinganishwa na awali maofisa wa mamlaka hiyo walilazimika walipwe malipo ya ziada baada ya saa za kazi kuisha.


"Mfumo wa awali ulisababisha wananchi kukaa zaidi ya saa tisa kwa kupanga foleni na kusababisha mwamko mdogo wa kujiandikisha, sababu mtu aliangalia akatumie saa nyingi kujiandikisha au akafanye shughuli zake za kiuchumi," alisema.

"Maofisa wa NIDA pia walitakiwa kulipwa fedha za ziada, kutokana na kukaa saa za ziada ili kukamilisha usajili wa wananchi. Pia gharama ilikuwa kwenye vifaa kwa ajili ya ku-scan nyaraka tofauti, kwa kila anayejisajili, mfumo huu utatumia muda mfupi na utatoa fursa kwa raia wageni na wakazi, diaspora kujisajili popote walipo," alisisitiza.

Tengeneza alisema kutokana na mfumo huo mpya, mwombaji atapaswa kuingia mtandaoni na kuandika eonline.nida.go.tz na kufuata maelekezo na kisha baada ya kujaza fomu hiyo ataichapisha, kupeleka kwa mwenyekiti wa mtaa kwa ajili ya kupigwa muhuri.

Alisema fomu hiyo itarudishwa ofisi za NIDA ikiwa na viambatanisho kadhaa, ikiwamo cheti cha kuzaliwa, barua ya utambulisho na kisha kufanyiwa mahojiano na maofisa uhamiaji, kuchukuliwa alama za vidole na kupigwa picha.

"Kwa wale wa diaspora watafanya mchakato huu kule waliko kwa kusaidiwa na Ubalozi, na watakamilisha usajili wao mtandaoni. Tunatarajia kasi ya kujiandikisha itaongezeka kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wana simu za kisasa na kompyuta, kuwezesha kujaza fomu," alisema Tengeneza.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kulia), akisikiliza maelezo ya utekelezaji wa mradi wa usambazaji maji kutoka Makongo hadi Bagamoyo kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto) jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Mahakama yaamuru kampuni ya mabasi kulipa fidia mil. 300/- kusababisha kifo

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imeamuru Kampuni ya Mabasi ya Kilimanjaro Express kuilipa fidia ya Sh. milioni 300 familia ya Leonard Kisena, baada ya kusababisha kifo cha Immaculate Kisena (16) aliyekuwa mwanafunzi wa kidato cha tano.

Hukumu hiyo imetolewa jana dhidi ya wadaiwa watatu ambao ni Kampuni ya Kilimanjaro Truck Ltd, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Rowland Sawaya, na Mjahidi Mohamed aliyekuwa dereva wa basi lililosababisha ajali lenye namba za usajili T 278 ALQ aina ya Scania.

Akisoma hukumu hiyo kwa niaba ya Jaji Leila Mgonya, Msajili wa Mahakama Kuu, Joseph Luambano, alisema wadaiwa wote wanatakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 300 kwa kusababisha kifo, majeruhi na uharibifu wa gari hilo.

Pia ,alisema watakapochelewesha malipo hayo, watatakiwa kulipa riba ya asilimia saba kila siku kwa mwaka na pia wadaiwa watatakiwa kulipa gharama za kesi hiyo na kwamba haki ya rufani iko wazi.

Kisena alifungua kesi hiyo ya madai namba 47, 2022 baada ya kupata ushindi katika Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani ambayo ilimtia hatiani Mohamed katika kesi ya trafiki kwa kukiri kuendesha gari hilo bila kuwa na bima, kusababisha kifo, majeruhi Omenis Kabora na uharibifu wa gari aina ya Toyota Landcruiser lenye namba za usajili T 323 CWB.

Kisena ambaye ni baba wa marehemu Immaculate, Desemba 24, 2021 akiwa na watoto wake wawili na mke wake, walikuwa safarini kwenda mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

Walipofika eneo la Kamala Bagamoyo saa 10:15 alfajiri, basi la Kilimanjaro liliacha njia na kuwagonga, hivyo kusababisha kifo cha Immaculate papo hapo.

Kutokana na ajali hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo, Mwanakombo Mmanya, aliamuru mshtakiwa huyo, Mohamed, kulipa faini ya Sh 110,000 kutokana na mashtaka manne yaliyokuwa yanamkabili au kutumikia kifungo cha miezi sita jela. Kisena aliyewakilishwa na Wakili Dk. Aloys Rugazia, aliiomba mahakama kulipwa fidia ya Sh, milioni 400 kutokana na gharama mbalimbali walizotumia na kuwasilisha mahakamani nyaraka zinazoonyesha gharama halisi za mazishi, uchunguzi wa mwili wa marehemu, gharama za matibabu kwa majeruhi na gari lililoharibika. Pia waliomba gharama za kumpoteza Immaculate katika ajali hiyo.

Hata hivyo, wakati wa maombi hayo wakili wa wadaiwa, Michael Ngalo, aliweka pingamizi akidai kuwa Kampuni ya Kilimanjaro haimtambui dereva wala ajali iliyotokea.

Wakili Rugazia alidai mahakama iliwapa nafasi mdai na mdaiwa kuingia kwenye mazungumzo ya usuluhishi lakini hawakutokea licha ya mahakama kuwapa onyo mara tatu la kufika kwa ajili ya usuluhishi.

Alidai baada ya wadaiwa kushindwa kutii wito wa mahakama, jalada la kesi hiyo lilirudishwa kwa Jaji Mgonya ambaye alitupilia mbali mapingamizi ya wadaiwa na kuamuru kesi isikilizwe kwa upande mmoja.

Baada ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Kisena alisema anaishukuru mahakama kwa kutenda haki kama ilivyokuwa katika kesi ya trafiki Bagamoyo.

Pia alisema familia yake inaendelea kusikitishwa na kitendo cha wamiliki wa basi hilo kutothamini binadamu na uhai wa mtu kwa sababu tangu ajali ilipotokea hawakuwahi kuona mtu yeyote katika kampuni aliyefika nyumbani kwake au kupiga simu kutoa pole.

"Walichokifanya wao ni kuliondoa gari lao katika kituo cha polisi haraka na kuendelea na biashara bila kujali kama kuna uhai wa mtu umepotea," alisema Kisena.

# Adaiwa kumuua mtoto wake kwa kumnyonga

Na Hamisi Nasri, MTWARA

MKAZI wa kitongoji cha Ng'wale kijiji cha Sinde kata ya Msanga Mkuu, Wilaya ya Mtwara, Mwazanije Dadi (34), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumnyonga hadi kufa mtoto wake, Najma Fadhili (4).

Inadaiwa kuwa wakati akitekeleza unyama huo, mwanamama huyo alikuwa uchi wa mnyama.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishina Msaidizi (ACP) Nicodemus Katembo, aliwaambia waandishi wa habari ofisini kwake jana kuwa tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki majira ya saa 4:00 katika kitongoji cha Ng'wale.

Alisema mama huyo alimnyonga mtoto wake hadi kufa na baada ya baadhi wakazi wa kijiji hicho kutoa taarifa hizo polisi ndipo walipokwenda na kumkamata.

Katembo alisema mwili wa mtoto huyo ulifikishwa hospitalini kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu ambao ulionyesha kwamba mtoto huyo alipoteza maisha baada ya kukosa hewa kutokana na kukabwa na kunyongwa na mama yake, hivyo kusababisha kifo,

"Jeshi la Polisi mkoani Mtwara tunamshikilia Mwazanije Dadi (34) kwa tuhuma za kumnyonga mtoto wake hadi kufa. Pia tunaendelea na ushunguzi na mara utakapokamilika tutamfikisha mahakamani kwa tuhuma zinazomkabili," alisema Katembo.

Kutokana na tukio hilo na mengine ambayo yamekuwa yakijitokeza ya mauaji, alisema Jeshi litaendelea kutoa elimu ya ukatili kwa watoto na kwamba jamii lazima ibadilike na kuacha vitendo hivyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rukia Hiyana ambaye ni mkazi wa kijiji hicho na jirani wa mama huyo, alisema usiku wa tukio mama huyo alionekana akiwa amemshika mtoto wake huku yeye mwenyewe akiwa amesimama mbele ya nyumba yake akiwa uchi wa mnyama.

Hiyana alisema watu walitaka kumkamata na kumnyang'anya mtoto mama huyo lakini akaanza kukimbia.

Alisema kuwa baada ya majirani kumwona mama huyo akiwa uchi huku amemshikilia mtoto wake, walianza kukusanyika kwa ajili ya kujionea na kushangaa kwa nini amesimama uchi usiku huo.

Hiyana alisema watu walipotaka kumkamata ili kumnyang'anya mtoto, mama huyo alianza kukimbia na kwenda porini na walipofika, walifanikiwa kumnyang'anya lakini tayari alikuwa ameshamuua kwa kumnyonga.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sinde, Hamisi Issa, kutokana na kitendo alichokifanya mama huyo, aliomba serikali kupitia vyombo vya dola na vile vya sheria, kuchukua hatua zinazostahili.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakifurika katika gulio juzi kwa ajili ya kununua mahitaji ya vyakula na nguo mpya katika maandalizi ya sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kilo 569 za heroin, cocaine zateketezwa

Na Gwamaka Alipipi

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imeteketeza kilo 2,584 za dawa za kulevya zikiwamo tani mbili za bangi na mirungi pamoja na kilo 569.25 za heroin na cocaine.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam baada ya kukamilika kwa uteketezaji huo, Mwakilishi wa Kamishna Mkuu wa DCEA, Veronica Matikila, alisema hatua hiyo imefanyika baada ya kumalizika kwa mashauri ya kesi zilizohusu kukamatwa kwa dawa hizo katika mahakama mbalimbali nchini.

Matikila alisema uteketezaji wa dawa hizo umehusisha mashauri ya kuanzia mwaka 2009 hadi mwaka huu, kwamba ni uteketezaji wa kawaida na hufanyika wakati mashauri katika mahakama yanapokamilika.

Alisema dawa za kulevya zilizoteketezwa zimetoka katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa.

Zingine ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Kibaha Pwani na Mahakama za Wilaya ya Kinondoni, Ilala,Temeke na Kigamboni.

Alisema kwa mwaka huu ni mara ya pili kwa DCEA kuteketeza dawa za kulevya, akifafanua kuwa mara ya kwanza ilifanyika Februari mkoani Mtwara kwamba dawa za kulevya kilo 355 ziliteketezwa.

Alisema tangu kuanzishwa kwa DCEA mwaka 2017 ni mara ya tatu kufanyika kwa uteketezaji wa dawa za kulevya na kwamba mara ya kwanza ilifanyika Oktoba 8, 2019, kilo 120.91 ziliteketezwa, mara ya pili ilikuwa Novemba 12, 2020 kwa kilo 118.174 kuteketezwa.

Matikila alisema wakati wa uteketezaji wa dawa hizo taasisi mbalimbali hushiriki ikiwamo mahakama zilizoendesha mashauri ya kesi hizo, washtakiwa wa kesi ambao huwakilishwa na watu wao, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambao huhakikisha mazingira yanakuwa salama wakati wa uteketezaji, na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika pindi wanapobaini au kuwaona watu wanaoendesha biashara ya dawa za kulevya.

Alisema Tanzania bila ya uwapo na dawa za kulevya inawezekana endapo kila mwananchi atatoa ushirikiano wa kuwafichua wahusika wanaoendesha biashara hiyo.

## Rais Mwinyi asisitiza wasomi kufanya utafiti

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema shughuli za utafiti ziko nyuma ikilinganishwa na shughuli zingine, hivyo amewataka wahitimu wa elimu ya juu kufanya shughuli hiyo ili kulisaidia taifa.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika mahafali ya 20 ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) yaliyofanyika katika chuo hicho, Kibele Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kutokana na mabadiliko ya dunia, wasomi wana jukumu la kusaidia maendeleo ya taifa lao.

Rais Mwinyi alisema licha ya shughuli hiyo kuwa inahitaji fedha nyingi, lazima wasomi kufanya utafiti na shughuli za ushauri.

Alisema mambo hayo yatawaongezea maarifa zaidi ya kitaaluma na kuwawezesha kupanda vyeo sambamba na kusaidia kutatua changamoto mbalimbali ndani ya jamii inayowazunguka.

Dk. Mwinyi alisema inapendeza zaidi kuona wataalamu wa ndani ya nchi wanashiriki katika utafiti na kutafuta ufumbuzi changamoto zinazoikabili nchi.

Kadhalika, aliwataka wahitimu hao watambue kuwa kiwango cha taaluma walichofikia wanakifanyia kazi kwa sababu nchi inahitaji kizazi kipya cha wasomi wenye upeo na uthubutu wa kutatua changamoto zilizoko katika ngazi mbalimbali ya jamii.

Alisema serikali inahitaji aina mpya ya wasomi wanaojituma wenye ubunifu na wasiosubiri kuhimizwa.

Kuhusu elimu, alisema sekta hiyo itaendelea kubaki kuwa nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo si kwa jamii ya Zanzibar pekee bali kwa dunia nzima.

"Elimu ni moja ya ajenda zilizopewa kipaumbele katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 -2025 kwa lengo la kuchochea kasi ya maendeleo ya watu wetu kwani ni vigumu kufikia maendeleo yaliyokusudiwa bila ya kuwa na watu wenye elimu bora," alisema.

Alikipongeza chuo hicho kuanzisha kozi ya shahada ya sayansi katika afya ya jamii na kuahidi kwamba serikali itahakikisha inawaunga mkono kufanikisha malengo yao katika kozi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa, alisema pamoja na serikali kuwekeza katika dhana ya uchumi wa buluu, bado kuna upungufu wa wataalamu katika nyanja hizo.

Alitumia fursa hiyo kuviomba vyuo vilivyoko Zanzibar kuanzisha programu ambazo zinaendana na mahitaji ya soko ya sera ya uchumi wa buluu ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kupata wataalamu ambao watawezesha mafanikio makubwa ya dira ya maendeleo ya mwaka 2050.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Mhandisi Dk. Abdulqadir Othman Hafiz, alisema matarajio yao chuo hicho kusifika kwa kutoa elimu bora ndani na nje ya nchi.

Wanafunzi 568 wakiwamo wanaume 251 na wanawake 317, wamehitimu masomo yao katika ngazi ya cheti, stashaha na shahada ya kwanza.

# Lengo la Samia uzalishaji mbolea latimia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema lengo la serikali la kuhakikisha mbolea ya kutosha inazalishwa nchini badala ya kutegemea kuagiza nje, limetimia baada ya kiwanda cha mbolea cha Itracom kilichoko Nala, jijini Dodoma kuanza uzalishaji.

Majaliwa alisema hayo juzi baada ya kutembelea kiwanda hicho na kujionea shughuli za uzalishaji wa mbolea unaoendelea na hatua iliyofikiwa katika uwekezaji huo.

Alisema uwekezaji huo ambao unaenda sambamba na ujenzi wa viwanda vingine vitatu, kiwanda cha chokaa ya kilimo, vifungashio vya mbolea na kiwanda cha maziwa, utaisaidia serikali katika kukabiliana na changamoto ya ajira.

"Kuna fursa nyingi katika kiwanda hiki ikiwamo upatikanaji wa mbolea ya uhakika na kwa gharama nafuu," alisema.

Waziri Mkuu alisema eneo hilo la uwekezaji lazima liwe na huduma zote muhimu zinazohitajika ili kukiwezesha kiwanda hicho kuendelea na uzalishaji. Huduma hizo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya uhakika ya barabara, maji, mawasiliano na umeme.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kutoa rai kwa Watanzania wanaofanya kazi kiwandani hapo kufanya kwa weledi na uaminifu wa hali ya juu ili wawe mabalozi wazuri kwa wawekezaji wengine wanaotaka kuwekeza nchini.

"Mkifanyakazi kwa bidii na uaminifu mtawarahisishia na wengine kupata kazi," alisema.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliipongeza na kuishukuru serikali kwa juhudi kubwa ilizochukua za kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini na hatimaye kumpata mwekezaji aliyejenga kiwanda hicho ambacho kinakwenda kuiwezesha nchi kupiga hatua kubwa katika suala zima la uzalishaji wa mbolea.

Bashe pia aliwataka mawakala wanaotekeleza usambazaji wa mbolea za ruzuku wafanye kazi hiyo kwa uaminifu kwa kuwa serikali ipo makini na itahakikisha inaendelea kuwachukulia hatua wale wote watakaobainika kufanya udanganyifu.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda hicho, Nduwimana Nazaire alisema ujenzi ulianza Julai 2021 na kimeanza uzalishaji wa tani 200,000 na kimeajiri watu 972. "Mitambo ya laini ya pili na ya tatu imeshafika na ujenzi unaendelea na mwakani tutakuwa tumekamilisha ujenzi wa mitambo itakayozalisha tani milioni moja kwa mwaka," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa uongozi wa kiwanda hicho umejipanga kuzalisha mbolea yenye ubora wa viwango vya juu na rafiki kwa udongo na mazingira ya eneo husika lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini na hivyo kuwaongezea tija wakulima.

## Rais Samia kufungulia maji Bwawa la Nyerere

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, leo anatarajiwa kushiriki tukio kubwa na la kihistoria la kuzindua ufunguaji wa lango la handaki litakaloruhusu maji kuanza kujaa katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

Kwa mujibu wa Waziri wa Nishati January Makamba, tukio hilo litashuhudiwa na wageni zaidi ya 2,300 wakiwamo watanzania 2000 na wajumbe kutoka Misri 300 wakiongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa taifa hilo.

Watanzania wanatarajia utekelezaji wa ujenzi wa bwawa hilo ambao ulianza mwaka 2019, huku serikali ikielekeza nguvu kubwa katika kukamilisha ujenzi huo, ikiwa ni juhudi za kupambana na tatizo la upungufu wa umeme linalolikumba taifa mara kwa mara.

Waziri Makamba, siku chache zilizopita alipotembelea mradi huo, alisema tukio litakalofanyika leo ni moja ya maendeleo makubwa kwa historia ya Tanzania katika kuendeleza mradi huo mkubwa ambao unaelezwa kuwanufaisha Watanzania na hata nchi jirani.

"Mradi huu umefikia asilimia 78 ya utekelezaji wake, na kutokana na umuhimu wake kitaifa, ni ishara kuwa ndoto za taifa katika kutekeleza mradi huo zinatimia," alisema na kuongeza:

"Handaki la kuchepusha maji lina urefu wa mita 700, yaani viwanja saba vya mpira wa miguu na lilijengwa miaka mitatu iliyopita kwa gharama ya shilingi takribani bilioni 235," alisema Makamba.

Bwawa hilo pia litakuwa kivutio cha watalii kwa kuwa liko ndani ya hifadhi na litabadili taswira ya hifadhi hiyo na thamani yake itaongezeka ndani na nje ya Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, alibainisha kwamba inakadiriwa misimu miwili ya kipindi cha mvua, itajaza maji katika bwawa hilo.

"Tunaanza kujaza maji kesho 'leo' wakati kuna mvua za vuli, pia tunategemea mvua za masika mwezi Machi 2023, ambazo zitakuwa za msimu wa kwanza, pia tutapata vuli ndani ya kipindi hicho, kisha tutapata zile za masika katika mwaka 2024 pamoja na vuli ya kipindi hicho, hivyo mvua mbili kubwa za masika zinaweza kujaza bwawa kwa hesabu zilizopo," alisema Chande.




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (katikati), akifafanua jambo jijini Dar es Salaam jana kuhusu ushirikiano walioingia na Benki ya NMB wa uhamasishaji na ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kupitia NMB. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Kodi wizara hiyo, Denis Masami na Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa NMB, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilio sekta binafsi bima afya, hifadhi ya jamii

**Na Christina Mwakangale**

CHUO Kikuu Mzumbe, kimesema asilimia 80 ya waliojiajiri na wa kipato cha chini hawaoni umuhimu wa kujiunga na huduma za bima ya afya na hifadhi ya jamii.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti huo wa miaka minne uliokoma mwaka jana, ukigusa eneo hilo la kisekta umewataja wahusika mahsusi unawajumuisha madereva wa bodaboda, daladala, makondakta, wamachinga, baba na mamalishe, ukiwaeleza hawaoni umuhimu wa huduma hiyo. Mratibu wa mradi huo na mtafiti, Dk. Godbertha Kinyondo, alisema sababu ya kufanya utafiti huo uliofanyika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam ni kubaini iwapo kuna waliomo kwenye sekta hiyo wananufaika na kufikiwa na huduma hizo.

"Tulibaini asilimia kubwa ya kundi hili hawana hifadhi ya jamii ila wenye watoto labda, kwa asilimia ndogo sana, ili amuuguze mwanaye atakata bima. Wawili tu ndio tuliowakuta wamejiunga kwenye mifuko ya hifadhi.

"Sababu ya wao kutokujiunga ni kwa sababu hawana elimu, wanaamini ni uchuro ukikata bima na magonjwa yanaanza, wana kipato duni, wanadai mlolongo ni mrefu kujiunga na kupata mafao huchukua muda mrefu, imekuwa kikwazo kwa kundi hili kujiunga," alisema Dk. Kinyondo ambaye ni Mhadhiri wa Uchumi Chuo Kikuu Mzumbe.

Alisema kundi hilo lipo tayari kushirikiana katika kupata huduma za kijamii kwa kusaidiana kupitia michango na sio kutoa fedha kwa ajili ya kupata huduma, na kwamba walieleza kwamba kuna urasimu na mfumo usio rafiki kufikia huduma hizo.

"Mradi ulianza mwaka 2017 sababu ni kujua jinsi wajasiriamali pamoja na wasafirishaji, wajenzi pia tuliwagusa wote hawana hifadhi ya jamii. Katiba inasema kila Mtanzania awe na hifadhi hata mikataba ya kidunia," alisema Dk. Kinyondo.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Vyama vya Waendesha Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam, Said Msisiri, alisema wapo kwenye mchakato wa kufahamu takwimu rasmi ya madereva wa vyombo hivyo mkoa wote, ili kuwahamasisha kujiunga na huduma hizo.

"Tunakusanya kanzidata kujua tuko wangapi, ili wote wawe na huduma hizi. Takwimu kama 360,000 kutokana na waliolipia maegesho kupitia Latra," alisema Msisiri.

Asha Hassan, ambaye ni mamalishe, alisema baada ya kupata mafunzo amepata uelewa mkubwa kuhusu kujiunga na huduma hizo, ingawa kundi lililopo kwenye sekta hiyo husahaulika katika elimu mbalimbali.

Aloyce Gervas, mmoja wa watafiti kutoka chuo hicho, alisema wasio katika sekta bado hawajanufaika na huduma za hifadhi ya jamii na bima ya afya, ingawa kundi hilo ndio limebeba vijana wengi katika ajira.

Alisema ni wakati wa watunga sera kuweka utaratibu tofauti kati ya walio kwenye mfumo rasmi na usio rasmi ili kunufaika na huduma hiyo, kwa kuwa walio kwenye sekta isiyo rasmi hupata pesa kwa siku zisizo rasmi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sikukuu isiwe mtaji kutajirisha wenye mabasi

**INAPOKARIBIA** kipindi cha mwisho wa mwaka na Sikukuu ya Krismasi, wakati wanafunzi na wafanyakazi wengi huchukua likizo kwa ajili ya kusafiri kwenda mikoani, usafiri huwa wa shida na nauli kupanda bei.

Kipindi hiki watu wengi huhangaika kupata usafiri na wanaofanyakazi kwenye mabasi yanayokwenda mikoani hugeuka miungu watu kwa kuwaringia wasafiri na kuwapangia bei wanazotaka wao.

Hali hii hujitokeza kila inapofika mwezi Desemba, kipindi ambacho watu wengi hupenda kusafiri kwenda mikoani kusalimia ndugu na jamaa.

Wenye mabasi hayo huanza kukata tiketi za wasafiri mapema na inapofikia kipindi cha wiki ya mwisho ya Sikukuu ya Krismasi, watu wengi hukosa usafiri kwa kuambiwa yameshajaa mapema.

Baadhi ya wamiliki na wahudumu wa mabasi hayo yaendayo mikoani hutumia kipindi hiki kujinufaisha kwa kuwapandishia abiria nauli wakijua kwa vyovyote watanunua tiketi kwa sababu hawana njia nyingine.

Wakati kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani kilipokuwa Ubungo, jijini Dar es Salaam, abiria katika kipindi cha sikukuu walikuwa wakisota kituoni hapo kuanzia alfajiri hadi jioni bila kupata usafiri.

Mazingira ya kituo hicho, sehemu kubwa ilikuwa wazi na kipindi cha mwezi Desemba huwa cha mvua na kukumbana na adha ya kunyeshewa kwa kusubiri usafiri.

Adha wanayopata kushinda pia kwenye jua huku wakiwa na watoto ni kubwa na wengine wanakuwa wameshakata tiketi na kuahidiwa basi litafika wakati wowote ili waweze kusafiri, lakini muda unapofika wa kusafiri huambiwa limepata tatizo hivyo waendelee kusubiri.

Kwa kukosa uwezo wa kukata tiketi kwenye basi lingine, huishia kusubiri na wakati mwingine mpaka jioni huku watoto wakilia njaa kwa kukaa kituoni muda mrefu.

Kutokana na adha hiyo wanayopata wasafiri, serikali iliamua kuingilia kati kwa kuiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), kuandaa utaratibu wa kuruhusu mabasi mengine yanayofanya safari za mjini kuruhusiwa kwenda mikoani katika kipindi hicho ili kutoa unafuu kwa wasafiri.

Latra iliamua kutoa vibali kwa mabasi kama Coaster ambayo yanakidhi vigezo vya kusafiri mikoani yachukue abiria kuwapeleka mikoani ili kuwaondolea adha hiyo.

Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, bado kuna suala la tiketi mtandao ambalo limekuwa tatizo kubwa kwa wanaotoa huduma hiyo ya usafiri.

Baadhi yao huwaambia abiria kuwa hawawezi kuwapatia tiketi mtandao mpaka mmliki wa basi aamue nauli ya siku hiyo. Hili ni tatizo na inaonesha jinsi gazi wamilikia hao wanavyokwenda kinyume na agizo la serikali.


Abiria hupewa sharti kuwa wakitaka kukata tiketi ya basi wakubali kupewa ya karatasi na siku ya safari ndiyo wachukue tiketi mtandao ambayo huwa na bei elekezi iliyopangwa na serikali.

Kwenye tiketi ya karatasi mmiliki wa basi ndiye anayepanga bei ya usafiri kwa siku hiyo na kutokana na shida ya usafiri, abiria inabidi akubaliane na bei hiyo ili aweze kusafiri.

Kuna wanaopendekeza katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, mabasi yafanyekazi usiku na mchana ili kuondoa kero hii wanayopata abiria kwa kusumbuliwa na wenye mabasi.

Baadhi ya wamiliki husubiri kipindi hiki ambacho hukiita cha neema kujinufaisha kwa kujipangia bei wanazotaka wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Anaeli Mbise

## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani, ni wakati hizi nadharia za mazingira tuzigeuze katika vitendo

**MAZINGIRA** ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka kiumbe hai katika maisha kama hewa, maji na mmea.

Ili kiumbe hai kiweze kuishi vizuri, kinahitaji mazingira safi na salama na kwa kawaida, mazingira yanahitaji utunzaji wa hali ya juu ili yawe na sifa hizo kuu mbili.

Kwa mantiki hiyo, maisha ya viumbe hai wa kizazi kilichopo na kijacho kinategemea uhusiano mzuri wa utunzaji mazingira. Hali ya kuharibu vyanzo vya maji na mifumo yake, ni miongoni mwa changamoto za mazingira zinazoendelea kukabili taifa letu na dunia, ingawa kuna jitihada mbalimbali za pamoja katika kukabiliana nazo.

Hatua zaidi zinahitajika kuhakikisha hali hiyo inadhibitiwa na kukomeshwa kabisa. Ni ukweli usiopingika kuwa viumbe kama vile binadamu na wanyama vinategemea maji ili kuishi. Viumbe hai hutegemeana na hapo ndipo umuhimu wa maji unapoonekana kuwa wa kiwango kikubwa.

Maisha yanategemea sana maji, mimea na hewa ili kuishi. Vivyo hivyo maisha ya mimea yanategemea maji na hewa katika uhai wake.

Wiki hii Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa katika kongamono la wahariri na wadau wa uhifadhi, mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji mkoani Iringa, lililoandaliwa na Kituo cha Wanahabari Watetezi wa Rasilimali na Taarifa (MECIRA), amesema serikali inaifanyia kazi taarifa za baadhi ya viongozi kudaiwa kuhujumu hifadhi za mazingira na vyanzo vya maji kwa maslahi binafsi na kuwachukulia hatua kwa kuzingatia misingi ya haki.

Kwa kauli hiyo ya Makamu wa Rais, Dk. Mpango aliyoitoa, ni vyema viongozi hao wa kiserikali pamoja na wawekezaji wakubwa wanaohujumu vyanzo vya maji na mazingira katika mto wa Ruaha kuacha mara moja tabia hiyo.

> **Maisha yanategemea sana maji, mimea na hewa ili kuishi. Vivyo hivyo maisha ya mimea yanategemea maji na hewa katika uhai wake.**

Suala hili limefanya uwepo wa harufu ya rushwa kutokana na viongozi pamoja na wawekezaji hao kutoa fedha nyingi kwa mamlaka husika ili waendelee na shughuli za kilimo na ufugaji.

Uharibifu wa namna hiyo katika Mto Ruaha unaleta athari nyingi kwa binadamu, kama vile ukame na hata ukosefu wa maji safi ya matumizi ya kawaida. Ni vyema sasa mamlaka husika zikachukua hatua stahiki ili kumaliza kabisa jambo hili la usimamizi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Hivi karibuni, tumeshuhudia kampeni ya upandaji miti ili nchi iondokane na tatizo la ukame kama ambavyo mwaka huu kulikuwa na mvua chache zilizotokana na mabadiliko ya tabianchi kama vile uharibifu wa mazingira.

Ni wito wangu kuwa viongozi wakubwa pamoja na wawekezaji hao watakuwa mstari wa mbele kuonyesha kwa vitendo umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji kwa wananchi waliozunguka mazingira hayo.

Miongoni mwa njia mbalimbali zinazotumiwa katika uhifadhi wa vyanzo vya maji ni kuepuka kutupa taka kwenye vyanzo vya maji zikiwemo za viwandani ambazo siyo tu zinaharibu mazingira hayo ila pia ni hatarishi kwa afya ya binadamu, lakini pia njia salama za uvuvi wa samaki.

Pamoja na njia hizo za kutunza vyanzo vya maji ni vyema pia binadamu wakaacha kabisa ukataji ovyo wa miti katika vyanzo hivi vya maji kwa ajili ya kuni na hata kuendesha kilimo katika kingo za vyanzo hivyo.

Hakika kila mmoja wetu akichukua hatua stahiki za utunzaji wa mazingira ile kauli ya kutunza mazingira ili yakutunze itakamilika maana uharibifu wa vyanzo vya maji utakuwa umeisha.

## Washauri serikali kupitia mapendekezo ndoa utotoni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MTANDAO wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni Tanzania (TECMN), umeiomba serikali kuyafanyia kazi mapendekezo ya kamati ya wataalamu wa haki za watoto ya Afrika katika kuchukua hatua ili kutokomeza ndoa za utotoni.

Ombi hilo lilitolewa jana mjini hapa kwenye kikao kilichojadili masuala ya mtandao huo na kutolewa tamko kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Akizungumza katika kikao hicho, Mratibu wa TECMN, Euphemia Edward, alisema kuna haja kwa serikali kuweka mkazo katika sheria za kuzuia ndoa za utotoni ili kupunguza idadi ya ndoa hizo nchini.

Edward alisema Juni, mwaka huu, Wizara ya Katiba na Sheria ilitoa barua inayoelezea mchakato wa serikali wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu ndoa za utotoni.

Mratibu huyo alisema mchakato huo umesababisha sintofahamu miongoni mwa wadau zikiwamo asasi za kiraia zinazojihusisha na utetezi wa haki za mtoto na taarifa za kina kuhusiana na mchakato huo hazijapatikana.

Kutokana na ukubwa wa tatizo la ndoa za utotoni, kwa mujibu wa takwimu za Utafiti wa Demografia na Afya (TDHS) za mwaka 2015/2016, asilimia 36 ya wasichana nchini wanaolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 na hizo ni kwa ngazi ya kitaifa

Utafiti huo pia uliainisha hali kwa kila mkoa huku Shinyanya ikiongoza kwa asilimia 59 ya wasichana wanaolewa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18 ikifuatiwa na Tabora asilimia 58 na mingine ni Mara na Dodoma.

"Kwa sasa tatizo ni kubwa na hawa wasichana wanaolewa wakiwa wadogo na wanakatishwa ndoto zao za kupata haki yao ya elimu, wanakuwa hawajakomaa na wapo kwenye hatari nyingine ya kufanyiwa ukatili" alisema.

Mratibu huyo alisema hali hiyo inasababisha ukatili dhidi ya wasichana hao ikiwamo vipigo kwenye ndoa ,ukatili wa kiuchumi kutokana na kukatishwa masomo kwa kuwa hawawezi kujitafutia kipato wala kulea familia.

"Kutokana na wasichana hao kupata mimba za utotoni zinachangia kuongezeka kwa vifo vitokanavyo na uzazi pingamizi," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape kutoka mkoani Shinyanga, John Miyola, alisema tatizo la ndoa za utotoni ni changamoto kubwa hususani katika mkoa huo kwa kuwa asilimia kubwa wanaongia kwenye ndoa wanaachika au kuondoka kwenye ndoa mapema kwa sababu bado ni wadogo.

" Lipo kundi kubwa la watoto wanaolewa bado wadogo na wanahitaji matunzo na malezi na wanapoingia kwenye jukumu la kuwa wazazi au kuwa wake wanashindwa kwenda kuhimili na kuzitunza familia zao," alisema Miyola.




Askofu Dk. Charles Gadi wa Kanisa la Good News For All Ministry akiongoza maombi ya kuombea mvua nchi ya Marekani jijini Dar es Salaam jana, ambayo imekumbwa na ukame. Kushoto ni Mchungaji Bezabel Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Programu TAKUKURU RAFIKI kupania wigo wa wananchi mapambano rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama amesema Programu ya TAKUKURU RAFIKI iliyozinduliwa inatoa fursa kwa kila Mtanzania kushirikiana katika mapambano dhidi ya rushwa.

Amesema serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeamua kuwashirikisha wananchi katika kutekeleza jukumu la kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa ambavyo ni kikwazo kikubwa cha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Mhagama aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizindua programu hiyo kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Viongozi wa TAKUKURU uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa St. Gasper.

Alisema kupitia TAKUKURU RAFIKI, kila Mtanzania atajiona kuwa sehemu ya TAKUKURU na anao wajibu wa kuzuia vitendo vya rushwa mahali alipo, anapoishi, anapofanya biashara au kazi yoyote ambayo inaendesha maisha yake.

Waziri Mhagama aliongeza kuwa TAKUKURU kupitia programu ya TAKUKURU RAFIKI itajiweka karibu na jamii na kuwa rafiki wa wananchi, hivyo kuwawezesha wananchi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa urahisi ambazo zitaiwezesha taasisi hiyo kutekeleza wajibu wake kwa manufaa ya taifa.

"Leo (jana) nimezindua TAKUKURU RAFIKI ambayo faida yake kwa taifa ni kuboresha mifumo ya utoaji wa taarifa na elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa, ili kila mwananchi ashiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa nchini," alisema.

Mhagama alisisitiza kuwa programu hiyo itajenga utayari wa wananchi kuichukia rushwa na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa ni adui mkubwa wa maendeleo katika taifa.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, alisema TAKUKURU RAFIKI ni programu ambayo itaongeza wigo wa wananchi kushiriki katika utambuzi na utatuzi wa vitendo vya rushwa katika jamii.

Alisema katika kutekeleza programu hiyo taasisi yake itajielekeza zaidi kwenye usimamizi wa utoaji wa huduma za kijamii na fedha zilizotolewa na serikali kutekeleza miradi katika sekta za kipaumbele za maji, elimu, kilimo, afya, barabara na ardhi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Abdallah Chaurembo, alisema programu hiyo itamwezesha mwananchi kutambua thamani ya mradi unaotekelezwa katika eneo alilopo na ni kwa namna gani atashiriki katika kusimamia utekelezaji wake ili uwe na tija katika jamii.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# Askari sita wa TFS wauawa 2022

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

ASKARI sita wa Jeshi la Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wameuawa kwa nyakati tofauti katika kipindi cha mwaka mmoja baada ya kushambuliwa na wananchi wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

Matukio hayo yameelezwa kutokea kwa nyakati tofauti katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, mwaka huu, katika hifadhi za Kanda ya Magharibi, Ziwa na Mashariki

Kamishna wa Uhifadhi waTFS, Prof. Dontos Silayo, alibainisha hayo jana wilayani Mvomero baada ya kutembelea kituo cha Hifadhi ya Msitu wa Pagale kilichovamiwa na kundi la zaidi ya watu 50 kwa lengo la kutaka kuwadhuru askari wa uhifadhi na walipowakosa walifanya uharibifu wa mali za serikali na kuiba baadhi ya bidhaa zilizokuwa katika kituo hicho.

Alisema tukio hilo la uvumizi lilitokea siku ya Desemba 16, mwaka huu, wakati askari wameenda kutekeleza majukumu yao na waliporejea walikuta uharibifu huo mkubwa.

"Tunalaani vikali sana matukio haya ya uvamizi katika vituo vyetu ambavyo vimesababisha hasara kubwa kwa serikali, lakini hata kugharimu maisha ya askari wetu sita tangu mwaka huu umeanza pamoja na raia ambao wamekuwa wakitusaidia katika uhifadhi kusababishiwa ulemavu wa kudumu," alisema.

Alisema pamoja na mambo mengine uvamizi huo uliofanywa na wananchi hao katika hifadhi ya msitu huo haukubaliki na tayari hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ikiwamo oparesheni ya kuwakamata wote waliohusika katika tukio hilo.

Prof. Silayo alisema katika msako ulioanza watuhumiwa 50 wameshakamatwa na magunia mawili na nusu ya mahindi yamekamatwa na kwamba watu hao wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya hatua za kisheria.

"Kama tulivyoshuhudia uvamizi huu wa kuharibu mali zaidi ya mamilioni ya serikali, hawakudhamiria kuiba pekee maana yake wangemkuta askari wetu wangeweza kuondoa maisha yake, lakini hatua zimeanza kuchukuliwa kwa watuhumiwa kuanza kukamatwa na kuhojiwa ili sheria ifuate mkondo wake," alibainisha.

Pia aliwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi hawa wanapokutwa wamevamia katika maeneo yaliyohifadhiwa kisheria kwa ajili ya manufaa ya taifa kwa ujumla

Awali, Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Mtibwa, Abdalah Mchomvu, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 16, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana kwa kile kinachohisiwa kuwa baada ya kuwakosa askari waliokuwa wanawasaka waliamua kuharibu na kuiba mali.

Alisema mali zilizoibwa ni pamoja na magunia 31 ya mahindi, viroba 10 vya unga wa ngano, kuku wa kienyeji 250, sukari kilo 25 pamoja na gunia moja la dagaa vyenye thamani ya Sh. milioni 14

Kwa mujibu wa mhifadhi huyo, uharibifu wa mali uliofanyika ni kuvunjwa kwa milango na madirisha katika nyumba zote mbili zilizojengwa katika kituo hicho ambapo thamani yake inafikia milioni 25.5.

"Katika tathimini tuliyoifanya awali uharibifu huu umegharimu kiasi cha Sh. milioni 40 katika mali zilizoharibiwa na zile zilizoibwa, lakini pia hata suruali sita za askari wetu ambazo zilikuwa ndani pia waliondoka nazo," alisema. Alisema uchunguzi wa awali unaonesha waliotekeleza uhalifu huo sio wafugaji peke yao bali unahusisha pia hadi wakulima ambao inasadikika wanataka kufanya shughuli za kibinadamu katika msitu huo uliohifadhiwa kisheria

Akizungumza kwa simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilimu, alithibitisha kushikiliwa kwa watuhumiwa hao ambapo wanaendelea kuwahoji ili kubaini chanzo cha tukio hilo

"Ni kweli hilo tukio lipo na watuhumiwa walikamatwa na mamlaka husika kwa sababu sheria zao zinawaruhusu, lakini kwa kuwa hawana sehemu ya kuwahifadhi walitukabidhi polisi ambapo tunaendelea na mahojiano na baada ya uchunguzi kukamilika watafikishwa mahakamani," alisema.




Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Halopesa, Magesa Wandwi na Ofisa Masoko, Roxana Kadio, wakikata utepe kuzindua rasmi kampeni mpya ya Halopesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjumbe wa NEC ataka viwanja vya CCM kutambulika kisheria

**Na Munir Shemweta**

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Angeline Mabula, amewataka viongozi wa chama hicho wilayani Ubungo, kuhakikisha viwanja vya chama vinatambulika kisheria kwa kuwa na hatimiliki ili kuepuka uvamizi.

Dk. Mabula ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema hayo juzi alipotembelea ofisi za CCM wilayani humo kwa lengo la kusalimia ikiwa ni siku chache baada ya kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa NEC.

"Ni lazima chama kisimame kiuchumi kwa kuhakikisha viwanja vinatambulika kisheria kwa kuwa na hatimiliki. Kama kuna nafasi chama kiweke mipango vizuri ikiwamo ya ubia," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, CCM inavyo viwanja vingi kwenye maeneo mbalimbali nchini lakini baadhi haviko kisheria ingawa vinatambulika kama mali ya chama. Alisema kutotambulika kisheria kumepitwa na wakati na kikubwa ni kujua namna ya uendelezaji rasilimali za chama unavyofanyika. "Kama kuna viwanja basi iwekwe mipango vizuri na ikiwezekana kuingia ubia na taasisi kwa ajili ya kuendeleza. Lazima tuangalie maeneo yaliyo katika 'prime area'. Tusiwe na mawazo tu kuwa hizi ni mali za CCM," alisema Dk. Mabula.

Mjumbe huyo wa NEC alipongeza CCM wilaya ya Ubungo kwa kuwa na eneo lake Kibamba na kufanikiwa kujenga ofisi ya chama huku akisema uamuzi huo unakisaidia chama kuepukana na utaratibu wa kupangisha ofisi.

Aliwataka wanachama wa CCM Wilaya ya Ubungo kufanya kazi kwa bidii na kuishauri serikali kutimiza majukumu yake. Alisema hayo yote yakitimizwa, basi wataweza kuiunganisha serikali na chama na kuongea lugha moja.

"Kubwa tufanye kazi kwa bidii na kuishauri serikali na kikubwa kutimiza majukumu kupitia ngazi mbalimbali za chama kuanzia shina na tukiweza kuyasimamia hayo ni jambo la msingi na tutakuwa tumeunganisha chama na serikali vizuri. Pia tutakuwa tunaongea lugha moja, kikubwa kuhakikisha utekelezaji wa ilani kama ilivyokusudiwa.

## Kampeni Halopesa kuwafurahisha wateja kwa zawadi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Simu ya Halotel imezindua kampeni ya 'Shinda tena na Halopesa' itakayowezesha wateja kujishindia pesa taslimu, runinga na bajaj.

Akiongea kwenye mkutano wa waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam, Naibu Mkurugenzi Mkuu, Magesa Wandwi, alisema furaha yao ni kutoa huduma za kifedha na kuwawezesha wateja hususani wa HaloPesa kufanya miamala tofauti ikiwamo ya kutuma benki, kulipia bili na kwenda mitandao mingine.

Alisema zaidi ya wateja milioni 2.5 wanaendelea kufurahia huduma zenye ubora na kwa gharama nafuu muda wowote.

Wandwi alisema kampeni hiyo ni kwa ajili ya kuhamasisha na kuwapa motisha wateja wa HaloPesa waweze kuendelea kutumia huduma za kampuni hiyo na kuwapa chachu wateja wengine waweze kuingia kwenye ulimwengu huo. "Ni ndoto yetu kuona Watanzania wote wanatumia huduma za kifedha kiganjani mwao."

Alisema kampeni ya Shinda na HaloPesa itakuwapo kwa miezi mitatu na wateja 135 wanatarajiwa kushinda zawadi mbalimbali zikiwamo pesa taslimu, runinga na bajaji mpya.

**Alisema zaidi ya wateja milioni 2.5 wanaendelea kufurahia huduma zenye ubora na kwa gharama nafuu muda wowote.**

# Chatanda apiga marufuku vikao kujadili watu

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa** KOROGWE

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Taifa, Mary Chatanda, amepiga marufuku mtindo wa baadhi ya viongozi wa umoja huo kufanya vikao vya kujadili watu ambao alisema unawagawa wanachama.

Amesema kukaa vikao vya kujadili watu ni hatari kwa uhai wa umoja huo, kwa kuwa unawafanya wanachama wa UWT wasiwe na maelewano, kitendo ambacho kinaweza kusababisha wasifanye kazi kwa ushirikiano.

Chatanda alisema hayo mjini Korogwe mkoani Tanga juzi, wakati wa mkutano wa mapokezi yake ikiwa ni mara ya kwanza kufika nyumbani kwao tangu achaguliwe kushika nafasi hiyo hivi karibuni.

"Napiga marufuku vikao vyote vinavyojadili watu kuanzia ngazi ya chini hadi taifa. Viongozi msiwagawe watu, fanyeni vikao vya kujadili mafanikio na changamoto zinazoikabili jamii na kuzitafutia ufumbuzi," alisema.

Alisema ni muhimu viongozi wa umoja huo kuunganisha watu, ili kumsaidia Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

"Lakini tuvunje makundi, uchaguzi umekwisha, sasa kazi iendelee ya kutekeleza majukumu yetu ikiwamo kuitetea CCM, shughuli za maendeleo ya jamii na kuongeza idadi ya wanachama wapya wa UWT," alisema.

Bila kufafanua zaidi, mwenyekiti huyo alisema mwaka 2025 wanawake wana jambo lao na kwamba ili jambo hilo litimie, wanapaswa kuwa kitu kimoja, kwa kuwa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

"Tuyafanye haya yote kwa pamoja, ili pia tuweze kurudisha chama na jumuiya zake kwenye enzi za TANU, kwani kila mwanachama aliwajibika kikamilifu kwenye nafasi yake na kuifanya UWT kuwa imara," alisema.

Chatanda pia alikemea mtindo wa baadhi ya viongozi wa CCM kuwachagulia wanachama viongozi, badala wawachie kazi hiyo wenyewe wachague ni yupi ambaye wanataka awaongoze.

Alisema hayo kufuatia malalamiko ya Diwani wa Kata ya Kwashemshi, Korogwe Vijijini (CHADEMA), Twahiru Salehe, aliyerejea CCM, huku akilaumu baadhi ya viongozi wa CCM waliosababisha ahamie upinzani.

"Viongozi acheni kubeba wagombea, waachieni wanachama wenyewe wachague kiongozi ambaye wanapenda awaongoze, msisababishe watu kuchukia chama kwa maslahi yenu," alisema.

Awali, alipopewa nafasi kuzungumza baada ya kurejea CCM, Salehe alisema alihamia CHADEMA wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 baada ya kufanyiwa figisu na baadhi ya viongozi wa chama wa kata hiyo.

"Kama nitawakweza naomba mnisamehe, nilihamia CHADEMA, ni kutokana na udhaifu wa baadhi ya viongozi wa CCM wa Kata ya Kwashemsi. Chama kisimshike mtu kishike maoni ya wananchi," alisema Salehe.

Alisema mtindo wa baadhi ya viongozi wa CCM kutofuata maoni ya wananchi, unasababisha chama kupoteza watu ambao wanapendwa na wapiga kura kama ilivyotokea kwenye kata hiyo.



Mratibu wa Programu za Kukuza na Kuendeleza Ujuzi (Sugeco), Irene Faustine, akisisitiza jambo wakati wa majadiliano ya mradi wa Tanga Yetu wenye lengo la kuinua vijana kupitia sekta ya kilimo jijini Tanga jana. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

## Viongozi wasiosimamia rasilimali watu kukiona

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema serikali haitosita kumchukulia hatua za kinidhamu na kisheria kiongozi yeyote atakayeshindwa kusimamia vizuri rasilimali watu kwa ajili ya ustawi wa taifa.

Mhagama alisema hayo juzi wakati wa kikao kazi chake na watumishi wa umma katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro kilicholenga kuhimiza uwajibikaji na kutatua changamoto zinazowakabili watumishi katika halmashauri hiyo.

Alisema hatamwonea aibu wala huruma kiongozi yeyote aliyepewa dhamana ya kusimamia rasilimaliwatu ambaye atabainika kukiuka sheria na taratibu za usimamizi wa rasilimaliwatu.

Aliongeza kuwa viongozi wenye dhamana ya kusimamia rasilimaliwatu wanapaswa kuiheshimu, kuithamini na kuhakikisha inakuwa kwenye mikono salama kwa sababu inategemewa na Serikali kwa kiasi kikubwa katika ustawi na maendeleo ya taifa.

"Rasilimaliwatu ambayo ndio watumishi wa umma ikisimamiwa vizuri itaisaidia serikali kutimiza lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kutekeleza mipango na mikakati ya maendeleo katika taifa," alisema.

Mhagama alisisitiza kuwa watumishi wa umma ndio wanategemewa kutoa huduma bora za afya, kuboresha huduma za maji, kuboresha huduma za elimu, kuboresha huduma za miundombinu pamoja na kilimo.

Akizungumza kwa niaba ya watumishi wa halmashauri hiyo, Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Kilosa Kilosa, Mwalimu Richard Shagungu, aliishukuru serikali kwa kuendelea kulipa kila mwezi madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi katika halmashauri hiyo na kuomba waajiri wasizalishe madai mapya ili serikali iyamalize.

# Mawakala kukusanya kodi za ardhi

**Na Munir Shemweta**

MATAWI 228 ya Benki ya NMB nchini katika kila eneo kupitia zaidi ya mawakala 17,000 yanatarajiwa kutoa huduma za ukadiriaji na ukusanyaji kodi na tozo mbalimbali za ardhi nchini.

Hayo yalibainishwa juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, wakati wa uzinduzi wa mkakati maalum wa ushirikiano wa wizara ya benki hiyo NMB katika ukusanyaji wa kodi na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Dk. Mabula alisema mkakati wa kushirikiana na NMB unalenga kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kuandaa kampeni maalum ya ukusanyaji kodi na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi. Wizara kupitia NMB na mawakala wake, watatoa huduma ya ukadiriaji na ulipaji kodi ya ardhi kwenye matawi 228 ya benki hiyo katika kila eneo ambako zaidi ya mawakala 17,000 watatoa huduma.

Alisema Wizara ya Ardhi tayari imetoa mafunzo ya namna ya ukadiriaji na ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kwa wafanyakazi wa NMB kupitia njia ya mtandao ambayo matawi yote yalishiriki. Mafunzo kwa mawakala yamefanyika kila mkoa na kazi inaendelea.

Waziri aliwataka wananchi wote kuchangamkia fursa hiyo ya usogezaji huduma karibu na ubunifu uliofanywa kwa kushirikiana na NMB.

Aidha, Dk. Mabula katika uzinduzi wa kampeni hiyo, aligusia pia suala la msamaha wa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusiana na riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi. Kupitia msamaha huo, wananchi walipewa nafuu ya kulipa deni ya msingi ili kusamehewa riba ya malimbikizo na nafuu hiyo ilitolewa kuanzia Julai, hadi Desemba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, tangu msamaha huo utolewe takribani miezi mitano na nusu imepita na kasi ya wananchi kujitokeza bado hairidhisha huku akibainisha kuwa takwimu zinaonesha wamiliki 2,819 ndio walioomba na kukidhi vigezo vya msamaha na Sh. 11,993,281,914 zililipwa kama deni la msingi.

Alitoa rai kwa wananchi wote kutumia kipindi hiki cha siku chache zilizobaki hadi Desemba 31, kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka kwa furaha ya msamaha wa riba baada ya kukamilisha kulipa deni la msingi.

Waziri Mabula alisema baada ya muda huo, ofisi zote za ardhi katika wilaya na mikoa zitachukua hatua za kisheria kwa wote wanaodaiwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria ili kukusanya maduhuli ya serikali.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB ambaye ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi, alisema benki imejipanga kikamilifu katika kuhakikisha mkakati wa kusaidia ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi unafanikiwa na kuiwezesha serikali kukusanya mapato kupitia sekta ya ardhi.

HABARI KITAIFA

# Mfumokazi wa bioanuwai wapitishwa COP15

**Na Mwandishi Wetu**

MAKUBALIANO ya Umoja wa Mataifa yanayolenga kubadilisha mwelekeo wa upotevu wa viumbe anuwai na kuweka dunia katika njia ya kurejesha bioanuwai zilizopotea, yamepitishwa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Bioanuwai (COP15) Montreal, Canada.

"Maudhui yamepitishwa," Huang Runqiu, Mwenyekiti wa COP15 na Waziri wa Ikolojia na Mazingira wa China, alitangaza juzi wakati akipiga siwa yake na baada ya hapo, shangwe na vifijo kutoka kwa wajumbe viliibuka katika ukumbi wa mkutano.

COP15, ambayo inajulikana rasmi kama mkutano wa 15 wa Mkutano wa Nchi Watiasaini wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Bioanuwai, ulihitimishwa juzi baada ya takriban wiki mbili za majadiliano. Makubaliano hayo yaliyopitishwa yanajulikana rasmi kama Mfumokazi wa Bioanuwai wa Dunia wa Kunming-Montreal.

Wadau wamekubaliana kuhusu masuala muhimu, ikiwa ni pamoja na malengo na shabaha, uhamasishaji wa rasilimali na habari mfululizo za kidijitali (DSI), chini ya mfumo huo. Mfumokazi huo unajumuisha malengo manne na malengo 23 ya kufikiwa ifikapo mwaka 2030.

Mfumokazi pia unaweka shabaha ya kuongeza mtiririko wa fedha wa kimataifa kutoka nchi zilizoendelea hadi nchi zinazoendelea, hasa nchi zilizoendelea kidogo, nchi za visiwa vidogo zinazoendelea na nchi zilizo na uchumi wa mpito hadi angalau dola za Kimarekani bilioni 20 kwa mwaka ifikapo Mwaka 2025 na angalau dola za kimarekani bilioni 30 kwa mwaka ifikapo mwaka 2030.

Pia unataka urejeshaji wa bioanuwai ukamilike au uendelee kwa angalau asilimia 30 ya ardhi iliyoharibiwa, maji ya bara, na mazingira ya pwani na baharini.

"Baada ya miaka minne ya juhudi, mchakato huo hatimaye umefikia kikomo," alisema Huang huku akiongeza kuwa maudhui hayo yaliyopitishwa yataongoza juhudi za pamoja za pande zote kukomesha mwelekeo wa upotevu wa bioanuwai ili kuweka dunia kwenye njia ya kurejesha bionuwai zilizopotea na kuwanufaisha wanadamu wote. Akielezea mpango huo kama wa kihistoria, Huang alisema mfumokazi huo umeonyesha maono ya Mwaka 2050 ya "kuishi kwa amani na mazingira ya asili."

China ikiwa nchi mwenyekiti wa COP15. COP15 ilifanya mkutano wa awamu ya kwanza huko Kunming, Mji Mkuu wa Mkoa wa Yunnan Kusini-Magharibi mwa China, mwaka 2021. Awamu ya pili ya mkutano wa COP15 Montreal, iliendelea ikiwa na kaulimbiu isemayo "Ustaarabu wa Ikolojia: Kujenga Mustakabali wa Pamoja wa Viumbe Vyote Duniani."



Mwenyekiti wa COP15 na Waziri wa Ikolojia na Mazingira wa China, Huang Runqui, akitangaza kupitishwa kwa Mfumokazi wa Bioanuwai wa Kimataifa wa Kunming-Montreal, katika mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Bioanuwai (COP15) Montreal, Canada, juzi. Kulia ni Katibu Mtendaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Bioanuwai, Elizabeth Mrema. **PICHA: XINHUA**

# LATRA yashauriwa kutoa muda wa majaribio ya usafiri SGR

**Na Pilly Kigome**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kutoa muda maalum kwa wananchi kutumia usafiri wa treni ya mwendo kasi SGR kwa majaribio kabla ya kutumia nauli pendekezwa itakayopangwa na mamlaka.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo katika ufunguzi wa mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu viwango vya nauli za abiria kwa watumiaji wa treni ya SGR kutokea Dar es Salaam hadi Bahi - Dodoma.

Alisema usafiri huo ni mpya nchini na kuiomba LATRA isipitishe nauli hizo ili kuwapa nafasi wananchi watumie usafiri huo kwa majaribio na kuridhika.

Alisema wananchi wengi wanahamu kubwa ya kuanza kutumia usafiri huo na kwamba inabidi wapewe muda wa kuuangalia.

Pia alilitaka Shirika la Reli Nchini (TRC), kabla ya kupanga nauli hizo wakumbuke kuna Watanzania wa hali za chini wakulima wa vijijini wanasubiri kwa hamu kubwa kutumia usafiri huo ili uweze kuwarahisishia katika shughuli zao.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema watahakikisha wanayafanyia kazi mapendekezo yote kwa kuwa jukumu lao ni kuona wananchi wote wanamudu kutumia usafiri huo.

Aliwataka Watanzania kuwa watulivu katika kipindi hiki cha mapendekezo kwakuwa kumekuwa na uelewa hafifu kwa baadhi yao kwa kudhani tayari mpendekezo yaliyotolewa na TRC ni nauli rasmi.

Alisema mapendekezo ya TRC waliyapokea wakiwa kama wadau na kuwataka Watanzania kujitokeza kutoa maoni yao kuanzia Desemba 19 hadi Januari 3, 2023 bila uwoga.

Alisema wanaweza kutoa mapendekezo kuandika barua kwa sanduku la barua Mkurugenzi Mkuu Latra, sanduku la barua 1742, barua pepe info@latra.go.tz, dg@latra.go.tz

Kaimu Mtendaji Baraza la Ushauri la Watumiaji wa huduma za usafiri ardhini (LATRA TCC), Leo Ngowi, alisema usafiri wa reli ya mwendokasi unasubiriwa kwa muda mrefu na Watanzania na wanatarajia matokeo chanya.

Alisema TRC wanatakiwa kuweka bei ya kuongeza ustawi wa jamii ambayo ni gharama ya chini za uendeshaji zinazolingana na mahitaji kuliko kuangalia faida kwa upande wao.

Alisema nauli iliyopendekezwa na TRC itawafanya wengi washindwe kutumia usafiri huo na asilimia 53 waliohojiwa walisema hawataweza gharama hizo kwa kuwa ziko juu.

Aliwataka TRC waombe ruzuku serikalini na baadaye wafanye mahesabu ya kumwezesha abiria kulipa gharama nafuu ya kumfanya aweze kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa kutumia usafiri huo.

Ngowi alisema Baraza limependekeza kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro kwa mtu mzima nauli iwe Sh. 8,000 na mtoto Sh. 4,000. TRC walipendekeza kwa safari hiyo mtu mzima Sh. 24,794 na mtoto Sh. 12,395.

Dar es Salam kwenda Dodoma wamependekeza mtu mzima Sh. 19,000 na mtoto Sh. 9,000. TRC ilipendekeza mtu mzima Sh. 59,494 na mtoto Sh. 29,747.

## KKKT yabadili chuo kuwa shule

**Na Elisante John,** SINGIDA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Dayosisi ya Kati limebadili matumizi ya Taasisi ya Kilutheri Kiomboi mkoani Singida kutoka Chuo cha Masomo ya Theolojia kwa wachungaji kuwa Shule ya Sekondari ya Junior Seminary ili kuandaa viongozi na wataalamu wakiwa na umri mdogo.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kati, Mchungaji Dk. Syprian Hillinti, alisema juzi kuwa uamuzi huo unalenga kuleta mageuzi makubwa ya elimu kwenye dayosisi hiyo kongwe nchini.

Akizungumza wakati wa ibada maalum ya kuwaingiza kazini wakuu wa majimbo matatu na wachungaji 31, alisema sasa wachungaji wapya watalazimika kupata elimu ya Theolojia katika vyuo vingine vya KKKT, ikiwamo Makumira (Arusha), Mweka (Kilimanjaro) na Tumaini (Iringa).

"Wachungaji hawa 31 walioingizwa kazini leo, ni wa mwisho kuhitimu kwenye Taasisi ya Kilutheri Kiomboi...sasa tunaanzisha Shule ya Sekondari Junior Seminary na maandalizi yameanza, tunatarajia itaanza rasmi Januari 2024," alisema Askofu Dk. Hillinti.

Alifafanua kuwa, utaratibu wa kupata wanafunzi utafanyika kwa majimbo yote ya dayosisi hiyo na maeneo mengine ya nchi, huku wanafunzi watano wa kwanza, watajiunga na shule hiyo, anayoamini italeta ushindani wa juu, miongoni mwa shule mahiri za sekondari nchini.

Katika hatua nyingine, Askofu Dk. Hillinti, aliwataka wachungaji wapya walioingizwa kazini, kuzingatia maadili mema, ikiwamo kudumu katika imani thabiti, unyenyekevu na kupenda watu wa aina zote, ili kuleta ufanisi kulingana na imani ya KKKT.

"Leo baada ya kuingizwa kazini, tumewapangia vituo vya kwenda kufanya kazi, kwenye maeneo inakoishi jamii...huko msijione wanyonge, nendeni mfanye kazi ya Mungu kwa uaminifu, hujui baadaye utakuja kuwa nani katika Dayosisi hii," alisisitiza Askofu.

Akiwasomea vituo vya kazi kwenye sharika mbalimbali, Katibu Mkuu wa Dayosisi hiyo, Shadrack Langu, alisema kuwa anaamini wachungaji hao watakwenda kufanya kazi kwa bidii, ili kuponya mioyo ya watu na kuipatia jamii maendeleo.

Kwa mujibu wa Katibu huyo, Kanisa la KKK Dayosisi ya Kati, pamoja na kutoa mchango mkubwa kwa sekta ya elimu na afya, kwa miaka iliyopita, linataka kuongeza kasi ya maendeleo zaidi, ili yaendane sawa na ukongwe wake, tangu ikiwa ni kati ya makanisa saba ya Kilutheri hapa nchini, yaliyoanzisha KKKT mwaka 1963.



## Watalii Hifadhi ya Mkomazi waongeza mapato ya kigeni

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

IDADI ya watalii wanaoitembelea Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi inatajwa kuongeza mapato ya kigeni kwa zaidi ya asilimia 100 katika kipindi cha mwaka 2021/22.

Kamishna Msaidizi wa Hifadhi hiyo, Happyness Kiemi, alisema idadi ya watalii kutoka nje na mapato hayo yaliongezeka, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kushiriki na kuzindua filamu ya 'The Royal Tour' inayotangaza vivutio vya utalii na hifadhi za Tanzania.

Kiemi alitoa takwimu hizo jana jijini Tanga wakati akizungumza na watumishi wa kada mbalimbali wanaohudumu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

"Sisi wa Mkomazi tunaishukuru sana serikali kwa kubuni na kutengeneza filamu ya The Royal Tour, kwa sababu kama sisi imetubeba kweli kweli na mapato yetu yamepanda kwa asilimia 100.

"Watalii wengi wameongezeka baada ya hiyo filamu kuzinduliwa na kutangazwa katika mataifa makubwa duniani. Katika kipindi cha nusu mwaka, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, tumeweza kuingiza watalii zaidi na kupita kiwango kwa mwaka 2021.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuicheza filamu hii ambayo ndani ya kipindi cha miezi sita tu, tumeweza kuingiza mapato zaidi ya mwaka mzima uliopita. Filamu imeleta manufaa makubwa kwetu Watanzania, kwa kuwa tunaamini itaongeza zaidi pato la taifa," alisema Kiemi.

Aidha, aliiomba serikali ya Mkoa wa Tanga kuwapa ushirikiano katika kukamilisha ujenzi wa malango mawili yaliyoko eneo la Umba, Wilaya ya Mkinga na eneo la Mnazi, wilayani Lushoto, ambayo yatakapokamilika yatarahisisha shughuli za utalii.

Ofisa Utalii wa Hifadhi hiyo, Raymond Laban, alisema hifadhi hiyo iliyoanzishwa mwaka 2008, ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 3,245 ina wanyama wa aina mbalimbali ambao wengine hawapatikani katika hifadhi nyingine nchini.

Hifadhi hiyo iko katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, kwa Mkoa wa Tanga imepakana na Wilaya za Mkinga, Lushoto na Korogwe na Mkoa wa Kilimanjaro imepakana na Wilaya za Same na Mwanga.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga (RAS), Sebastian Masanja, alisema lengo lao kwa sasa ni kuhakikisha kuwa watendaji wa mkoa huo, wanazifahamu vizuri hifadhi zinazowazunguka.

# TASAF, UNICEF watoa msaada wa taulo za kike 12,943

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WANAFUNZI wa kike 12,943 wanaotoka kwenye kaya maskini zilizoko katika Halmashauri ya Arusha, ambao walikuwa hawana uwezo wa kununua taulo za kike wamepatiwa msaada wa taulo hizo zitakazowawezesha kujisitiri.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Seleman Msumi, taulo hizo zimetolewa kwa ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Shirika la Umoja Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF).

"Wasichana waliopewa taulo hizo ni wale wanaonufaika pia na mpango wa kunusuru kaya maskini. Tunaamini kwamba taulo hizi zitawasaidia wasichana hao kwa kuwa na hedhi salama na isiyokuwa na vikwazo.

"Serikali inahakikisha kila mwanafunzi anahudhuria masomo mwaka mzima na bila kuwapo kwa kikwazo chochote. Rai yangu, mtunze vifaa hivi, kwa kuwa vitawasaidia kufikia malengo yenu katika elimu,"alisema Msumi.


Alisema vifaa hivyo ni mkakati wa serikali wa kuhakikisha wanaweka mazingira bora na rafiki kwa wanafunzi wa kike kupata elimu bila kukumbana na tatizo lolote sambamba na kuhakikisha watoto wote wanahudhuria masomo hasa kipindi cha hedhi.

Mratibu wa TASAF wa Halmashauri hiyo, Grace Makema, alisema ofisi yake ilipokea vifaa hivyo kwa ajili ya wasichana walio kwenye kaya maskini zinazonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini kwenye vijiji 88.

Catherini Felix, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Sokon II, alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakishindwa kumudu kuwanunulia watoto wao vifaa wakati wa hedhi.

Alisema wazazi na walezi wamekuwa wakishindwa kuwanunuliwa vifaa hivyo kutokana na kutokuwa na uwezo wa kifedha.

Lightness Maina mwanafunzi wa shule hiyo alisema: "Baadhi ya wasichana hushindwa kuja shuleni wakati wa hedhi kutokana na kukosa taulo za kike na kusababisha kushindwa kuhudhuria masoma na inachangia kushuka kitaaluma ukilinganisha na wavulana."




Mbunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki kutoka Tanzania, James Ole Millya (kushoto), akiapa kushika nafasi hiyo kwenye makao makuu ya Bunge hilo jijini Arusha juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Bonite yatoa zawadi shindano V.I.P

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPUNI ya vinywaji baridi jamii ya Coca Cola ambavyo vinazalishwa na Bonite Bottlers Ltd ya Moshi (BBL), imehitimisha promosheni ya shindano la V.I.P la mwaka 2022, kwa kuendesha droo maalum iliyowaibua washindi wa zawadi za seti ya runinga na sanduku za soda kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Singida.

Droo ya kuwapata washindi wa promosheni hiyo iliyoanza Novemba mosi, ilifungwa Desemba 20, mwaka huu baada ya kushuhudiwa na Mjumbe wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT).

Akizungumza jana wakati wa ufunguzi wa droo hiyo, Meneja Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers Ltd, Christopher Loiruk, alisema zawadi hizo zinalenga kuimarisha biashara na kurejesha faida kwa wateja.

Alisema wateja wanaonufaika ni wale ambao wanaonunua bidhaa za soda jamii ya Coca-Cola na kuuza bidhaa nyingi, huku akisisitiza kuwa BBL imejipanga kuhakikisha inawasaidia wateja wake kuboresha biashara zao.

"Bonite Bottlers Limited kwa kutambua mchango wa wateja hawa, tumeamua kuwapa zawadi hizi ili ziweze kuwasaidia katika ukuzaji wa biashara zao. Hata anayetaka kuwa mteja wetu, tunamwezesha vitu mbalimbali kama majokofu, meza viti na vitu vingine, mradi tu biashara yake iweze kukua," alisema.


Kwa mujibu wa Loiruk, katika bahati nasibu hiyo kwenye kila mkoa zimetolewa runinga tisa, sanduku 50 za soda kwa washindi watatu, na nyingine 100 kwa washindi watatu, hivyo kufanya jumla ya washindi wote kuwa 45.

Alisema: "Niwaombe tu wateja wetu ambao hata kama leo hawajabahatika wasikate tamaa. Kwa sababu tunawathamini na hata hivyo tutawapa vinywaji zikiwamo soda na maji, waende wakasherehekee na familia zao msimu huu wa sikukuu."

Evergreen Mshana ambaye ni mmiliki wa duka la vinywaji baridi la Mshana Shop lililoko Kijenge jijini Arusha, alisema anajisikia furaha kuwa mmoja wa wanufaika wa bahati nasibu hiyo.

"Hii bahati nasibu imeendelea kunisogeza kibiashara, nimejipatia sanduku 100 za soda, ambazo si chini ya shilingi milioni moja. Nawasihi wafanyabiashara wenzangu kuendelea kununua bidhaa za Bonite, kwa sababu hakuna ujanja ujanja, kila mshindi kashinda kihalali," alisema.

Aidha, Jackline Mashim, mshindi wa seti ya runinga ambaye ni mmiliki wa Ndafu Bar ya Mkoa wa Kilimanjaro, alisema zawadi hiyo aliyoipata itamsaidia katika biashara yake ya vinywaji kwa vile soda ndiyo nyenzo mojawapo katika kuwavutia wateja.





# OSHA yaagizwa kupanua wigo wa programu atamizi

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ameiagiza Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA), kupanua wigo wa programu atamizi za wajasiriamali wadogo ili kuyafikia makundi mengi zaidi, hasa sekta za uzalishaji mali.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa OSHA na kueleza kuwa nia ya kutaka kufanyika kwa maboresho hayo ni kuiwezesha sekta isiyo rasmi kupiga hatua kubwa kiuchumi.

Hotuba yake ilisomwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya OSHA, Dk. Adelhelm Meru.

"Ninawaagiza kupanua zaidi wigo wa programu atamizi ya wajasiriamali ili muweze kuyafikia makundi mengi zaidi ya wajasiriamali wadogo katika sekta zote kiuchumi.

"Tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia sana nchi yetu kwa kuwa sekta isiyo rasmi ina makundi mengi ya wajasiriamali wadogo na ambayo inaajiri idadi kubwa ya Watanzania," alisema Dk. Meru.

Zaidi alisema: "Natambua kwamba taasisi hii yenye dhamana ya kulinda nguvukazi ya taifa letu bado ina kazi kubwa ya kufanya kwa vile maeneo ya kazi hapa nchini ni mengi na yanazidi kuongezeka kila siku.

"Hivyo tunahitajika kujituma zaidi na kuwekeza zaidi katika miundombinu na rasilimali muhimu zitakazotuwezesha kufikisha huduma hizi muhimu za masuala ya usalama na afya kwa Watanzania wote."

Dk. Adelhelm Meru alisema OSHA kwa mwaka wa fedha 2021/2022, iliwafikia wachimbaji wa madini na wajasiriamali wadogo 11,204.

Awali Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22 walitekeleza majukumu kikamilifu na hivyo kuvuka baadhi ya malengo iliyojiwekea.

"Tulifanikiwa kusajili maeneo ya kazi 7,260 ukilinganisha na lengo la kusajili maeneo ya kazi 7,000 na hivyo kufikia asilimia 103.7. Mafanikio mengine ni pamoja na kufanya kwa ukaguzi 217,102 ukilinganisha na ukaguzi 200,000 zilizopangwa kufanyika.

Alisema kwenye kupima afya OSHA ilifanikiwa kuwapima wafanyakazi 252,733 zaidi ya lengo walilojiwekea na kuwapima wafanyakazi 250,000, kutoa mafunzo kwa maofisa 14,661 ikilinganishwa na maofisa 10,000 waliolengwa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Jamal Katundu, aliwataka watumishi wa OSHA kuendelea kuchapa kazi huku akiwahakikishia kuwa ataendelea kushirikiana na viongozi wa taasisi hiyo kutatua matatizo wanayokutana nayo katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Nitumie fursa hii kuwahakikishia kwamba sisi viongozi wenu tupo pamoja nanyi na tutajitahidi kwa kadri inavyowezekana kusaidia kutatua matatizo yaliyoainishwa ili kuiwezesha taasisi yenu yenye dhamana kubwa ya kulinda nguvukazi ya taifa kuweza kufanikisha malengo yake.

"Hivyo nisisitize kila mmoja wetu kuchapakazi pamoja na kuzingatia weledi na maadili ya utumishi wa umma kwa maslahi mapana ya OSHA na Tanzania kwa ujumla," alisema Prof. Jamal Katundu.

Agenda kuu ya kikao hicho ilikuwa ni kutathmini utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 pamoja na nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

# Vifo vitokanavyo na uzazi K'njaro vyapungua

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imesema idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi mkoani Kilimanjaro imepungua kutoka 66 mwaka jana hadi kufikia 38 kwa mwaka huu.

Jana Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu, alisema ahueni hiyo inatokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na wadau ikiwamo uelimishaji wajawazito kuhudhuria kliniki.

Babu alitoa takwimu hizo wakati wa uzinduzi wa mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga maarufu kama 'M-mama' ambao lengo lake ni kumsaidia mama anapopata dharura.

Alisema mfumo huo utahakikisha zahanati, vituo vya afya na wateja wenye dharura, hasa wajawazito walioko majumbani wanapata usafiri wa dharura utakaokuwa ukipatikana kwa wakati wote.

"Tutachagua na kuwatambua wamiliki wa magari katika kila kata na kuingia nao mikataba kupitia halmashauri, madereva wataingia kwenye mfumo wa M-mama na watahusika kutoa usafiri pindi magari ya kubeba wagonjwa yatakapokosekana," alisema.

Alisema lengo la mfumo huo ulioanzishwa na serikali na wadau wa Maendeleo Vodacom/Vodafone ni kuhakikisha kinamama wajawazito wanafika kwenye vituo vya afya kwa wakati na kupata huduma.

Alisema Mkoa wa Kilimanjaro una magari 30 ya kubebea wagonjwa yanayofanya kazi za dharura, magari 13 ya serikali na 17 ya taasisi binafsi lakini bado kuna upungufu wa usafiri, hivyo anaamini mfumo wa M-mama, utasaidia kumaliza tatizo hilo.

Kaimu Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Kilimanjaro, Anne Shuma, alisema baadhi ya wajawazito wanajifungulia nyumbani na wengine njiani hasa katika Wilaya za Same, Mwanga na Siha, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa usafiri wa kuwafikisha kwenye vituo vya afya.

Alisema: "Kuanzia Januari hadi Desemba kuna vifo 38 na sababu ya vifo hivyo ni pamoja na kupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua, kifafa cha mimba, vifo vya watoto vimepungua kutoka 416 hadi 384," alisema.

Mfumo huo umeanza kutumika tayari katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga na umefanikiwa kwa asilimia 27 na kwa Mkoa wa Kilimanjaro, utaanza kutumika baada ya miezi mitatu kuanzia sasa.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Leopord Fungu, akiteremka kwenye basi baada ya kutoa elimu kwa abiria pamoja madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani juzi wilayani Korogwe. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mameneja NHC watakiwa kuingia ubia na wawekezaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwan Kikwete, amewaagiza mameneja wa mikoa wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuanza kuingia ubia na wawekezaji, kujenga miradi ya nyumba za makazi na biashara ili kutanua wigo wake wa uwekezaji.

Alitoa maagizo hayo jana katika Manispaa ya Moshi alipotembelea maeneo yatakayoingiwa ubia kati ya NHC na wawekezaji.

"Jambo la kwanza muhakikishe kwamba miradi ya nyumba itakayoingiwa ubia na wawekezaji, mnaisimamia kikamilifu ili iweze kutekelezwa kwa ufanisi kwa faida ya taifa. Serikali inapenda kuona NHC mnajenga ubia imara na wawekezaji.

"Mkifanya hivyo, mtasaidia ukuaji wa sekta ya nyumba ambayo ni moja ya sekta muhimu hapa nchini. Hata hivyo, nitayatembelea maeneo yote yaliyotengwa na NHC Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya uwekezaji," alisema Ridhiwan.

Alisema Watanzania bado wana mahitaji makubwa ya nyumba za kuishi, nyumba za biashara na ofisi, hivyo kuagiza mameneja wa mikoa kuhakikisha maeneo yote yanatangazwa ili kuwaalika wadau wengi zaidi kuwekeza.

Ridhiwan alisema serikali inatambua makazi ni jambo muhimu kwa maendeleo ya taifa, ndiyo maana imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuwezesha sekta ya nyumba kuwa endelevu na yenye tija kwa wananchi.

Akitoa taarifa kuhusu maeneo ya uwekezaji ya ubia, Meneja wa NHC mkoani Kilimanjaro, Juma Kyaramba, alisema mkoa huo umetenga maeneo matatu, ambayo yameshatangazwa kwa ajili ya kuingia ubia na wawekezaji.

"Tumetenga maeneo matatu ambayo ni kiwanja namba 4, kitalu E, Barabara ya Sekoture, kiwanja namba 51 kitalu C kilichoko Barabara ya Mawenzi na kiwanja namba 97 kilichoko Barabara ya Market. Viwanja vyote tulivyo vitangaza tunatarajia kupata wawekezaji wengi," alisema Kyaramba.

Kyaramba alisema wamefungua milango kwa wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi hivyo anaamini ubia huo utasaidia kupunguza tatizo walilokuwa wanakabiliana nalo la mrundikano wa maombi ya wapangaji.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Mkoa wa Kilimanjaro, Leonard Msafiri, alisema Watanzania wengi wana hitaji kubwa la nyumba za kuishi, hivyo NHC haliwezi kujenga nyumba za kutosheleza mahitaji ya wananchi na ndiyo maana imeanza kushirikiana na sekta binafsi katika miradi yake.



Ukurasa 15

## WASICHANA MORO & UKATILI JINSIA ... Mwenyekiti aja juu kuoza binti, Ofisa Ustawi ang'aka sumu ngoma ya Mkole



## SAFARI YA KIJINSIA MIKOA SABA... Kote alikopita waziri ameibua'madudu' yamuweka rehani mama na afya yake

Ukurasa 16

# Wataalamu wa Jakaya Kikwete: Wenye shida moyo 60% hufika wamechelewa

**Na Pendo Thomas, Mwanza**

Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, imesema asilimia 60 ya watu wanaowapokea wanakuwa wamefikia hatua mbaya ya magonjwa ya moyo. Kutokana na kuishi muda mrefu pasipo kutambua hali zao, hivyo kujikuta wakilazimika kutumia gharama kubwa zaidi kwenye matibabu, ambazo zingeweza kupungua kama wangejua hali zao mapema.

Akielezea kuhusu wagonjwa wa moyo wanao pokelewa katika taasisi hiyo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Dk.Peter Kisenge, anasema kwa siku wanawaona wagonjwa wastani wa 400, wengi wao huwa tayari moyo umefikia hatua ya kutokutenda kazi vizuri au misuli imeshatanuka .

Anasema katika utendaji wao wa kazi, wamebaini uwepo wa watoto wenye matundu kwenye moyo, lakini wazazi hawana uelewa kuhusu ugonjwa huo, hivyo wanawaomba wazazi kupeleka watoto kufanyiwa uchunguzi, pindi wanapoona dalili kama za kuumwa kifua, kukohoa kila mara ,mtoto anashindwa kukua vizuri na anachoka sana anapocheza na wenzake. Katika kusogeza huduma kwa wananchi, timu ya madaktari kutoka taasisi hiyo wameanza kutembelea mikoa mbalimbali kutoa huduma, ikiwa ni hatua ya kusaidia wananchi kupata huduma karibu, ikiwamo ushauri wa kiafya.

"Mfano tumeenda Geita tumegundua watoto 37 wenye matatizo ya matundu kwenye moyo na wazazi wao walikuwa hawajui, sisi tumewaambia wawalete Jakaya Kikwete, tunaweza kuyaziba na mtoto anapona kabisa," anasema Dk.Kisenge.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Dk. Peter Kisenge.

Pia, anafafanua kuwa endapo watu wakifanya vipimo angalau mara moja kwa mwaka kujua afya zao, inasaidia kubaini matatizo mapema na kupunguza madhara makubwa pamoja na gharama za matibabu ambazo kwa wastani inafika Sh. milioni 25 hadi 45, pale mtu anapopelekwa kutibiwa nje ya nchi.

Anaeleza, kwa sasa serikali imeboresha kwa kiasi kikubwa huduma katika taasisi hiyo, hivyo imewezesha asilimia 96 ya wagonjwa wa moyo kutibiwa nchini na asilimia nne tu ndio hupelekwa nje ya nchi wakati wakitibiwa na inawagharimu wastani wa shilingi milioni 15.

Dk.Glory Manyangu wa Magonjwa ya Moyo, kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, anasema jamii inatakiwa kuzingatia maisha ya kawaida, ambayo mtu akiyafuata inamsaidia kujikinga na magonjwa kama kiharusi, kupumua, moyo, kichwa,ubongo na figo.

Moja ya njia ni bora za kukabili anataja inajumuisha kula chakula bora, kuacha kutumia bidhaa za tumbaku, kufanyisha mwili kazi na kupima kila mara sukari, shinikizo la damu na wingi wa lehemu kwenye damu yake.

Vilevile anasistiza watu wanapaswa kutumia kiasi kidogo cha mafuta, ili kupunguza lehemu kwenye damu na kuzingatia aina ya mafuta anayotumia pamoja na kupunguza matumizi ya vyakula vyenye sukari, akisema theluthi ya wagonjwa wa kiharusi na magonjwa ya moyo, husababishwa na shida ya lehemu kwenye damu.



Daktari wa Magonjwa ya Moyo, Glory Manyangu, kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda, Bugando. **PICHA ZOTE: PENDO THOMAS.**

Kaimu Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, Varelia Milinga, anasema kutokana na ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza wanaendelea kuelimisha jamii kuachana na tabia zinazo changia magonjwa hayo pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya utakaoboresha utoaji huduma.

Pia, anasema mwaka ujao wanalenga kufanya utafiti utakaotambua idadi ya Watanzania wenye aina fulani ya ugonjwa pamoja na kubaini idadi ya wanaotumia tumbaku na vileo hatua itakayo wezesha kuchukua hatua za kudhibiti kulingana na ukubwa wa tatizo .

Anasema hadi sasa mpango huo wamefanikiwa kuandaa mtaala wa mafunzo kwa watoa huduma ngazi ya vituo vya afya na zahanati ambako huduma hizo zilikuwa hazitolewi moja kwa moja lakini kwa sasa huduma hizo zinatolewa kwani kuna watoa huduma wenye elimu ngazi ya shahada katika vituo vya afya na Zahanati

Mratibu wa Utafiti na Machapisho Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, James Kengia, anasema mwaka 2022 /2023 wameratibu kwa nchi nzima afua zote muhimu za magonjwa yasiyo ambukiza zinazo pelekwa kwenye halmashauri zote.

Anaeleza takribani shilingi bilioni 3.3 zilitengwa kwenye bajeti hiyo, kwa kuzingatia hali halisi ya tatizo katika eneo husika ikiwa ni pamoja na kuratibu uwepo wa huduma zote muhimu kama huduma tiba na kinga kwenye vituo pamoja na utoaji elimu katika jamii ili kutoa uelewa utakao saidia kupunguza ongezeko la magonjwa yasiyo ambukiza.

AFYA

## HOSPITALI BUGANDO VITANI....

# Magumu ya kukabili kansa ya watoto kuanzia uponyaji, hadi gharama yake

**Na Pendo Thomas, Mwanza**

MWANANGU alianza kuugua mnamo mwaka 2016, anakuwa anachemka sana tukampeleka Hospitali ya Wilaya ya Tarime, wakampatia matibabu, tukaambiwa tuwe tunamrudisha hospitali na baadaye wakasema labda ana UTI (mkojo mchafu). Akaendelea kuwa na hali hiyo, baadae akiwa na miaka mitano, jicho lake likabadilika likatoa rangi za ajabu ajabu," anatamka Martha Petro, mkazi wa mkoani Mara.

Mama huyo anasimulia walivyoendelea kupata matibabu ya jicho hospitalini hapo pasipo mafanikio na jicho likaanza kuweka rangi nyeupe na ukungu, ndipo mume wake akaamua kusitisha matibabu hospitalini na kumpeleka kwa mganga wa kienyeji.

Anaeleza ndani ya miezi mitatu ya matibabu kwa mganga wa kienyeji, hali ilibadilika jicho likavimba, hatua iliyoibua ugomvi kati yake na mume baada ya kulazimisha mtoto wake asitishiwe matibabu ya kienyeji, watafute suluhisho zaidi hospitalini kubaini chanzo cha tatizo hilo, kwani jicho linazidi kuharibika.

Martha anaeleza baada ya mvutano huo, alifanikiwa kumrudisha hospitali mtoto huyo na kuandikiwa kupelekwa Hospitali ya Rufani Kanda Bugando, ambako alifanywa vipimo na kubainika mtoto wake, alikuwa na ugonjwa wa saratani.

"Natamani jamii ielewe juu ya huu ugonjwa na iachane na kuhusianisha na imani za kishirikina kwani mimi mtoto wangu alikuwa na hali mbaya, lakini baada ya kupata matibabu sahihi sasa anaendelea vizuri," anasema Martha.

Ili kufanikisha matibabu ya mwanangu, ilinibidi nianze kuchangisha fedha angalau kutokana na matibabu kuwa endelevu na yanayohitaji gharama kubwa, kwani kila baada ya muda mfupi inatakiwa kurudi hospitali kuendelea na matibabu zaidi.

Anasimulia, tangu mtoto wake aanze kupata matibabu ya ugonjwa wa saratani mwaka 2017 maendeleo yake sasa ni mazuri anaendelea na masomo, japo anakiri wakati anaanza matibabu kwa muda wa siku tano, alikuwa hali chakula wala kunywa maji, huku nywele zikiwa zimenyonyoka, jambo lililompa shaka. Anasema daktari alimpatia ufafanuzi kuwa hayo ni matokeo ya matibabu na hali ingebadilika.



Jengo la kuhudumia wagonjwa wa kansa, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, jijini Mwanza.

Baraka Elias, mkazi wa Runzewe, wilayani Bukombe, Shinyanga, pia ana mtoto aliyebainika kuwa na saratani, anasema mwanawe aliota uvimbe kifuani wakati akiendelea kutafakari nini chanzo na hatua za matibabu yake, hali iliendelea kubadilika, akaenda hospitalini alikoambiwa kwa vile uvimbe ni mdogo wamfanyie upasuaji.

Mwezi mmoja baada ya upasuaji, uvimbe ulimrudia kwa kasi na ikabidi arudi hospitali. Walivyoona tatizo hilo, wakampa rufaa kwenda Hospitali ya Rufani Nkinga mkoani Tabora, ambako nako walisema ni tatizo kubwa akaelekezwa rufaa ya kwenda katika hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Mwanza.

Anaeleza walivyofika Hospitali ya Bugando, walianza taratibu za matibabu wakiwa wodini kwa kipindi cha wiki tatu na baadaye majibu ya vipimo yalionyesha kuwa mtoto wake ana ugonjwa wa saratani.

''Ikabidi nimuhoji daktari, sasa huu ugonjwa ni mara ya kwanza kusikia kama mnasema mwanangu ana saratani, je matibabu yapo? Akaniambia matibabu yapo, usiwe na wasiwasi, ila kuna masharti tutakupa kama utazingatia mtoto atapona, usipozingatia hatapona''akaeleza Baraka.

Anataja miongoni mwa masharti aliyopewa, ni kuzingatia tarehe za kurudi hospitalini kama maelekezo ya daktari yatakavyoeleza pamoja na kumpeleka mtoto hospitali kila siku kusafishwa kidonda alichokipata, baada ya kufanyiwa upasuaji, kwani hakikushonwa, mambo ambayo aliyatekeleza.

### MADAKTARI BINGWA

Daktari mbobezi wa magonjwa ya saratani ya damu kwa watoto kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, Heronima Kashaigili, anasema saratani inavyozaliwa kwa watoto na wakubwa, ni sawa japo saratani za watoto zinatengenezwa bado akiwa tumboni na chembe hizo zinakuwa hazijakomaa, hivyo kutibika kwake ni rahisi.

"Kwa mwaka tunapokea watoto wenye saratani 250 na zaidi ya asilimia 50 huwa wamecheleweshwa kwenye matibabu hivyo kusababisha madhara makubwa wakati kama wangewahishwa wangeweza kupona,' anasema Dk. Heronima.

Anafafanua alichokibaini baada ya mahojiano na baadhi ya wazazi hospitalini hapo, ni kwamba bado jamii haina uelewa wa kutosha kuhusiana na ugonjwa wa saratani, kwa watoto hivyo wengine wanahusianisha na dalili zisizo za kawaida na imani za kishirikina au magonjwa mengine.

Dk. Heronima anasema kuna watu wanapoambiwa watoto wao wana ugonjwa huo, huonyesha wazi kutokuamini na wanageukia tiba za kienyeji, hivyo wanapoondoka hospitalini hawarudi kuendelea na matibabu.

Kuhusu gharama za matibabu ya saratani hutofautiana kulingana na aina zake, saratani ya figo ndio yenye bei nafuu kuliko zingine kwani hadi mgonjwa kupona inamgharimu kuanzia milioni tatu hadi tano. Gharama huchangia wazazi wengi kushindwa kuendelea na matibabu hayo.

Rina Luhaga, ni daktari bingwa wa magonjwa ya watoto kitengo cha saratani, anasema dalili za saratani kwa watoto zinafanana na dalili za magonjwa mengine, hivyo hali hiyo husababisha wazazi kushindwa kubaini mapema au kumpeleka mtoto kwenye matibabu mengine.

Anataja viashiria ambavyo mzazi anapaswa kuwa navyo ni tumbo kuvimba, kutokwa jasho jingi usiku, kupungukiwa damu, macho kupata ukungu, uvimbe shingoni na kupungua uzito, ingawaje inasisitizwa kwamba dalili hazimaanishi moja kwa moja mtoto huyo ana saratani.

Kitabibu, Daktari Rina anasema, saratani nyingi kwa watoto zinahitaji upasuaji. Anaendelea: "Dalili hizi zinafanana kabisa na dalili za magonjwa mengine, hivyo hadi vipimo vifanyike ndio tuseme hii ni saratani ya aina fulani. Ni vyema wazazi wawahi kupata matibabu husika pindi wanapoona hali isiyo ya kawaida."

### ANGALIZO LA WHO

Shirika la Afya Duniani (WHO), linatamka kupitia ripoti ya mwaka juzi, 2020, kwamba kila mwaka kuna watoto 400,000 hugundulika kuwa na saratani, huku katika nchi zenye uchumi wa juu asilimia 80 ya watoto baada ya kupata matibabu wanapona, ilhali katika nchi zenye uchumi wa kati na chini, asilimia 20 hadi 30 ndio wanaopona.

Mpango wa Taifa wa WHO wa Saratani ya Watoto, ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 duniani, asilimia 60 ya watoto wenye saratani waweze kuishi na kupunguza maumivu yanayosababishwa na ugonjwa huo.


Mtaalamu katika Hospitali ya Rufani Bugando, akionyesha vifaa vya kuhudumia wagonjwa wa saratani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

## WASICHANA MORO & UKATILI JINSIA ...

# Mwenyekiti aja juu kuoza binti, Ofisa Ustawi ang'aka sumu ngoma ya Mkole

**Na Christina Haule, Morogoro**



Baadhi ya wanafunzi wa shule ya Sekondari Tomondo, wakionyesha igizo la ukatili wa kijinsia mkoani Morogoro. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE.**

MKOANI Morogoro wanavutana shati kuhusu adha ya jinsia na ukatili wake kwa mabinti zao. Matokeo yake, inawaumiza kuanzia saikolojia, afya hadi uchumi.

Sasa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Lucas Lemomo, anakuwa mkali akikemea wazazi wanaokataza watoto wasifaulu darasa la saba, kwani hawana uwezo wa kuwaendeleza kimasomo. Mbadala ni kwamba wanawaingiza katika ndoa, jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao.

Lemomo, ambaye ni Diwani wa Matuli, anasema jitihada za kiserikali zikakutana na vigingi vya wazazi kuwazuia watoto kufaulu, jambo lisilo na faida. Anasema dunia ilikofika ya Sayansi na Teknolojia, inahitaji robo ya Watanzania wawe na elimu ngazi ya chuo kikuu.

Anatumia mfano hata daktari anayeutumikia umma kila mtu na wasifu wake, chimbuko lake alisomeshwa na hiyo inajenga maana pana ya haja ya mzazi kuwa na wivu wa maendeleo kumsomesha watoto wake, akinyooshea kidole jamii ya mkoani Morogoro iliyo mstari wa mbele kuozesha mabinti zao.

"Unakuta mtoto kazuiwa kufaulu na kuozwa kwa mahari ya shilingi 70,000, hata miaka mitatu haijaisha ameshaachwa na anarudi akiwa na mtoto, hapo mzazi utakuwa umepata faida gani, kama sio mzazi kuchukua mzigo mkubwa wa kubaki kulea mtoto na mjukuu pamoja?" anahoji Lemomo.

Lemomo anasema umuhimu wa jamii kusomesha unamuwezesha binti ajitegemee baadaye, pia kuwasaidia wazazi wakiwa wamechoka kiumri, huku akienda mbali kutaja uozeshaji binti ni 'ukatili wa aina yake' wenye sura mpya kila kukicha.

### MKASA WAKE

Lemomo ana ushuhuda wa yaliyomkuta akiwa na umri wa miaka mitano, kaka yake aliyekuwa shule kidato cha sita alifariki ghafla, hali iliyowasababisha wana - ukoo kukaa wakidai ni tukio la kichawi hawatasomesha mtoto katika familia kuanzia hapo.

Anasema alipofika umri mwafaka alianza 'kujiiba' kwenda shule na alipofika darasa la sita, wana ukoo walikaa tena na kuazimia kumkana na kumtenga kwa 'kumtolea laana ya ukoo' kwamba hawamtambui tena kwa kuwa ameamua kusoma, hata yeye Lemomo akaamua kwenda kuishi kwa rafiki zake.

Mwenyekiti huyo anafafanua alipofika kidato cha pili alienda likizo kwa rafiki zake Dar es Salaam, ndipo matokeo yalipelekwa nyumbani kuwa, alikuwa amefaulu vyema, wakati huo ndugu zake wakihisi ameshapotea baada ya kumfukuza. Hata hivyo, mama yake akawa na huruma, akamtafuta na kumchukua aendelee na masomo.

Kupitia simulizi hiyo, Lemomo anawaasa wanafunzi waamini hakuna cha kuwazuia ikiwamo kuwalazimisha kuolewa, anahimizia hoja kwamba kumnyima mtoto elimu ni kumuondolea urithi wa kudumu.

### HALI MBAYA

Hapo Lemomo anarejea mwaka huu, kuna kesi 82 mahakamani za ukatili kijinsia zimeripotiwa wilayani Morogoro, kati yake 26 ni za watoto na 13 zimekwishatolewa hukumu; kesi 52 za wanawake, 22 zimeshatolewa hukumu na zilizobaki 30 zipo katika hatua mbalimbali.

Anasema, suala la ukatili linaendelea kuiumiza jamii kwa kuwagusa zaidi watoto na vijana na mwaka huu kwenye kijiji cha Bwakila, kuna mkasa wa mwanafunzi wa darasa la nne alibakwa hata akapoteza maisha, huku katika kata ya Kiroka, kuna mauaji ya kijana kukatwa mapanga hata akafariki.

Pia, anazungumzia ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto unaendelea kuwepo ubakaji, mimba za wanafunzi, vipigo kwa wanawake, ukeketaji wafugaji, kwamba ni ukatili wa kumnyima haki mwanamke asiishi kwa amani.

Hivyo anaupongeza Umoja wa Mataifa kwa kutambua umuhimu wa maadhimisho hayo kwa kutenga siku maalum duniani za kutoa elimu ya kutokomeza ukatili wa kijinsia. Kaulimbiu ya mwaka huu 'kila uhai una thamani, tokomeza mauaji ya wanawake na watoto'.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Lucas Lemomo, akinena jambo katika kikao kupinga ukatili wa kijinsia.

### KAULI TAHADHARI

Lemomo anaomba wadau wote wa masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia, yakiwemo mashirika na taasisi zisizo za kiserikali, watambue kuwa bado wana wajibu wa kuendelea kushiriki utoaji elimu, ili kuisaidia jamii kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Pia, anawataka wazazi kuwasikiliza watoto wanapowafikishia malalamiko ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia, kwani ukimya unaonyesha kuchangia kuwapo madhara makubwa katika kuzalisha ukatili kwa watoto wao.

Aidha, anakemea tabia ya watoto kulazwa na ndugu wa karibu katika chumba kimoja, nayo ni chanzo cha kuwasababishia watoto kuingizwa kwenye ukatili wa kijinsia, ikiwemo kubakwa na kulawitiwa.

Mwanafunzi wa shule ya Sekondari Tomondo mkoani hapa, Jeniffa George, anawaomba wazazi wawaache wasome, kwa sababu elimu inachangia kuwakomboa na mengi yanayowakabili kimaisha.

### WENYE USHUHUDA

Ofisa Mwezeshaji wa Shirika la Kikristo la Kuhudumia Wakimbizi nchini (TCRS), Gasper Werema, anasema wamefanikiwa kutoa elimu katika vijiji 15 wilayani Morogoro, tangu mwaka 2006.

Werema anaeleza TCRS inashughulikia masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia, kwa kuanzisha vikundi vijijini, ikitoa vitendea kazi kama simu za mikononi, kwa ajili ya kuwasiliana na polisi panapotokea matukio ya ukatili wa kijinsia yanayoonekana kuzaa matunda kwa matukio mbalimbali, polisi kufikishiwa taarifa kwa wakati.

Anayataja baadhi ya matukio hayo, mwaka 2021 kwenye kata ya Tawa, la Mwalimu wa shule kumpa mimba mwanafunzi na familia ilichukuliwa hatua baada ya mwalimu kukimbia.

Meneja wa TCRS, Rehema Samwel, anasema wamefanikiwa kuunda Kamati za Ulinzi wa Mama na Mtoto (MTAKUWA) katika vijiji 15, sambamba na kutoa elimu ya kukabiliana na kupinga ukatili wa kijinsia, inayoanza kuzaa matunda katika kata za Tomondo, Mikese na Kiroka, ili kusaidia kupinga ukatili wa kijinsia kwa jamii.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilaya ya Morogoro, Frolence Mwambene, anaiomba halmashauri kuweka sheria ndogo zitakazozuia masuala ya ngoma za Mkole, mahsusi kuwaandaa mabinti 'kunema', kwa sababu yameonekana kuchangia ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Florence anasema ngoma ya Mkole kwa dhana ya 'kumfunda mwali' imekuwa ikileta ukatili wa kijinsia, hasa kwa watoto kuachwa maziwa wazi wanapofanyiwa Mkole na kuleta ushawishi kwa wanaume kwa kuanza kufikiria kuwafanyia ukatili kwa kuwafuatilia hali, inayowasababishia ndoa na mimba za utotoni.

AFYA

## SAFARI YA KIJINSIA MIKOA SABA...

# Kote alikopita waziri ameibua 'madudu' yamuweka rehani mama na afya yake

**Na Christina Mwakangale**




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akisalimiana na Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Selemani Bishagazi, mmoja wa washiriki wa ziara iliyofanyika mikoa saba, kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

UKATILI wa kijinsia ni masuala yanayopewa kipaumbele sasa kukabiliana nayo hasa kwa nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, huku mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa ikiwa na takwimu zinazoongoza kwa matukio hayo, ikiwaathiri zaidi wanawake, wasichana na watoto.

Kila mwaka dunia hutenga Siku 16 kupinga ukatili wa kijinsia, nchini wanaharakati na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum waliadhimisha siku hiyo kwa kampeni ya kuzunguka mikoa saba.

Kampeni hiyo iliyofika mikoa ya Pwani, Morogoro, Singida, Shinyanga, Geita, Mara na Arusha kupaza sauti na kupinga ukatili wa kijinsia kwenye maeneo hayo kwa kaulimbiu 'Kila uhai una thamani, tokomeza mauaji, na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.'

Miongoni mwa washirika wengine ni madawati ya kijinisa kwenye mikoa husika, SUMAUJATA, Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA) na Wasaidizi wa Kisheria.

Kwenye kampeni hiyo kupitia midahalo iliyohusisha wananchi kwenye mikoa hiyo ikiwamo maeneo ya shule, soko, penye wafanyabiashara tofauti kama vituo vya madereva waendesha bodaboda, bajaji, machinga, mama na babalishe, wachangia mada waliweka bayana wanayopitia na kuishi nayo na kugeuka utaratibu wa kawaida maishani mwao.

### WAANZA KUFUNGUKA

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, kinamama waliopo maeneo hayo, baadhi waliweka wazi namna utaratibu wa malezi ndani ya familia, ulivyobadilika na wanawake kuachiwa mzigo wa kulea familia huku waume zao kutotoa mchango wowote.

"Hivi mwanamke akiwa mvivu inatakiwa afanywaje kwenye familia, mwanaume mvivu, ameoa ana watoto, afanywe nini? Mwanaume anapewa jina la kichwa cha familia, lakini uhalisia haupo, mwanamke ndio nimebeba mzigo wote," anasema mwanamke mjasiriamali katika Soko la Kilombero, mjini Arusha.

Mkazi wa eneo hilo, Deogratius Shayo, anasema vitendo vya ukatili wanaishi navyo kila siku na kwamba watoto wengi wanaishi na kulala mitaani, akiomba utaratibu wa vituo maalumu kwa ajili yao uwepo.

Mmoja wa wakazi wa Tarime Mjini mkoani Mara, ambaye hakuwa tayari kutaja jina lake anasema awali hakubaini kuwafanyia ukeketaji watoto ni tatizo na kwamba baadhi ya maeneo yalifanya ukeketaji hata kwa mabinti 50 kwa siku hasa msimu wa matukio hayo Desemba.

Mwanamke aliyewahi kukeketwa, anachangia mada hiyo akisema zamani kukeketwa ilikuwa ni vitendo vya ufahari kwa msichana, ila hivi sasa 'amaeokoka'na mila hizo potofu akizipiga vita.

"Mimi nilikeketwa, nikachongwa na meno na mwanya, sasa hivi katika uzee wangu nimeokoka nimepata elimu. Lakini, kabla sijaokoka nilimfanyia ukeketaji binti yangu mmoja kutokana na mila, ila mtoto wangu wa mwisho sikumkeketa, tuache kuharibu watoto wetu," anasema bibi huyo katika eneo la Serengeti Shamba la Bibi, Tarime Mjini.

Mmoja wa wafanyabiashara eneo la soko la Kilombero mkoani Arusha, Alphonce, akizungumza kwenye mdahalo huo, anasema namna ya kuripoti matukio hayo ni changamoto kwenye jamii na kwamba wanawake wanaotendewa vitendo hivyo huhisi ni sehemu ya maisha yao.

"Hapa Kilombero kuna tatizo na rushwa ya ngono imetawala, kinamama ambao wanataka biashara yao iende hasa eneo la barabarani ambako kuna wateja, wanatoa rushwa ya ngono wanapewa eneo la biashara," anasema.

Washiriki wa kampeni kutoka mashirika tofauti, Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Selemani Bishagazi, anasema kampeni hiyo imebaini jamii kuathiriwa na vitendo vya ukatili jinsia, akifafanua vinaendelea katika maeneo hayo, ikiwamo ubakaji, ulawiti, ndoa za utotoni, ajira utotoni, rushwa ya ngono, ukeketaji, vipigo, matusi na utelekezaji familia.

Anaongeza kuwa, wanawake na watoto, wanandoa kunyimana unyumba, kutupwa wototo, kunyimwa chakula, ukatili kiuchumi, watoto kutopewa haki ya elimu na walemavu kubaguliwa, vyote ni ukatili wa kijinsia.

### TAARIFA KWA WAZIRI

Baada ya kampeni, Waziri mwenye dhamana, Dk. Dorothy Gwajima, anasema katika mikoa saba aliyotembelea, ametembelea makundi ya kijamii wakiwamo wanafunzi na walimu wa shule za msingi na sekondari, wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo sokoni, madereva malori ya kubeba mchanga, mabasi, daladala na magari binafsi; bodaboda, bajaji na baiskeli.

Anasema, kwa upande wa shule misafara yake ni 11 na shule tano zilikuwa sekondari na sita za msingi na jumla ya wanafunzi 4,482 walipata mafunzo. Kati ya hao wanafunzi wa kike walikuwa 2,307 na wakiume walikuwa 2,175.

Kwa upande wa jamii msafara huo, ulitembelea masoko sita na kituo kimoja cha mabasi, vituo 51 vya bodaboda, bajaji, baiskeli na jumla ya watu 13,245 walipata mafunzo, kati ya hao wanaume walikuwa 7,482, wanawake 5,000 na watoto 183.

Vilevile msafara ulihusisha uonyeshaji wa mpira wa miguu Kombe la Dunia na mechi tatu zilionyeshwa katika mikoa mitatu ya Morogoro, Singida na Shinyanga, watu 580 walihudhuria katika mechi hizo na kupatiwa elimu dhidi ya ukatili wa kijinsia, na mikakati ya kutokomeza vitendo hivyo.

Pia taarifa hiyo, inasema kampeni imebaini kuwa wasichana wanapokeketwa viungo vyao vinavyokatwa huuzwa kwa wafanya biashara wakubwa wa madini na wa samaki ambao wanaamini kuwa viungo hivyo vinaweza kutumika kuongeza wingi wa madini na samaki.

Aidha, viungo hivyo huuzwa kati ya shilingi milioni moja hadi milioni 20 kutegemea na wingi wa viungo vilivyopatikana. Inatajwa kuwa ni hali inayochochea vitendo hivyo, ikimaanisha tatizo la ukatili wa kijinsia ni zaidi ya mila na desturi kama ilivyozoeleka. Hivyo, kuna umuhimu wa serikali na wadau kutafiti ili kugundua wanaonufaika na biashara hiyo, hata wachukuliwe hatua za kisheria.

Vilevile, wananchi walitoa taarifa za kusambazwa kadi za mialiko ya sherehe za ukeketaji zilizotarajiwa kufanyika mwezi huu kati ya Desemba 10 hadi 20 katika vijiji vya Msati, Iganana, Kibanga, Songambele, Ronsoti wilaya ya Tarime na wengine walitarajiwa kupelekwa katika nchi jirani, ambako mila hizo nako zinafanyika.

Pia, kunaelezwa mikasa ya ukatili wa kiuchumi kwa baadhi ya wanawake wajasiriamali sokoni, wakinena namna waume zao huwafuata sokoni na kuwapiga na kuwanyang'anya fedha za mauzo, hivyo kuathiri mitaji yao, ilhali baadhi inatokana na mikopo ya serikali kwa wanawake.

Pia, wakati wa msafara jumla ya mashauri 125 yalishughulikiwa papo hapo na wanasheria pamoja na wasaidizi wa kisheria wa maeneo husika. Zipo kesi ambazo zilishughulikiwa zikamalizika na zingine zilikabidhiwa kwa maofisa maendeleo ya jamii na vyombo vya sheria watatue.

AFYA

## MWENYE ULEMAVU ANAYEWEZA

# Evodia Nchimbi: Dereva Bajaji anayevuka magumu ya hali yake, hadi mafanikio

**Na Pilly Kigome**



Evodia Nchimbi, akiwa kazini na chombo chake cha usafiri. **PICHA: PILLY KIGOME.**

EVODIA Nchimbi ni mwanamke mwenye mlemavu wa miguu, anayesimama mwenyewe katika kuijenga familia, bila ya kuwa na usaidizi wowote na anaitunza familia kwa kazi za mikono yake mwenyewe.

Mwanamke huyo anayevutia walio wengi wapitao na wafikao maeneo yake ya kazi kituo chake cha kazi Kivukoni, Dar es Salaam, haonyeshi kuchoka katika kazi yake japo ana mapungufu ya kimaumbile mwilini mwake.

Mama huyo mwenye familia ya watu wanne watoto wawili akiwemo na mdogo wake wa kike, ndiye baba na ni mama. Kila kitu kwa familia yake hiyo katika hali zote yaani afya, malazi na hata mavazi anategemewa yeye.

Ni mama mwenye historia ya kuongoza njia, asiyekata tamaa hata kama kuna mtu anajitokeza kumkatisha ama kumrudisha nyuma kimaendeleo, yeye ni mtu wa kutafuta nini afanye ili aweze kusonga mbele.

Safari yake kimaisha ya kuingia barabarani ilikuja baada ya kujiongeza na kwenda kusomea udereva katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Chang'ombe, Dar es Salaam kwa miezi sita na akabahatika kupata leseni ya udereva, ambayo inamsaidia kumuendeshea maisha hadi aliko sasa.

### ALIKOINUKIA VITANI

Anasema, awali alijitokeza mfadhili kutoka hospitali ya CCBRT jijini Dar es Salaam, aliyetaka kuwafadhili wanawake wawili walemavu, kwa kuwa, mfadhili huyo aligundua hata kazi ya udereva walemavu wanaiweza kufanya na kujiingizia kipato cha kila siku.

Evodia anaeleza kuwa mfadhili huyo aliguswa kuona kila anapopita katika baadhi ya barabara tofauti anakutana na walemavu wanaume pekee wanaendesha chombo hicho cha bajaji, hata akajitosa kutangaza ufadhili wa wanawake wawili walemavu, aweze kuwakopesha Bajaji waingie barabarani watafute riziki zao kwa kutumia usafiri huo.

Hapo ndipo nafasi hiyo akabahatika kuipata Evodia, akiwa na mwenzake mmoja aliyemtaja kwa jina la Mariam Mponji. Walikabidhiwa Bajaji hizo kwa njia ya mkopo na walitakiwa warudishe marejesho kwa hatua hadi deni litakapoisha bila ya riba.

Anasimulia safari ya maisha yake kwamba ni tukio lililomsahangaza sana hata hakuamini kilichotokea, japo ni kwa mkopo. Anasema, ni kwa sababu yeye hakuwa na uwezo wa kununua chombo hicho, ingawaje alitamani kwa kipindi kirefu. Mkopo huo alitakiwa alipe jumla ya shilingi milioni saba na makubaliano yao na mfadhili, ni kulipa shilingi 20,000 kwa siku.

Evodia anasimulia alipata ujasiri na kuingia barabarani, akisema ilimuwezesha kupata hela ya marejesho na ya kujikimu, kwa kuwa kipindi hicho kilikuwa na neema kubwa ya wateja waendesha 'Bajaji za Daladala' walikuwa wachache ikilinganisha na sasa hivi.

Mama huyo anasema, ni bahati mbaya katika kipindi hicho kabla ya marejesho ya hilo deni kumalizika, alipata bahati mbaya ya kuteleza kwake barazani na akaumia sana hata kuvunjika mguu.

Anaieleza hali hiyo kwamba alifika hatua mbaya, hakuweza kuingia tena barabarani kwa madhila ya kiafya ambayo ni nyongeza ya shida zake, juu ya ulemavu alio nao.

Hapo anaeleza kuwa hatua hiyo hakuweza tena kuendelea na kazi, kutokana na ugonjwa huo na ilimlazimu amtafute dereva wa muda, maarufu 'deiwaka' ili aweze kuendesha bajaji hiyo imsadie kumpatia marejesho ya lile deni.

Ni hatua anayosimulia alivyopata mkasa baada ya siku tatu kutoka kumkabidhi Bajaji hiyo iliibiwa na hali hiyo ilimvuruga sana, kwa kuwa ndio ilikuwa tegemezi katika kuendesha maisha yake ya kila siku.

Evodia anakiri ukweli wa kuibwa bajaji ile na katika katika uchunguzi ikagundulika kwa kushirikiana na ndugu na watu wengine wa karibu, wakamsaka mwizi huyo na baada ya miezi mitatu, alipigiwa simu Bajaji imeonekana Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Hapo anasema, akasafiri hadi mjini Moshi kufuatilia mali yake na akaikuta katika hali ya uchakavu na aliyekutwa nayo, hakuwa mwizi wa moja kwa moja. Mamlaka za dola zilimkamata kijana aliyekutwa na Bajaji, huku ndugu wakiahidi kumlipa mama huyo taratibu.

Anasikitika kwamba, hatua za ulipaji huo hazikudumu sana na akaagiza iletwe jijini Dar es Salaam katika hali yake hiyo ya uchakavu, akakiingiza barabarani, kisha baadaye akaifanyia matengenezo makubwa, walau kukinusuru hali yake.

Evodia anasema walau wakati huo hali yake iliimarika kiasi na hakukata tamaa na tayari, akipigana kufanikisha kupata mkate wake wa kila siku. Anasema ndipo alipopata wazo la kuingia benki na kufanikisha kupata mkopo wa kununua Bajaji nyingine kutoka benki, inayompa nafasi hadi sasa anaendelea na shughuli zake za kujitafuatia hadi sasa.

Hapo anataja mafanikio yake aliyoyapata kutokana na kazi yake hiyo, ikiwemo kujenga nyumba huko eneo la Mvuti jijini Dar es Salaam, pia anasomesha watoto wake na kutunza familia bila ya usaidizi wa mume.

AFYA

## WANAOKAMATA THELUTHI YA DUNIA;

# India inavyochuana kuipiku China kwa idadi kubwa ya watu duniani

**Na Mwandishi Wetu**

MNAMO mwezi Aprili mwaka huu, India ilitabiriwa kuipita China hata kuongoza kwa idadi ya watu duniani. Mataifa hayo makubwa ya Bara Asia tayari, sasa yanakadiriwa kuwa na zaidi ya watu bilioni 1.4 kila moja na kwa zaidi ya miaka 70 wamechukua zaidi ya theluthi moja ya idadi ya watu duniani.

Idadi ya watu China inabashiriwa huenda ikaanza kupungua mwaka ujao. Mwaka jana, watu milioni 10.6 walizaliwa, ikiwa ni zaidi kidogo kuliko idadi ya vifo.

Kiwango cha uzazi nchini India, pia kimepungua kwa kiasi kikubwa katika miongo ya karibuni, kutoka uzazi wa watoto watano mwaka 1950, hadi watoto wawili kwa kila mwanamke kwa sasa. Je, India itaipiku China, kutoka kileleni kwa idadi kubwa ya watu?

China ilipunguza kiwango cha ongezeko la watu kwa karibu nusu, kutoka ongezeko la asilimia mbili hadi asilimia 1.1 mwaka 1983. Wataalamu wa takwimu wanaoanisha mabadiliko hayo na wanachokitaja kuminywa kwa haki za binadamu; kampeni za kuzaa mtoto mmoja tu wakati fulani na kuwepo ndoa za baadaye na pengo refu kati ya watoto wanaozaliwa.

Prof. Tim Dyson, mtaalamu wa takwimu kutoka Shule ya Uchumi London, Uingereza, anasema India iliona ukuaji wa haraka hasa mwishoni mwa karne iliyopita na baada ya muda, viwango vya vifo vilipungua, umri wa kuishi uliongezeka na mapato yalipanda. Watu zaidi na hasa wanaoishi mijini huduma bora kiafya zinapatikana.

Anasema, mwaka 1952, India ilizindua mpango wa uzazi, wenye sera ya kitaifa hata kufika mwaka 1976 kukashuhudiwa kupungua kasi ya uzazi katika jamii na kuigwa na nchi za Mashariki mwa Asia kama vile Korea, Malaysia, Taiwan na Thailand, zilizozindua programu za idadi ya watu baadaye, hata kuongoza viwango vya uzazi na kupunguza vifo.

Prof. Dyson anasema, kupungua viwango vya kuzaliwa kumekuwa kwa kasi zaidi Kusini mwa India kuliko Kaskazini, ambako kuna watu wengi zaidi. "Inasikitisha kwamba sehemu kubwa ya India haijaweza kuwa kama India kusini."

Kuna takwimu kuwa, mmoja kati ya watu watano walio na umri chini ya miaka 25 duniani anatoka India. Pia, theluthi mbili ya Wahindi walizaliwa baada ya India kufanya uchumi huria mapema miaka ya 1990.



Jamii ya Wahindi waliokusanyika kwenye mitaa yao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### CHANGAMOTO ILIYOKO

India inahitaji kuunda nafasi za kazi za kutosha kwa idadi ya watu wa umri wa kufanya kazi ili kupata faida ya idadi ya watu. Asilimia 40 pekee ya watu wenye umri wa kufanya kazi nchini India wanafanya kazi au wanataka kufanya kazi, kulingana na Kituo cha Kufuatilia Uchumi wa India (CMIE).

Wanawake wengi zaidi wangehitaji kazi, kwani wanatumia muda mfupi katika umri wao kufanya kazi, kutokana na kuzaa, pia kutunza watoto. Taswira hapo ni mbaya zaidi. Takwimu linganishi inasema, asilimia 10 tu ya wanawake wenye umri wa kufanya kazi walikuwa wanashiriki kazini mwezi Oktoba kwa mujibu wa CMIE, ikilinganishwa na asilimia 69 nchini China.

Pia kuna wastani wa Wahindi milioni 200 wamehamia mbali na majumbani kwao, wengi wao ni wafanyakazi ambao huondoka vijijini kwenda mijini kutafuta maisha. "Miji yetu itakua kadiri wahamiaji wanavyoongezeka, kwa sababu ya ukosefu wa ajira na mishahara duni katika vijiji."

Wataalamu wa idadi ya watu, wanasema India pia inahitaji kuzuia ndoa za utotoni na inatakiwa kusajili ipasavyo uzazi na vifo. Uwiano wa jinsia potofu wakati wa kuzaliwa, ikimaanisha wavulana wengi huzaliwa kuliko wasichana, bado ni wasiwasi mwingine wa kijinsia.

Matamshi ya kisiasa kuhusu udhibiti wa idadi ya watu, nayo yanaonekana kulengwa kwa baadhi ya jamii walio wachache nchini humo, utafiti kutoka Kituo cha Utafiti cha Pew, ukisema "mapengo katika kuzaa watoto kati ya makundi ya kidini ya India kwa ujumla ni madogo sana kuliko yalivyokuwa."

### WAKATI WA UHURU

Wataalamu wa idadi ya watu, wanasema suala la umri wa watu nchini India bado unapata umakini mdogo. Mnamo 1947 India ilipopata uhuru, umri wa wastani wa India ulikuwa miaka 21. Asilimia tano ya watu walikuwa zaidi ya umri wa miaka 60. Leo, umri wa wastani ni zaidi ya 28, na zaidi ya asilimia 10 ya Wahindi wana zaidi ya miaka 60. Majimbo ya Kusini kama vile Kerala na Tamil Nadu yalipata viwango vya mbadala takribani miaka 20 iliyopita.

"Kadri idadi ya watu wa umri wa kufanya kazi inavyopungua, kusaidia watu wazee kutakuwa mzigo unaoongezeka kwa rasilimali za serikali," anatamka mwanahabari Rukmini na kuhitimisha hoja kwa swali "je, takwimu zinaweza kusema nini na haziwezi kutuambia kuhusu India ya sasa. Miundo ya familia itabidi ibadilishwe na watu wazee wanaoishi peke yao watakuwa chanzo cha wasiwasi."

***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***



Jumuiya za Wachina mitaani.

MAZINGIRA

# Wajue wadau wapya na nyenzo mpya zinazokabili uvuvi batili Ziwa Victoria

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

FUO ni taasisi ya kiraia inayojishughulisha na masuala ya kuwajengea uwezo wavuvi kufanya uvuvi endelevu ziwani, kutoa elimu ya mazingira au kwa jina lake halisi 'Fishers Union Organization' (FUO).

Hivi sasa imepewa jukumu na Wizara ya Uvuvi na Mifugo, kutoa elimu kwa wavuvi wa dagaa ziwani kutumia taa aina ya sola ya jua kuvua, ikiwa imeidhinishwa na serikali, kufanikisha uvuvi endelevu.

Pia ina majukumu ya kutoa elimu ya kuacha kutumia taa za betri za kuchaji pamoja na taa za karabai katika uvuvi, ambazo zimegundulika katika tafiti kuwa na madhara majini, hata kwa binadamu wanaotumia maji ya ziwani.

Mwenyekiti Mtendaji wa taasisi hiyo, ambaye ni mkongwe wa shughuli za uvuvi Ziwa Victoria, Juvenary Matagili, anabainisha kuwa elimu hiyo tayari imeshaanza kutolewa katika mialo mbalimbali ya wavuvi Ziwa Victoria, visiwani na kwa wadau.

Bwiru, ni miongoni mwa mialo iliyofanyiwa tafiti hizo na kuwa mfano katika maeneo mengine kwa wavuvi wa dagaa ziwani.

Matagili anasema taa za sola ni bora katika matumizi ya uvuvi ziwani, ambazo zimefanyiwa tafiti na wataalamu zikiidhinishwa kwa ajili ya uvuvi endelevu, kuliko taa zinazotumia betri za chaji aina ya zile za pikipiki.

Matagili anasema, betri hizo zinazosababisha madhara wakati wanapopata ajali wavuvi na kuzama maji nazo huzama chini ziwani na kugeuka kuwa taka ziwani. Vilevile kuna suala la uchafuzi wa mazingira, kuacha kemikali majini na sumu kwa binadamu wanaotumia maji na samaki wote inaelezwa wanaathirika.

Anaeleza kuwa taa za betri ni hatari zinazofungwa juu ya chelezo zilizotengenezwa kienyeji na wavuvi wenyewe wakitumia miti ya mielezi ambayo hukatwa ndani ya ziwa na kusababisha uharibifu wa mazalia ya samaki ikiwamo mazingira.

"Sola hizi zinafaa zaidi uvuvi wa dagaa mwanga wake siyo mkali, hauathiri hata samaki wengine kama vile Sangara wadogo, zinatengenezwa nchi za nje Uholanzi, China na India, anasema Matagili.

Aina za sola hizo baadhi zinatajwa ni nyepesi hata ikitokea ajali ya wavuvi, hazizami bali huelea majini.



Wachuuzi wa dagaa wakifanya shughuli zao za kununua na kuuza dagaa katika Mwalo wa Mswahili jijini Mwanza. **PICHA ZOTE : ANTHONYGERVAS**

Tayari wadau wa uvuvi na wavuvi wenyewe wanaendelea kupata elimu hiyo kupitia mikutano yao, huku Wizara ya Uvuvi na Mifugo ikipiga marufuku kuendelea kutumia taa hizo za betri kuvulia dagaa na samaki wengine.

**MADHARA YALIYOKO**

Maragili anabainisha madhara ya kutumia taa za betri, husababisha kemikali au sumu hatari ziwani, huathiri maisha ya viumbe maji na watu wanaotumia maji na samaki.

Pia inatajwa kuchangia kusababisha kansa na magonjwa kama ya figo na moyo kwa binadamu, inapogeuka taka na kuzama majini ikichafua mazingira.

Taa za betri anazitaja zinasababisha kuharibu mazalia ya samaki, kwani wavuvi hukata miti kwa ajili ya kutengeneza chelezo za kufungia taa na betri kwa ajili ya uvuvi. Miti inayokatwa ndio mazalia ya samaki, inayotunza mazingira hivyo husababisha uharibifu mkubwa ziwani.

Matagili anafafanua faida za kutumia sola jua, kuwa rafiki kwa mtumiaji mvuvi, imara zinahimili maji, zinawaka saa 12, kuanzia saa moja usiku hadi asubuhi nyepesi hazizami ziwani.

Vilevile anasema haziharibu mazingira na zimetengenezwa kwa uvuvi endelevu, baada ya kufanyiwa utafiti zikionekana bora zaidi katika shughuli za kuvulia.

**KILIO CHA WAVUVI**

Mwenyekiti huyo anasema, kilio kikubwa cha wavuvi hao kwa sasa ni bei kubwa ya kununua taa hizo za sola zilizoidhinishwa na serikali katika uvuvi endelevu, ambayo inafikia zaidi ya shilingi 500,000.

Matagili anasema muswada wa sheria ya uvuvi upelekwe na wizara bungeni kujadiliwa, kuhusu taa hizo kuwa na bei kubwa ambayo hawawezi kuimudu wavuvi kwa ajili ya kuendesha shughuli zao ziwani.

Anasema kutokana na gharama hizo, mtumbwi mmoja unatakiwa kutumia taa saba hadi nane, hivyo mtu akiwa na mitumbwi hata 40 hawezi kumudu kuinunulia yote, matokeo yake atashindwa kuendelea na uvuvi.

Kwa mujibu wa Matagili, wamiliki wengi wa mitumbwi na wavuvi mitaji yao ni midogo hivyo mwisho wa siku anayumba mtaji na kufilisika, hivyo ni muhimu kusikiliza kilio chao ili kusaidia kudhibiti kuendelea uvuvi haramu wa dagaa na samaki wengine ziwani, jambo hilo kwao bado ni kikwazo kikubwa cha shughuli zao.

Anafafanua kuwa, hadi sasa asilimia 95 ya wavuvi hasa wa dagaa wanaendelea kutumia taa zilizopigwa marufuku na serikali zinazotumia betri na karabai zinazotumia mafuta.

Mmiliki wa mtumbwi wa kuvulia dagaa Ziwa Victoria, Baraka Joseph, anasema uendeshaji wa shughuli za uvuvi ni mgumu na ameshindwa kumudu gharama kununua taa za sola ambaye anamiliki mtumbwi mmoja wa kuvulia dagaa.

"Serikali iangalie hatuna uwezo wengine wa kununua sola hizo, zilizoidhinishwa na serikali, bei ni kubwa hatuna mikopo wavuvi yakutuwezesha kufanya uvuvi wenye tija na endelevu," anasema Joseph.

Analalamika kuwa mtaji wake bado ni mdogo, ukilinganishwa na gharama za kununua taa za sola, ikiwa mtumbwi mmoja unatakiwa kuwa na taa zisizopungua nane.

Anadai kutengeneza mtumbwi mmoja unagharimu hadi shilingi milioni 3 kukamilika, ikiwamo kununua nyavu na vifaa vingine vya uvuvi.

Anasema wavuvi ziwani hawana bima za uvuvi hata wanapopata ajali wakati wa shughuli za uvuvi, lakini wanaingiza pato kubwa la taifa.

Anasema agizo la Wizara ya Uvuvi na Mifugo, bado linawatesa kichwani, lakini hawana namna ya kuacha kuendelea na uvuvi sababu ndiyo ajira yao.

Kiza Jaledy ni mvuvi wa dagaa aliyefanya kazi hiyo tangu mwaka 1996 alipomaliza darasa la saba kwao Kigoma, anasema changamoto ni nyingi zinazowakabili ikiwamo kukamatwa na maofisa uvuvi wakidaiwa kutumia nyavu zenye matundu madogo.

Anasema dagaa huvuliwa kwa nyavu zenye matundu yenye ukubwa wa milimita nane kisheria, chini ya hapo unakuwa ni uvuvi haramu hivyo serikali huchukua mkondo wake. Anafafanua, chanzo kingine ni kuwapo maduka yanayouza nyavu za matundu madogo au wenye viwanda vinavyotengeneza, lakini misako yote hufanywa kwao na serikali.

Anadai sheria ya uvuvi bado inayumba haijakaa sawa kuhakikisha wavuvi wanathaminiwa kama wazalishaji muhimu wa sekta ya uvuvi.




Taa za sola zilizoidhinishwa na serikali kwa uvuvi endelevu, zinazotajwa kutokuwa na madhara majini.

# Kanuni tano za kukupa afya bora usonge vyema mwaka ujao 2023



Mtu akifanya mazoezi.

MWISHO wa mwaka huwaleta pamoja ndugu, jamaa na marafiki, katika mikusanyiko kama hiyo vyakula na vinywaji vya kila aina huandaliwa, ili kunogesha sikukuu.

Nyakati kama hizo, baadhi ya watu wanakabiliwa na kibarua kigumu kufuata utaratibu wao wa kawaida, hasa katika masuala ya lishe. Kutokana na hilo mtindo wa maisha hubadilika na hapo ndipo uzito wa mwili pia huweza kubadilika.

Ni nyakati hizi pia ambapo utasikia jamaa na marafiki wakiwa wana mazoea ya kusema "nitaanza kesho", msemo ambao unaweza kuendeleza tabia zisizofaa.

Lakini je unawezaje kufurahia msimu huo bila kuathiri mpango wako wa afya?

Kwanza, kabisa ukiwa na nia ya dhati ya kudhibiti uzani wako lazima ujiwekee mipaka katika ulaji wako ili kuimarisha malengo yako, anasema mtaalamu wa lishe bora Irine Nduta: "Ni vyema kuachana na mienendo ambayo haiendani na malengo yako."

Ili usiongeze uzani kupita kiasi msimu wa sikukuu za Krismasi na mwaka mpya zingatia vidokezi hivi vitano.

Moja, Chagua vyakula usile kila kitu : Ni muhimu pia kufahamu kuwa unaweza kuteleza mara moja au mbili katika safari hii ya kudhibiti uzani anasema mtaalamu wa lishe bora. Mara nyingi watu huachana na malengo yao baada ya hili kutokea. Lakini, ni bora kuendelea kuzingatia lishe bora kuliko kurudi nyuma.

Pili, kula kwa kipimo: Punguza vyenye wanga katika sahani yako, ikiwezekana kwa karibu theluthi tatu, kile kinachoitwa sheria ya udhibiti wa chakula ili kuboresha afya.

Unaweza kifikia lengo hili kwa kujizoesha kula chakula kidogo kwa saa chache za siku au kufunga na kula katika masaa manane kwa siku au kufunga kula chakula siku mbili kwa wiki. Hii ni mambo yanayoaminiwa kupunguza hatari ya kupata magonjwa yanayohusiana na umri.

Tatu, jifuatilie mwenyewe: Ingawa kuzingatia malengo ya kudhibiti uzani kunaweza kuwa kibarua kigumu, wataalamu wa masuala ya afya wanasema, ni vyema kuhakikisha kuwa unapunguza ulaji wa vyakula vilivyokaangwa kwa kutumia mafuta mengi wakati wa likizo.

Nne, fanya mazoezi: Maisha ya kutofanya mazoezi ya mwili husababisha asimilia 10 ya vifo vya mapema duniani vinavyotokana na magonjwa kama vile ugonjwa wa moyo, kisukari aina ya mbili na aina mbali mbali za saratani.

Hakikisha unatembea au kuogelea hali ya hewa ikikuruhusu na epuka kutumia kipindi cha sherehe kukaa mahali pamoja.

Tano, usinywe pombe: Epuka vinywaji baridi na pombe kupita kiasi kila siku. Unapokunywa pombe hakikisha unakunywa maji pia kati ya kila kinywaji cha pombe.

Ukizingatia malengo yako kwa bidii, unaweza kuona kwamba umefanikiwa kudhibiti uzani wako hata wakati wa msimu huu wa sherehe.

***Kwa mujibu wa BBC.***



Chakula cha binadamu. **PICHA ZOTE: MTANDAO,**


---

## CHEMSHABONGO NA -00 34 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Sayari iliyo kubwa kuliko zote
5. kataa kumjibu mtu
8. kipingamizi
9. afisi
12.nchi ya pili kwa uwingi wa watu duniani
14.shuhudia kwa macho
15.chunguza kwa makini
16.kansa


Chini:
1. nyumba iliyojengwa
2. sehemu iliyo kandokando ya bahari
3. kuwa wa awali kufanya jambo
4. ukosefu wa chakula
6. awali
7. husemwa mwisho wa sala na Wakristo
10.tenda
11.dhamira
13.mahali bidhaa zinapouzwa



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

ADABISHA
MWAKA
WAKATI
ISRAELI
MWASHO
WADAI
AKARI
KABA
MTAKATIFU
SARA, KATA,
KIATU, ALOI
DAU, ATI, SIE, HII
MAKUTI

maoni SMS: 0787 00 97 94





Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | A | K | A | Y | A | | Z |
| A | D | A | M | U | | | A |
| K | A | M | B | A | | | M |
| O | | B | A | N | D | I | A |
| L | A | I | T | I | | | N |
| I | N | N | A | | M | T | I |
| | A | I | N | I | K | A | |
| | S | | A | | I | B | A |
| Y | A | L | | D | A | U | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | K | A | T | A | B | A | |
| W | | J | | M | | D | |
| A | M | E | R | I | K | A | |
| N | | N | | | A | | U |
| G | I | D | A | M | U | | F |
| A | | A | L | I | K | W | A |
| Z | | | A | T | I | A | |
| A | | | M | A | A | N | A |
| | N | I | A | A | | A | |



## Waanzisha operesheni kamata wazazi wanaowafungia watoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

OFISA Elimu Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, amesema wameanza operesheni ya kuwakamata wazazi au walezi wanaowafungia ndani watoto wenye ulemavu.

Akizungumza na Nipashe jana, Hinju alisema utafiti mdogo walioufanya unaonesha kuwa watoto wengine wanaofungiwa ndani wamefikia umri wa kwenda shule.

Hinju alisema katika kuhakikisha tatizo hilo linashughulikiwa Mkoa wa Mbeya umeandaa utaratibu kupitia kwa viongozi wa mitaa, vijiji kufanya msako wa nyumba kwa nyumba kuwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto shule. Alisema hatua hiyo itasaidia watoto wenye ulemavu kwenda shule na kujifunza stadi mbalimbali za maisha na kuweza kutimiza ndoto zao kupitia elimu.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha mkoa huo unatoa nafasi kwa watoto wenye ulemavu kupata nafasi ya kusoma na kujifunza kupitia Programu ya Elimu Jumuishi, shule za sekondari nne zimeteuliwa kuwa kwenye mradi huo.

Alisema shule za msingi 334 kati ya 811 za mkoa huo zimeingizwa kwenye programu hiyo kama vile Mwenge, Kyela, Katumba ambazo zinawahusisha watoto wa kawaida na wenye ulemavu kusoma pamoja.

Baadhi ya wabunge wa Mkoa wa Mbeya wamesema miongoni mwa ajenda walizonazo kwa sasa ni kutoa elimu kwa wazazi juu ya athari za kuwafungia watoto majumbani.

Alisema elimu hiyo ina lengo la wazazi au walezi kutambua madhara ya kufanya vitendo hivyo kuwa ni sehemu ya unyanyasaji wa kijinsia hivyo haikubali kwa mujibu wa sheria za haki za mtoto.

Mkurugenzi wa Shirika la Child Support Tanzania linalojihusisha na kuwahadumia watoto wenye ulemavu kupitia programu ya peleka marafiki zangu shule, Noela Msuya alisema mradi huo unalenga kuboresha mazingira rafiki na salama kwa watoto wa kitanzania kupitia mfumo wa elimu jumuishi.

Mradi wa peleka rafiki zangu wote shule wenye thamani ya Sh. milioni 200 unalenga kuwafikia watoto wengi zaidi kwenye mikoa ya Mbeya, Rukwa, Mwanza, Kigoma na Mtwara katika kipindi cha miezi mitano ijayo.

# Wadau wa pareto waiomba serikali kuwakamata vishoka

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA na wadau wa pareto wameiomba serikali mkoani Mbeya, kusaidia kuchunguza na kuwakamata watu wanaofadhili ununuzi wa zao hilo nje ya utaratibu ujulikanao kama vishoka.

Wamesema watu hao wamekuwa wakiwaibia wakulima na kudhoofisha jitihada za kuendeleza zao hilo.

Ombi hilo limetolewa juzi na wadau wa pareto wakati wa kikao cha kujadili namna watakavyoweza kuboresha mnyororo wa thamani kwenye zao hilo ambalo kwa sasa limevamiwa na vishoka na kusababisha wakulima kupata fedha kidogo.

Mwakilishi wa Kampuni ya Pareto Tanzania (PCT), Jamal Issa, alisema wakulima wanakabiliwa na tatizo kubwa la vishoka kutoka kwa wanunuzi ambao hununua zao hilo kwa bei ndogo.

Alisema hali hiyo inawaumiza wakulima kwani hawapati faida licha ya kutumia nguvu kubwa ya kuzalisha lakini faida ni ndogo.

Alisema mara kadhaa wamekuwa wakizungumza na viongozi wa kata na halmashauri kuhusu vishoka ambao huwalangua wakulima lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kuwadhibiti.

"Ni muda sasa wakulima hao kuangaliwa kwa jicho la huruma ili waweze kupata faida kutokana na kilimo chao cha pareto inaongoza kwa uzalishaji na ubora nchini," alisema Issa.

Akizungumzia suala la vishoka hao kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, Ofisa Tarafa wa Isangati, Aron Sote, alisema tayari hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima kuacha kuwauzia vishoka mazao yao.

Alisema kazi kubwa wanayoifanya ni kuwahamasisha wakulima hao kujiunga kwenye vyama vya ushirika ili kuuza mazao yao kwa pamoja na kupanga bei itayowanufaisha.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Kata ya Santilia, Mwajuse Mwarwanda, alisema tatizo kubwa linalowakabili wakulima wa eneo hilo ni kukosekana kwa soko la uhakika kuuza mazao yao.



Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, juzi alifanya ziara ya kukagua ujenzi wa barabara Kata ya Iyela yenye urefu wa kilomita moja inayojengwa kwa kiwango cha lami. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wapendekeza Kiswahili kitumike shule za msingi hadi chuo kikuu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa elimu nchini wameishauri serikali kutengeneza mitaala mipya ambayo itaandikwa na kutumia lugha ya Kiswahili kwa lengo la kusaidia kukuza lugha hiyo na kuwawezesha wanafunzi kuanzia darasa la awali hadi vyuo vikuu kujifunza kwa ufasaha.

Walisema umefika wakati wa Tanzania kuanza kuienzi lugha ya Kiswahili kwa kuitumia kujifunzia kuanzia darasa la awali mpaka elimu ya juu.

Mtaalamu wa lugha ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki (CUCoM) kilichoko jijini Mbeya, Prof. Joshua Madumulla, alisema kuna tatizo kubwa kwa wananchi juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili ikiwamo kwenye sekta ya elimu tangu enzi za utawala wa Hayati Mwalimu Nyerere.

Alisema licha ya Hayati Mwalimu Nyerere kuhamasisha matumizi ya lugha za Kiswahili lakini hakuna jitihada zozote zilizofanyika ili kuifanyia lugha hiyo kuwa rasmi kwenye mitaala ya elimu.

"Kuna mgawanyiko wa makundi hapo, moja linahamasisha lugha ya Kiingereza iendelee kutumika kwenye masomo na lingine ambalo ndilo lina watu wengi linaomba lugha ya Kiswahili itumike kujifunzia na kufundishia, tunahitaji kushikamana maana hata hao wachache ambao wana uwezo na wanasomesha watoto wao shule binafsi lugha ya Kiingereza hawaijui vyema," alisema Prof. Madumulla.

Aidha alitoa tahadhari kwa serikali kutoweka kando lugha ya Kiswahili katika mitaala ya elimu ili kukuza na kueneza lugha hiyo kinyume na hapo tunaweza kuwa watumwa wa lugha za kigeni.

Mwanafunzi wa kidato cha tano Shule ya Sekondari Samora jijini Mbeya, Magreth Millinga, alipendekeza lugha ya Kiswahili kutumika kujifunzia na kufundishia kuanzia ngazi ya chini ya elimu hadi juu.

Alisema serikali ifanye mazungumzo na wamiliki wa shule binafsi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye masomo yao kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kuelewa masomo wanayofundishwa.



# Kaya 156,590 kuondolewa TASAF

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeziondoa kaya 156,586 zilizofuzu katika mpango wa kuhudumia kaya maskini na kuongeza zingine ambazo zinahitaji kusaidiwa ili ziondokane na umaskini.

Aidha, kaya 730,138 bado zina hali duni kiuchumi, hivyo zitaendelea kuwapo katika kipindi cha pili cha mpango wa kupokea ruzuku unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema kaya hizo zinaondolewa kutokana na kukidhi vigezo vya kiuchumi ikiwamo kujihudumia.

Mwamanga alisema mpango huo ni endelevu kila kaya ambazo zitafuzu zitaondolewa na kuingizwa zingine ambazo zina hali mbaya kiuchumi.

Alifafanua kuwa kaya hizo zitaondolewa Januari, mwakani na nafasi zao zitachukuliwa na watu wengine ili kuendelea kupokea ruzuku ili nazo zijiinue kiuchumi.

"Kuanzia mwakani, watu hawa hawatakuwapo katika mpango huu kwa sababu wameshafuzu na kujikwamua kiuchumi," alisema Mwamanga.

Alisema katika kipindi cha awamu ya pili kilichozinduliwa Februari, 2020 kilikuwa na zaidi ya kaya milioni 1.3 zenye zaidi ya watu milion tano ambao ni sawa na asilimia 55.

Pia alisema katika kipindi hicho, jumla ya Sh. bilioni 580 zilitumika katika utekelezaji wa mpango huo kwa walengwa wa mpango huo hapa nchini.

"Pamoja na kaya hizo, zingine 16,490 pia zitatolewa kwenye mpango huo ifikapo Januari 2023 ambazo zimekidhi vigezo kwa ajili ya kujihudumia," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kaya hizo zimetoka katika halmashauri za wilaya za Bagamoyo, Kibaha, Lindi, Chalinze na katika Manispaa za Mtwara, Lindi na Unguja.

Alisema pia TASAF itaendelea kutoa elimu kwa walengwa kuhusu taratibu za mpango kuhamasisha ushiriki wa walengwa katika masuala mbalimbali kuwekeza ili wanapohitimu waweze kujihudumia wao wenyewe.

Hata hivyo, alisema katika mpango huo endelevu, kaya zingine 223,418 ambazo nazo zimeimarika kiuchumi zitaondolewa Septemba, mwakani ili kupisha wengine waingie katika mpango huo.

Naye mlengwa wa mpango huo, Janeth Mbelwa, aliishukuru serikali kutokana na kuleta mpango huo kwa sababu umewasaidia sana.

Alisema walengwa wengi hivi sasa wanaendesha biashara ndogo ndogo na ufugaji kutokana na fedha za TASAF ambazo wanapewa katika mpango huo.



Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Ushauri (RCC) Dodoma jana, (kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule na Spika mstaafu, Job Ndugai. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Serikali yaahidi kumalizia ujenzi zahanati

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

SERIKALI kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeahidi kutoa fedha ili kumalizia ujenzi wa boma la zahanati ya kijiji cha Mtumile wilayani Mpwapwa, baada ya nguvu kazi za wananchi kuishia hatua ya kuezeka.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alitoa ahadi hiyo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Mtumile, Jimbo la Kibakwe, wilayani Mpwapwa.

"Serikali itatoa Sh. milioni 50 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa boma la zahanati hiyo pamoja na kuanza ujenzi wa nyumba mbili za watumishi kwa kutumia fedha hizo. "Nguvu zenu mlizojitolea na nguvu zangu nilizojitolea haziwezi kwenda bure, serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imesikia kilio chetu," alisema.

Aidha, alifafanua kuwa katika Mkutano wa Mkuu wa 10 wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais alielekeza viongozi kuhakikisha wanachapa kazi na kutenda haki kwa wananchi wanaowaongoza.

"Niwaombe viongozi simamieni watu wafanye kazi, kazi ya serikali ni kuweka huduma za msingi za kijamii ambazo zipo kwa kiasi kikubwa," alisema.

Akitoa salamu za kumkaribisha Waziri, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Richard Maponda, alisema kuna kazi nzuri zimefanywa katika Jimbo la Kibakwe ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, elimu, afya na umeme.

"Tunapaswa kuungana na kiongozi wetu kwa kumwamini katika kazi zilizotangulia kufanyika. Maendeleo ni kupanga na kuchagua. Huwezi kuyafanya yote kwa wakati mmoja, hivyo kuna mambo yatatangulia na mengine yatafuata," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mtumile, Tito Mduwile, aliishukuru serikali kwa fedha ilizopatia serikali ya kijiji ambazo zimesaidia kuimarisha miundombinu ya elimu na afya.

"Kiasi cha Sh. milioni 25 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa Shule ya Msingi Mtumile na kiasi kingine cha fedha za madawati zilizotolewa na wadau wa elimu ikiwa ni pamoja na fedha kutoka mfuko wa jimbo ambazo zimetumika kupauwa zahanati ya Mtumile," alisema.

## Serikali yashauriwa kuwaamini wazawa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIONGOZI wa mashirika na taasisi wametakiwa kujenga uzalendo kwa wataaalamu wa ndani katika uendeshaji wa miradi ya maendeleo nchini.

Hayo yalisemwa jana na Dk. Kafuku Mkurugenzi wa Kituo cha Uendelezaji na Uhawilishaji wa Teknolojia wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Gerald Kafuku wakati wa mkutano wa wadau wa sayansi unaoendelea jijini Dodoma.

Alisema kuna wataalamu wengi sana hapa nchini kinachotakiwa tu ni waaminiwe ili waweze kupatiwa miradi ya kufanya.

"Viongozi tunatakiwa tujenge utaratibu wa kuwaamini wataalamu wa ndani lengo ni kuhakikisha miradi inafanyika kikamilifu, kumekuwa na tabia ya kutowaamini wataalamu jambo ambalo si sahihi kwa sababu tunatakiwa kupenda vya kwetu ndio vifuate vya wengine," alisema.

Akizungumzia kuhusu mkutano huo, alisema lengo ni kuangalia namna ya kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inatekelezwa nchini ili kuhakikisha inasonga mbele.

Dk. Cecilia China kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, alisema mkutano huu utasaidia wataalamu kufanya utafiti wao kulingana na viwanda vinahitaji nini tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema awali walikuwa wakifanya utafiti kupitia maabara lakini ukipelekwa sokoni unakuta hauhitajiki kwa sababu umefanya utafiti ambao wenye viwanda hawaihitaji.

Kutokana na hilo alisema mashirikiano haya walioanza kufanya yatasaidia kwa kiasi kikubwa watafiti kufanya utafiti ambao ni sahihi na unaohitajika katika viwanda mbalimbali hapa nchini.

Mbali na hilo alisema hii itasaidia kuboresha mifumo, mitaala ili kufanya wanafunzi kufanya tafiti zao kwa ufasaha na uzoefu ambao utaleta matokeo chanya kwa jamii.

Alisema sera ambazo zitakuwa zinasapoti mambo mbalimbali ya utafiti zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupiga hatua kwenye masuala ya utafiti unaofanywa nchini.

Dk. Cecilia alisema wanaishukuru COSTECH kutokana na kuandaa mkutano huo ambao utawasaidia kwa kiasi kikubwa kuleta mahusiano mazuri katika ufanyaji tafiti mbalimbali.





## Wananchi wakumbushwa umuhimu wa ulipaji kodi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, amesema kuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kuwa anaziunga mkono jitihada za serikali ukusanyaji wa mapato akisisitiza kuwa hakuna nchi yoyote duniani iliyoendelea bila ya kuimarika kwa mifumo ya kodi.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akikabidhi msaada wa chakula uliotolewa na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa wananchi wa Kijiji cha Kangagani, Mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa katika shamrashamra za kusherehekea mwezi wa Shukrani na Furaha kwa walipakodi.

Aliwataka wananchi hao kuwa na utamaduni endelevu wa kudai risiti za kielektroniki kwa kila ununuzi wanaofanya ili serikali ipate mapato na kuwanufaisha wananchi kwa ujumla.

Alisema serikali haina nia mbaya kwa wananchi wake na imejipanga vizuri kuhakikisha mianya yote ya upotevu wa mapato inazibwa na kila mmoja anatimiza wajibu wake, pamoja na kutoa ahadi kuwa Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba ipo tayari muda wowote kuungana na ZRB kuhamasisha wananchi kulipa kodi.

Mkurugenzi wa Ofisi ya ZRB Pemba, Jamal Hassan Jamal, alisema kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi na wafanyabiashara kulikosababisha kuongezeka ulipaji kodi wa hiari na kupanda kwa makusanyo ya kila mwezi, ZRB imeamua kuufanya mwezi wa Desemba kuwa ni wa kuwashukuru na kufurahi na walipakodi.

Wananchi wa kijiji hicho waliishukuru ZRB kwa uamuzi mzuri walioufanya wa kuwafikiria wananchi wa kijiji hicho ili kusaidia serikali ukusanyaji wa mapato.

Jumla ya kaya 100 za Kijiji cha Kangagani zimefikiwa na msaada huo wa chakula kutoka ZRB.

# Serikali yaitaka Uhamiaji kudhibiti wahamiaji haramu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, ameutaka uongozi wa Idara ya Uhamiaji, kuimarisha mifumo vizuri na kupanga mikakati iliyo bora ili kuwa na utaratibu mzuri katika bahari kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu.

Waziri Pembe aliyasema hayo katika uzinduzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo masheha wa Zanzibar kuhusu masuala ya Uhamiaji uliofanyika Shule ya Mkwajuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja, yaliondaliwa na Idara ya Uhamiaji.

Alisema katika maeneo ya bahari ikiwamo bandari bubu kunahitaji udhibiti ili kuziba mianya ya usafirishaji haramu wa binadamu na kwamba ushirikiano wa pamoja unahitaji kati ya masheha wavuvi na Idara ya Uhamiaji.

Alisema katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kuna maeneo mengi ya wazi ambayo ni lazima wawe na mkakati maalumu wa kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo.

Masheha wanajukumu kubwa kisheria kuwatambua wageni wanaoingia katika shehia zao wakiwamo wenyeji ambao uhama kutoka shehia moja kwenda nyingine na wanaotoka nje ya nchi ambao uhamia kwenye shehia zao.

"Lazima muhali tuweke pembeni na kwa kushirikiana na wenzetu wa Uhamiaji hasa katika kuona wanawatambua vizuri na pia kutoa taarifa vizuri kwenye mamlaka husika," alisema.

Alisema suala hilo likifuatwa litaleta weledi mkubwa wa kutambua wageni na nyaraka zao ambazo zitawawezesha kuishi katika nchi zao.

Pamoja na kuwa na majukumu mengi, alisema suala la ulinzi na usalama wa raia wao ni muhimu.

Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Hassan Ali Hassan, alisema bado kuna tatizo la uhamiaji usiofuata sheria za nchi hasa kwa wahamiaji wanaotoka katika nchi jirani za Afrika Mashariki ikiwamo Kenya, Uganda, Congo, Burundi na Rwanda.

"Kama tunavyojua Zanzibar ni nchi ya visiwa na ina mianya mingi hutumiwa na baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu kwa maslahi yao," alisema.

Alisema wameamua kutoa mafunzo kwa masheha kwa sababu kazi za Uhamiaji haziwezi kukamilika bila ya ushirikiano.

Wakizungumza kwa niaba ya masheha wenzao, Sheha wa Matemwe Wadi, Ali Wadi na Machano Pandu Machano wa Kiwengwa, walisema masuala ya uhamiaji haramu yamo katika maeneo yao hasa yaliyozungukwa na hoteli za kitalii.

Walisema ni vyema masheha wakapita katika hoteli za kitalii ili kujua uhalali wa kufanya kazi ndani ya hoteli hizo na kupewa marejesho kwa hatua ambazo wanazichukua.

"Shehia ambazo zipo katika Kanda za Pwani zinakabiliwa na tatizo la uhamiaji haramu hasa kwa maeneo yenye bandari bubu ambapo kwa jinsi zinavyoendeshwa zinaonekana kuwa halali," alisema Sheha wa Banda Kuu, Haji Khamis Haji.



Mwandishi wa gazeti la Nipashe, Rahma Suleiman akimkabidhi zawadi Zulfa Hassan Hussein baada ya kumaliza shahada yake ya Sayansi ya Jamii katika Utawala wa Umma, Chuo Kikuu cha Zanzibar ZU jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wa3 akiwamo mganga wa kienyeji watuhumiwa udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar, linawashikilia watu watatu akiwamo mganga wa kienyeji kwa tuhuma za makosa ya udhalilishaji wa kijinsia.

Watu hao wanadaiwa kumteka mtoto wa miaka 12 na kumlawiti.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika ofisi za makao makuu ya polisi visiwani humo, Kamishna Msaidizi wa jeshi hilo, Zubeir Chembera, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Khamis Dilshadi Muradi (33), Juma Dilshadi Muradi (23) na Dickson Ndushi (40) ambaye ni mganga wa kienyeji.

Alisema mganga huyo ameingia hatiani baada ya kumpa masharti mteja wake Khamis Dilshad kuwa ili kumtatulia tatizo lake lazima amlawiti mtoto.

Alisema Novemba 12, mwaka huu majira ya saa 1:00 asubuhi, maeneo ya Chukwani Wilaya ya Magharibi 'B' mlalamikaji, aliripoti kituo cha polisi Mazizini kuwa mtoto wake alitekwa nyara na watu wasiofahamika na kumpeleka mahali kusiko julikana.

Aidha, alisema siku hiyo mtoto huyo akiwa na ndugu yake waliondoka nyumbani kwao kuelekea madrasa na ilipofika saa 7:00 mchana muda wa kurudi nyumbani, alirudi mdogo wake pekee na alipoulizwa hakuwa na majibu ndipo mzazi wa mtoto huyo alipopatwa na wasiwasi na kuanza kufuatilia na kisha kutoa taarifa kituo cha polisi.

Baada ya taarifa hiyo, jeshi hilo lilianza kufanya uchunguzi wa kina na wakati upelelezi ukiendelea kufanyika, baba wa mtoto huyo kwa nyakati tofauti aliendelea kupokea ujumbe wa simu zenye vitisho vya kutakiwa atoe fedha ili arudishiwe mtoto wake.


Alisema licha ya kumtumia ujumbe wa vitisho, pia alimtumia picha za mtoto wake na kumwambia yupo hai ila anachotakiwa kutoa pesa, kadri siku zilivyozidi kusonga mbele na kiwango cha pesa kiliongezeka.

"Alianza kumwambia akiwa anamtaka mtoto wake atoe shilingi milioni tatu, akaenda shilingi milioni tano hadi kufikia shilingi milioni nane kwa kumuona baba wa mtoto huyo kidogo ana hela, lakini hata hivyo tulifanikiwa kumnasa bila ya kuambulia chochote," alisema Kamishna.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya taarifa, lilifanikiwa kunasa mawasiliano ya namba za simu kwa njia ya mtandao kwa wale wote ambao wanahusika na kutoa vitisho hivyo.

Alisema baada ya mtoto huyo kupatikana kwa kushirikiana na wazazi wa mtoto na watu wa Ustawi wa Jamii, mtoto huyo alipelekwa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kwa lengo la kujua afya yake huku uchunguzi wa awali ulibaini kuwa mtoto huyo amelawitiwa. Kamishna huyo alisema, Desemba mwaka huu majira ya alasiri maeneo ya Bambi, Jeshi la Polisi liliendelea kufanya uchunguzi na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa Juma Dilshadi Muradi katika mahojiano ya awali alikiri kumteka mtoto na kisha kumpleka kwa mganga Dickson Ndushi kumficha na kukiri kumlawiti mtoto huyo kwa nyakati tofauti.

Alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea na utakapokamilika watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma hizo.



# Machinga waendelea ‘kupeta’ barabarani

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAFANYABIASHARA wadogo (machinga), wameonekana kurudi kwa kasi maeneo yasiyoruhusiwa kuendelea na biashara zao kama kawaida.

Machinga hao wameondoka katika masoko rasmi yaliyokuwa yametengwa na Manispaa ya Ilemela na Jiji la Mwanza na kurudi kupanga bidhaa zao barabarani.

Baadhi ya machinga hao wametoka katika masoko ya Igoma, Pasiansi Mchafukuoga, Buhongwa na sasa wamerudi maeneo ya katikati ya jijini likiwamo eneo la Makoroboi na sehemu zingine ambazo waliondolewa.

Kutokana na hatua hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amewataka viongozi wa wafanyabiashara hao kuhakikisha wanawaondoa wafanyabiashara hao waliorudi kufanya biashara katika maeneo yaliyozuiliwa kabla hawajachukuliwa hatua za kisheria.

Malima alitoa agizo hilo juzi katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mwanza (RCC). “Ole wenu nyie viongozi mkawe chanzo cha kuchochea vurugu zitakazosababisha watu waingie barabarani kwa kufanya maandamano nyinyi mtakuwa wa kwanza kuhusika,” alisema.

Alisema amepata taarifa kwamba wafanyabiashara hao watafanya biashara popote hadi ofisini kwa Mkuu wa Mkoa watapanga.

Alionya waache mchezo wa kujaribu kuvunja amani kwa kuwa hatawavumilia.

“Nyie viongozi wa wamachinga tunapanga vizuri, lakini mkifika huko hamtekelezi hali inazidi kuwa mbaya wamachinga wanarudi kwenye maeneo tuliyokataza, sasa ninawaambia lolote litakalotokea huko nyinyi ndiyo nitawawajibisha, nendeni mkazungumze nao waondoke bila kushurutishwa maana nyinyi ndiyo wanawasikiliza,” alisema Malima.

Naye Mwenyekiti wa Shiriko la Machinga mkoani Mwanza, Mohamed Dauda, aliomba serikali ya mkoa kutenga maeneo ya mjini kati kwa kuteua barabara moja ifungwe ili wafanye shughuli zao kwa urahisi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondoa mgogoro unaoendelea katika maeneo mengi ya Jiji la Mwanza kuhusu machinga kupanga bidhaa barabarani.

Baadhi ya machinga waliomba serikali kama haitokuwa na maeneo watakayowatengea katikati ya jiji, wawaruhusu kila saa 10 jioni wapange biashara katika maeneo wanayoona ni rafiki kwa ajili ya kufanyia biashara.

“Suala la machinga serikali inapaswa kulitazama kwa umakini sana, kwa sababu ni jamii iliyotumia fursa ya kujiajiri na kujipatia kipato halali, hivyo serikali iwatambue na kuwarasimisha kama wafanyabiashara wadogo, tunaomba serikali kulitambua kundi hili muhimu,” alisema Zainabu Shakuru.



Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, akipanda mti baada ya uzinduzi wa soko jipya la wajasiriamali Manispaa ya Shinyanga juzi, soko hilo liligharimu Sh. milioni 114. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Maofisa kilimo watakiwa kuwa wabunifu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATAALAMU wa kilimo katika Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera wametakiwa kuweka mipango thabiti itakayowezesha uchumi wa wananchi hususani vijana wa kukuza sekta hiyo.

Akizungumza katika kikao cha ushauri cha kujadili maendeleo ya wilaya hiyo (DCC), jana mjini hapo, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Hamed Njovu, aliwaagiza maofisa kilimo kukaa na kupanga ni kilimo cha mazao gani kitaleta matokeo ya haraka ya kiuchumi kwa wananchi.

Njovu alisema huwezi kuhamasisha kilimo cha miti au mazao ambayo yanaleta matokeo ya kiuchumi baada ya miaka 10 ama 15, halafu ukategemea wananchi hususani vijana waitikie.

“Vijana wanaangalia wafanye kitu gani cha kuwaletea matokeo ya haraka na ndiyo maana wanakimbilia kwenye kuendesha bajaji na bodaboda, lakini maofisa kilimo wetu wakichagua zao ambalo linaweza likampa mkulima matokeo ya haraka vijana wataenda huko,” alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Mosses Machali, alisema wataalamu wa kilimo wanapaswa kujadili ni mazao gani au aina zipi za matunda yakilimwa yatapata soko ndani na nje ya nchi ili lengo la kuinua uchumi wa wananchi litimie.

“Ni aibu kwa wilaya yetu kwa hali ya hewa nzuri iliyoko na jiografia yake ilivyo kutegemea hata maparachichi yaletwe hapa kutoka mikoa mingine kama Mwanza, Kigoma, hili sikubaliani nalo, tunapaswa kuweka mkazo angalau kila kaya iwe na miti ya matunda,” alisema. Katibu wa Chama cha Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) mkoani Kagera, Rwechungura Mali, alishauri watendaji kutokaa ofisini na kuacha kuwachekea wananchi, badala yake wawahimize kufanya kazi kwa bidii na kutumia muda wao kuwatembelea na kukagua shughuli zao za maendeleo ikiwamo kilimo.

“Mkurugenzi kama ofisa kilimo hakuletei taarifa ya migomba mingapi mipya imepandwa, mibuni mingapi au miparachichi mingapi imepandwa, unamlipaje mshahara, kipimo kiko wapi kwamba mtumishi huyo anafanya kazi, tunaleana na hili ndilo tatizo la Bukoba,” alisema.

Akizungumza katika kikao hicho, Mtendaji wa Kata ya Kitendaguro, Manispaa ya Bukoba, Novatus Mwesiga, alishauri kuandaa vipaumbele vya mazao gani yalimwe kwa kushirikisha taasisi za kifedha ili wananchi watakaoonyesha utayari wawezeshwe kufikia malengo yao.

## Taasisi yakumbuka watoto wenye usonji

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

TAASISI ya kusaidia watoto na vijana wenye usonji ya Living Together Autistic Foundation (Li-TAFO), imewakatia bima watoto na vijana 150 wenye usonji.

Taasisi hiyo imeomba serikali na wadau wengine kusaidia upatikanaji wa bima za afya, elimu na vifaa wezeshi ili kuwasaidia katika mambo yao watoto wenye usonji.

Akizungumza katika hafla ya chakula cha jioni ya kujumuika na watoto na vijana wenye usonji pamoja na uzinduzi wa kitabu cha safari ya ushindi ya mama na mtoto mwenye usonji jijini hapa hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa Li-TAFO, Shangwe Mgaya, alisema mpango wa taasisi hiyo kwa mwaka huu ilikuwa ni kukata bima za afya 300, lakini walishindwa kufikia lengo hilo kutokana na uhaba wa fedha.

Alisema lengo halikutimia kwa sababu ya uwezo mdogo huku akiwashukuru wadau mbalimbali walioguswa na kuchangia misaada mbalimbali.

Alisema, tatizo lililoko ni jamii kutokuwa na uelewa kuhusu kundi hilo na kuwachukulia watoto wenye usonji kama laana.

Aliitaka jamii itambue wana haki kama walivyo wengine ikiwamo kusoma, kufurahia maisha na wataendelea kuwa na makongamano kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu usonji.

Alisema tatizo lililoko ni watoto hao kutopata malezi bora huku akiwataka wazazi kuwapenda watoto hao, kuwatunza na kuacha kuwanyanyapaa.

“Tatizo la usonji ni kubwa sana nchini nikikumbuka nilipopata mtoto wangu mwenye tatizo hilo nilidhani nchi nzima ni mimi peke yangu, lakini baada ya kuanza kutangazwa na kutoa elimu watu wengi zaidi walijitokeza na kuongelea tatizo hilo, tunawaomba viongozi na serikali kulichukulia suala la usonji kwa umakini zaidi vinginevyo tutakuwa tunatengeneza bomu, kumlea mtoto mwenye usonji ni gharama,” alisema Shangwe.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Massala, akizungumza katika hafla hiyo, alisema tatizo la usonji siyo la mtu mmoja na linaweza kumpata mtu yeyote.

Alisema hakuna mtu mwenye uwezo wa kuomba kupata tatizo hilo bali hutokea pasipo matarajio na kuahidi kushirikiana na taasisi hiyo katika kuwalea watoto wenye usonji.

Aidha, aliwaomba wadau mbalimbali kuungana na taasisi hiyo ili kufanikisha upatikanaji wa bima ili kuleta furaha ndani ya kundi hilo na kuiomba iendelee kujifunza.

# Mchungaji atuhumiwa kwa wizi na udanganyifu

**WASHINGTON, Marekani**

MCHUNGAJI wa Marekani Lamor Whitehead ambaye alishambuliwa na mtu aliyekuwa na bunduki na kuibiwa kipuli cha zaidi ya dola milioni moja wakati alipokuwa akihubiri katika matangazo ya moja kwa moja ya mtandao mjini New York ameshitakiwa kwa wizi na udanganyifu.

Inaelezwa kuwa Whitehead, aliporwa saa na Almasi yenye thamani ya Sh. Bilioni 2.3 na zumaridi Julai mwaka huu, huku mahakama ikisema kwa sasa mchungaji huyo ameshitakiwa kwa uhalifu wa madini.

Ilielezwa kuwa mchungaji huyo anashutumiwa kwa kumlaghai na kumuibia mmoja wa waumini wa parokia yake pesa zake za akiba ya kustaafu, na kujaribu kumdanganya mfanyabiashara na kulilaghai shirika la upelelezi la Marekani (FBI).

Kwa mujibu wa taarifa ya wizara ya sheria, Whitehead, alikamatwa mwanzoni mwa wiki hii na atafika katika mahakama ya shirikisho.

Pia taarifa ilisema fedha zinazodaiwa kuchukuliwa kutoka kwa muumini wake ni takriban dola 90,000 ambazo ni zaidi ya Sh. milioni 210, na kwamba zilitumiwa kununua bidhaa za anasa na nguo.

Aidha, inaelezwa kwamba mchungaji huyo anaweza kufungwa kifungo cha hadi miaka 20 jela, iwapo atapatikana na hatia ya mashitaka yanayomkabili.

Inabainishwa kuwa baada ya tuhuma hizo mchungaji huyo alituma ujumbe kwenye mtandao wake wa Instagrum unaosomeka 'Not guilty' akimaanisha kuwa hana hatia, huku akiwaomba wafuasi wake kujiunga na matangazo yake ya moja kwa moja ya mtandao.

Baada ya kuibiwa mwezi Julai mwaka huu, mchungaji Whitehead, ambaye alipewa jina bandia 'bling bishop' na vyombo vya habari vya New York, aliapa kwamba mhusika hataepukana na wizi.

Kwa mujibu wa gazeti la New York Post, vitu vilivyochukuliwa kutoka kwake na mke wake ni pamoja na saa ya Rolex na za Cavalier , Rubi ya utume yenye thamani ya dola 25,000 na pete ya almasi yenye thamani ya dola 25,000 sawa na Sh. milioni 58.3 pamoja na hereni.

***BBC***



Mchungaji Lamor Whitehead akizungumza katika mazishi ya muimbaji wa muziki wa rap, Biz Markie mwaka 2021. **Picha: BBC.**

## Libya yawahukumu kifo wanachama 17 wa IS

**TRIPOLI, Libya**

MAHAKAMA ya Libya imewahukumu adhabu ya kifo watu 17 baada ya kukutwa na hatia ya kujiunga na kundi linalojiita Dola la Kiislamu (IS), na kufanya mashambulizi kwa kutumia jina hilo.

Mwendesha mashtaka alisema jana kuwa mahakama ya Tripoli pia imewahukumu watu wawili kifungo cha maisha gerezani na wengine 14 vifungo vidogo jela.

Taarifa ya mwendesha mashtaka ilieleza kuwa watu hao walikutwa na hatia ya kufanya shughuli zinazohusishwa na IS, pamoja na ghasia za kutumia silaha kwenye mji wa Sabratha.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, watu walioshtakiwa wamewaua jumla ya watu 53 na kuharibu majengo ya umma, aidha uraia wa watu waliohukumiwa kifo haujatangazwa.

Mwaka 2010, Libya ilipiga kura kupinga azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa linalotaka kusitishwa kwa adhabu ya kifo duniani kote, lakini haijachapisha takwimu za kuaminika kuhusu adhabu ngapi kama hizo ambazo zimetolewa.

***DW***

# Rais Ghana awanyooshea kidole Burkina Faso

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

RAIS wa Ghana Nana Akufo Addo amesema kwamba Burkina Faso imewapa mamluki wa Russia haki ya kuchimba madini nchini mwao, huku waziri wa madini wa Burkina Faso akijitokeza na kukanusha madai hayo

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, Rais Addo wiki iliyopita alizua mtafaruku baada ya kudai kwamba Burkina Faso ilia-jiri mamluki kutoka kundi la Wagner la Russia, ili kusaidia kwenye mapambano dhidi ya wanamgambo wa kiislamu.

Wakati akizungumza na wanahabari akiwa na waziri wa mambo ya nje wa Marekani, Rais Addo, alisema kwamba anaamini mgodi ulioko kusini mwa Burkina Faso umepewa mamluki hao kama njia ya malipo kwa huduma zao.

Serikali ya Burkina Faso haijakanusha wala kukubali madai hayo, ingawa imemuita balozi wa Ghana nchini humo kwa mkutano unaotarajiwa kufanyika kesho, ili afafanue zaidi kuhusu matamshi ya rais wake.

Aidha, ilibainishwa kwamba Mali ambayo ni jirani wa Burkina Faso, mwaka uliopita pia iliwakaribisha mamluki wa Wagner, ili kuwasaidia kwenye vita dhidi ya wanamgambo.

***VOA***

# 19 mbaroni kushiriki harusi wapenzi jinsia 1

**KANO, Nigeria**

JESHI la polisi la Kiislamu kaskazini mwa mji mkuu wa Nigeria limewakamata Waislamu 19, kwa tuhumu za kuhudhuria harusi ya wapenzi wa jinsia moja.

Msemaji wa kikosi hicho Lawal Ibrahim, alisema kikosi hicho kilivamia sherehe ya ndoa mwanzoni mwa wiki hii huko Kano baada ya kupewa taarifa kuhusu tukio hilo.

Alisema wanandoa hao ambao walikuwa bado hawajaweka viapo vyao, walifanikiwa kukimbia na polisi walikuwa wakiwatafuta.

Inaelezwa kuwa Kano ina idadi kubwa ya waislamu, ambapo mfumo wa kisheria wa Kiislamu unafanya kazi pamoja na sheria za kilimwengu.

Pia inatajwa kuwa vitendo vya mahusiano ya jinsia moja ni haramu chini ya mifumo yote miwili ya kisheria nchini Nigeria, na kwamba wale wanaoishi kaskazini ni Waislamu na watu wa kusini ni Wakristo.

Kikosi cha polisi cha Kiislamu cha Kano kinajulikana kama Hisbah na kinatekeleza kanuni kali za maadili.

Msemaji huyo aliambia BBC kwamba Jeshi la Polisi halikukusudia kuwaadhibu waalikwa 15 wa kiume na wanne wa kike waliokamatwa wakati wa uvamizi huo, badala yake lilikuwa likiwapatia ushauri, huku wazazi au walezi wao wakihimizwa kujitokeza.

"Tutachunguza njia ya mabadiliko kabla ya kuwafungulia mashtaka mahakamani, kwanza tunawashauri, na kuwahusisha wazazi na tuna matumaini kuwa watabadilisha mtindo wao wa maisha," alisema Ibrahim.

Inabainishwa kuwa mahakama za kiislamu za Kano hazijawahi kumhukumu mtu yeyote kwa kuwa mpenzi wa jinsia moja.

Ibrahim alisema kuwa watu 18 waliohudhuria sherehe hizo za harusi mwaka jana wameachiliwa baada ya kutia sahihi hati iliyotoa ahadi kwamba watabadili mtindo wao wa maisha.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu nchini Nigeria kwa muda mrefu yamekuwa yakifanya kampeni ya kutaka haki za wapenzi wa jinsia moja ziheshimiwe, lakini kuna upinzani mkubwa dhidi yake katika nchi ambayo Waislamu na Wakristo wengi wanashikilia maadili ya kidini.

***BBC***

# HABARI PICHA



Mafundi ujenzi wa barabara wakidhibiti maeneo korofi katika mji wa Songe, Kilindi mkoani Tanga, barabara inayotoka makao makuu ya wilaya hiyo kwenda Gairo mkoani Morogoro. **PICHA: DEGE MASOLI.**



Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa mahafali ya 20 ya chuo hicho yaliyofanyika jana katika viwanja vya chuo hicho, Kibele wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: IKULU.**



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akimkabidhi hati mkazi wa wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, wakati wa utoaji hati kwa wananchi wa wilaya hiyo waliokamilisha taratibu za kupatiwa katika urasimishaji makazi holela jana. **PICHA; WANMM.**




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akizungumza na viongozi wa TAKUKURU wakati akifunga Mkutano Mkuu wa Mwaka wa viongozi hao, uliofanyika jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mwananchi akipita jirani na taka zilizojaa katika soko la Mbezi Mwisho, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SIMON WANGWE ERNEST** anatangaza kupotea kwa cheti cha Diploma in Education at Open University Tanzania Adm **Na. ND 2016986469** kilichotolewa mwaka 2020.

Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:MAS/RB/2346/2022**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEEP POLL**
**CHANGE OF NAME**
**(THE REGISTRATION OF DOCUMENT ACT, CAP 117 R.E.2002)**



By this Deed I, LINES ISACK SIKAONGA, 68 Years, of P.O.BOX 1249-DODOMA do hereby abandon the names LINES ISACK SICHONE and input pursuant of such change on my name I HEREBY DECLARE that I shall at all records, deeds and instrument in writing in all actions and proceedings and all transactions and upon all occasions whatever use and sign by LINES ISACK SIKAONGA AND I HEREBY authorize and request all persons to designate and address me by such name LINES ISACK SIKAONGA and I relinquish my former names of LINES ISACK SICHONE this 2nd day of December,2022.

SIGNED and DELIVERED by the said LINES ISACK SIKAONGA who is known by me personally in my presence this 2nd Day Of December,2022 **DEPONENT**

**BEFORE ME:**
**SIGNATURE:**
**NAME: MAJALIWA WIGA**
**POSTAL ADDRESS:57 DODOMA**
**QUALIFICATION: ADVOCATE**

**THE DISTRICT COURT OF IRINGA**
**AT IRINGA**
**Probate and Administration Cause No 4 of 2022**
**In the matter of the Estate of the late SIZA DAVID SIMBEYE Of Mwangata ward within Iringa**
**And**
**In the matter of application for letter of administration by MARTHA BANTU SIMYOTA.**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the **10TH day of FEBRUARY, 2023**

Dated at Iringa this **21st day of DECEMBER, 2022.**

**RESIDENT MAGISTRATE**

**DRAWN AND FILED BY:**
**REHEMA JAILO MWAKYUSA(ADVOCATE)**
**AFRITANZA ATTORNEYS**
**MPAKANI CENTER BUILDING,SAM NUJOMA ROAD,**
**P.O.BOX 3176 DAR ES SALAAM**
**Phone; + 255 658 303 102**

**COPY TO;**
**HEIRS**

BURUDANI

# HAMISA: NAMPENDA MBAPPE



MWANAMITINDO na mwanamuziki, Hamisa Mobetto, amekiri upendo wake mkubwa kwa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe.

Mobetto alidokeza kuwa anavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambapo kupitia kwenye Instagram yake akadai kwamba anajifunza lugha ya Kifaransa kwa ajili yake.

"À se damner???? (Nakukufia)," aliandika kwenye ukurasa wake. Najifunza Kifaransa kwa ajili ya Mbappe," alieleza.

Mama huyo wa watoto wawili aliambatanisha ujumbe huo na picha yake nzuri inayoonyesha akiwa ameshika tumbo lake huku akiwa anawaza.

Mobetto ni miongoni tu mwa wanadada wengi ambao wametekwa moyo na mshambuliaji huyo wa PSG hasa baada ya mchezo wake mzuri katika fainali ya Kombe la Dunia ambayo ilifanyika Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Lusail nchini Qatar.

Licha ya Ufaransa kupoteza, Mbappe alikonga nyoyo za wengi kutokana na uchezaji wake mzuri kwenye mechi dhidi ya Argentina ambapo alifunga mabao matatu.

Pia, alipewa tuzo ya mfungaji bora baada ya kumaliza mashindano hayo na mabao nane.

Mwezi uliopita, mpenzi huyo wa zamani wa Diamond Platnumz, pia alikiri upendo wake kwa muigizaji wa Marekani, Michael B. Jordan.

## KWANGWARU YAFIKIA WATAZAMAJI MILIONI 100



VIDEO ya wimbo wa supastaa wa Bongo Fleva, Harmonize 'Kwangwaru', akimshirikisha bosi wake wa zamani, Diamond Platnumz, umefikisha watazamaji milioni 100 katika mtandao wa YouTube.

Kwangwaru inakuwa video ya nne Tanzania kufikisha watazamaji milioni 100 baada ya 'Yope Remix', 'Inama' na Waah!' zote za Diamond.

Video ya wimbo huo iliyotoka Aprili 14, 2018 iliongozwa na Kenny na Laizer Classic.

Itakumbukwa video ya wimbo 'Jerusalema' wake Master KG wa Afrika ndio video ya muziki iliyotazamwa zaidi YouTube Kusini mwa Jangwa la Sahara, tangu kutoka kwake Desemba 13, 2019 imefikisha watazamaji milioni 534.6.

## WAHU AFUNGUKA KUPATA MTOTO WA 3



MWANAMUZIKI wa kike wa Kenya, Wahu Kagwi, amefichua kwamba tayari alikuwa akijaribu kukubaliana na hali ya kuwa mama wa watoto wawili pekee kabla ya kubarikiwa mtoto wake wa tatu.

Akizungumza kupitia ukurasa wake wa Facebook, mama huyo wa mabinti watatu, alifichua kwamba madaktari tayari walikuwa wamemfahamisha kuwa ingekuwa vigumu kwake kupata mtoto mwingine.

Alidokeza kuwa tayari alidhani haingewahi kutokea kamwe yeye kupata mimba kwa vile alikuwa amepewa taarifa kwamba hawezi kupata ujauzito bila matibabu.

"Januari ikiwa mtu yeyote aliniambia kwamba ningemaliza 2022 kama mama wa watoto watatu ningesema huo ni utani wa kikatili. Waliniambia kuwa haiwezekani kupata ujauzito tena bila msaada wa matibabu. Nilikuwa najaribu kufanya amani na kuwa mama wa watoto wawili," alisema.

Mke huyo wa mwanamuziki, Nameless, alibainisha kwamba ilikuwa ndoto yake kuwa mama wa watoto watatu na akaeleza furaha yake kuona imetimia.

"Nina kila sababu ya kushukuru. Yeye hufanya vitu vyote kuwa vema kwa wakati wake," alisema mwanamuziki huyo.

Nameless na Wahu walimkaribisha duniani mtoto wao wa tatu Oktoba 11, 2022.

Katika taarifa yake, Wahu alisema alifurahia kubeba mtoto wake na alitazamia kwa hamu siku ambayo angekutana naye.

# CHAMA ATOA SIRI KUSHANGILIA BAO AKIWA AMESHIKA MASIKIO

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, ambaye ametoa pasi tisa za mwisho za mabao (assists 9), akifunga mabao matatu kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, amefunguka na kutoa tafsiri ya kushangilia mabao yake huku akiwa ameshika masikio.

Chama ambaye kwa siku za karibuni amekuwa na tabia ya kushika masikio anapofunga bao huku akikimbilia kwa mashabiki kushangilia, amesema kuwa maana ya ushangiliaji huo ni kwamba yeye na wachezaji wenzake wanasikia mambo mengi yanayoongelewa mabaya na mazuri kuhusu timu yao.

"Kushika masikio, ni kwamba watu wana mambo mengi ya kusema, tunasikia mambo mengi, hata tukiwa kwenye mitandao ya kijamii kuna mambo mengi yanakuwa yanasemwa na kuandikwa. Kwa hiyo mimi nashika masikio vile ni kwamba tunasikia vile vitu ambavyo wanaviongea, lakini muhimu ni kwamba vile vizuri vinavyoongelewa ndivyo tunavishika na kuvifanyia kazi, vile vibaya tunaviacha na kuwaonyesha watu kazi inayofanyika uwanjani," alisema Chama.

Mchezaji huyo raia wa Zambia hakusita kuonyesha furaha yake kwa mchezaji mwenzake Kibu Denis kufunga bao la kwanza msimu huu, huku yeye akiwa ndiye aliyetoa 'assist.'

"Kati ya 'assist' zangu bora kabisa ni ile niliyompasia Kibu, akafunga bao la kwanza msimu huu, unajua alikaa muda mrefu hajafunga, kwa hiyo ilikuwa ni furaha sana mimi na wachezaji wenzangu kumuona amefunga, nikaenda kumpongeza. Baadaye tulibaki mimi na Henock Inonga, tukawa tunaendelea kuongea naye na kumpa moyo, tukamwambia hilo bao liwe chachu ya wewe kujiamini na kufunga mengine kwa sababu limemrudishia imani kwa wanachama na mashabiki," alisema Chama.

Mchezaji huyo hakusita kumiminia shukurani kwa wanachama na mashabiki wa Simba kwani wao ndiyo wanaowafanya kuwa na furaha kwa sababu muda wote wanawapenda, wanawashangilia, wanafuata kila wanapokwenda na kuwapa moyo.

"Sisi hatuna cha kuwapa ila ni kujitahidi kujituma kwa ajili ya kuwapa furaha, lakini hata wao wanapokuwa wanasali watuweke kwenye maombi yao ili tupate afya njema, tuwe na nguvu ya kuwatumikia," alisema mchezaji huyo.

## Ruvu Shooting hali tete Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Ruvu Shooting sasa inaburuza mkia Ligi Kuu Bara, ikiwa imecheza mechi 11 mfululizo bila kupata ushindi baada ya kulazimishwa suluhu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Mtibwa Sugar.

Ushindi wa jana wa Tanzania Prisons dhidi ya Dodoma Jiji FC, unaifanya kufikisha alama 12 sawa na Ruvu Shooting, lakini ikiizidi kwa idadi ya mabao ya kufunga, hivyo kukwea hadi nafasi ya 15 na kuishusha timu hiyo ya mkoani Pwani.

Mara ya mwisho timu hiyo kushinda ilikuwa ni Septemba 29, mwaka huu ilipoichapa Coastal Union mabao 2-1 kwenye uwanja huo huo wa Uhuru na baada ya hapo imepita michezo 11 bila kupata ushindi ikipoteza michezo tisa na kutoka sare miwili.

Pia, timu hiyo imepata sare kwenye mechi ya juzi, baada ya kupoteza mechi tano mfululizo.

Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Mbwana Makata, amesema kwenye mechi hiyo umaliziaji ndiyo ulikuwa tatizo licha ya kutawala kwa dakika zote.

"Umaliziaji ndiyo tatizo, labda kama nilivyowahi kusema huko nyuma kuwa hatuna mastraika asilia, nawatumia mawinga kucheza kama mastraika kwa sababu wachezaji wetu wanane wamekwenda kwenye kozi za kijeshi, lakini ukiacha hilo, mechi hii tumeitawala sana na hatujakata tamaa tutaendelea kupambana," alisema Makata aliyechukua nafasi ya Charles Boniface Mkwasa, aliyejiuzulu hivi karibuni kutokana na matokeo mabovu.

Naye Kocha Msaidizi na Mtibwa Sugar, Awadh Juma, alisema ilibidi waingie kwa nidhamu kwenye mechi hiyo kwa sababu Ruvu Shooting ni timu nzuri na kwa muda mrefu wamekosa matokeo, hivyo walijua watakuja kwa kushambulia.

"Walicheza kwa kufunguka zaidi wakitaka matokeo, na hata sisi tuliingia hivyo hivyo, tukawa tunapishana, lakini baadaye tukaona tubadilike kwa sababu sisi tuko ugenini pointi moja ilikuwa muhimu kwetu," alisema Awadh.

## NABI NA MTIHANI

INATOKA UK. 32

Polisi Tanzania, ambapo Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera anamtaka, Makambo kwa mkopo.

Katika hatua nyingine, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema ushindi wa juzi wa mabao 3-0 dhidi ya Coastal Union ni maandalizi yao ya kukabili Azam FC Jumapili wiki hii.

Alisema walijua hauwezi kuwa mchezo rahisi kwani Coastal Union ni timu yenye wachezaji bora kwenye safu ya ushambuliaji, hivyo walichukua tahadhari zote.

"Tulijua kuwa ili tufunge tunapaswa kuwa na subira, tucheze kwanza mpira, wao wacheze nyuma ya mpira, watachoka halafu tutapata njia za kufunga mabao.

"Kipindi cha kwanza hatukupata nafasi nyingi, cha pili walichoka baada ya kukimbia nyuma ya mpira kwa muda mrefu, tukapata mabao mawili, kikubwa ilikuwa mechi nzuri kwa umakini waliouonyesha hii ikiwa ni maandalizi ya michezo ijayo, alisema na kuongeza;

"Unajua kila mechi unayoenda kucheza unazingatia ulichokifanya katika mchezo uliopita, na mchezo unaofuata kuna mabadiliko ya kiufundi Tuisila Kisinda aliumia hivyo ikabidi tuwatumie wengine.

"Wachezaji waliocheza leo (juzi), tuliamini kuwa wangetupatia matokeo, hivyo sasa tunaangalia mchezo unaofuata ambao ni mgumu, unahitaji umakini sana."

Alisema kuwa kitendo cha Denis Nkane, kuumia ni suala la kawaida kwenye mchezo wa mpira wa miguu kwa kuwa unaruhusu mgusano wa moja kwa moja na kwamba kwa mwonekana kabla ya vipimo inaonyesha majeraha aliyopata yalikuwa ni makubwa.

"Mpira ni mchezo unaoruhusu kugongana kitu tunachokilalamikia ni faulo zisizokuwa na ulazima mtu hana mpira unamfanyia madhambi.

"Kwenye mpira kumfanyia mwenzio faulo ni jambo la kawaida ndio maana refarii yuko pale kwa ajili ya kuhakikisha wachezaji wanakuwa salama muda wote wa mchezo dakika 90," alisema Kaze.

Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alisema ulikuwa mchezo mgumu na waliingia kwa ajili ya kutafuta pointi tatu, lakini ubora wa Yanga umeamua mechi hiyo.

"Tuko kwenye kipindi kigumu tumeondokewa na kocha mkuu tukiwa kwenye maandalizi, hivyo kuna vitu havikwenda tulivyopanga nawapongeza Yanga kwa ushindi walioupata ingawa wachezaji wangu walipambana bahati haikuwa yetu," alisema Lazaro.

## LA TATU...



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia), akishangilia sambamba na winga wa timu hiyo, Jesus Moloko, baada ya kuifungia timu yake bao la tatu wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Coastal Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens, Yanga vita leo

INATOKA UK. 32

kocha wa SHE Coparates ya Uganda na Nkoma akiwa anainoa Simba na kufanikiwa kushinda mechi zote mbili katika hatua ya makundi na fainali.

Licha ya kukutana kwa timu hizo huku Simba Queens wakiwa wanaongoza kupata matokeo mazuri mbele ya Yanga Princess, ambapo katika mechi 10 zilizokutana, Simba Queens imeshinda nane, kufungwa moja na sare moja.

Kuelekea mchezo huo, Kocha wa Simba Queens, Lukulu ambaye ni mwenyeji wa mchezo huo, alisema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo wa leo na utakuwa mgumu sana kwa sababu ina kikosi imara na kocha mzuri.

Alisema wanahitaji kupata matokeo, hivyo lazima kucheza kwa heshima kubwa kwa kila timu watakayokutana nayo na kwamba pamoja na Yanga kuwa vizuri, lakini Simba Queens ni bora zaidi.

"Hii ni 'dabi' yangu ya kwanza, lakini ninaifahamu Yanga nimecheza nao na kuwaona wapinzani wangu, nimeandaa kikosi changu imara na tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo wetu wa kesho (leo).

"Ni mpambano wa makocha, Seba aliwahi kufundisha Simba Queens, anaifahamu vizuri, lakini nitaingia na mbinu zangu kuhakikisha tunapata ushindi katika mchezo wa leo," alisema kocha Lukulu

Nahodha wa Simba Queens, Opa Clement, alisema wamejiandaa vizuri na kwamba kazi kubwa iliyobakia ni kufanya majukumu yao uwanjani ili kuendeleza ubabe wao mbele ya Yanga.

"Tuko tayari kwa ajili ya mchezo wa kesho (leo), tumechukua ubingwa na tukaenda kuwakilisha CECAFA katika michuano ya kimataifa, lakini tunahitaji kurejea huko kimataifa, hivyo tunalazimika kushinda mechi zote za ligi ikiwamo dhidi ya Yanga Princess kupata alama tatu," alisema Opa.

Kocha Nkoma, alisema utakuwa mchezo mgumu kidogo kwa sababu ni 'dabi' ambayo siku zote inakuwa na ugumu hasa kwa sababu Simba Queens wametoka kucheza mechi kubwa na wanaingia kwa heshima kubwa.

"Tumejipanga vizuri kukabiliana na Simba Queens nina waheshimu sana kwa sababu mchezo utakuwa mgumu kutokana na sina muda mrefu ndani ya Yanga Princess ambayo haijakuwa na muunganiko mzuri," alisema Nkoma.

Nahodha wa Yanga Princess, Amina Bilal, alisema kila mchezaji ana morali wa mechi hiyo na wako tayari kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wa leo.

"Kocha ametuandaa vizuri na kazi kubwa imebaki kwetu na tunaenda kucheza kwa kujitoa kuhakikisha tunafuta uteja na kuondoka na ushindi," alisema Amina.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUSAINI SAUDIA

KLABU ya Saudia ya Al Nassr inatarajia mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri wa miaka 37, kukamilisha uhamisho wake mwishoni mwa mwaka. Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United atasaini mkataba wa miaka miwili na nusu wenye thamani ya euro milioni 200. ***(Marca)***

### MARTINELLI KUFUNGWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Brazil, Gabriel Martinelli, mwenye umri wa miaka 21, anatarajiwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Mail)***

### MESSI KUBAKISHWA PSG

MABINGWA wa Ufaransa, Paris St-Germain, wanataka kusalia na mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, kwenye klabu hiyo siku chache zijazo. Mkataba wa mshindi huyo wa Kombe la Dunia unamalizika msimu ujao wa majira ya joto na yuko huru kuzungumza na klabu nyingine nje ya Ufaransa kuanzia Januari Mosi mwakani. ***(Goal)***

### COSTA KULIPWA MILIONI 65

KLABU ya Manchester United italazimika kumlipa kipa wa Porto, Diogo Costa, kitita cha pauni milioni 65 iwapo wanataka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 23, mwishoni mwa msimu huu. ***(Correio da Manha)***

### GVARDIOL KUBAKI LEIPZIG

MLINZI wa Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 20, huenda akasalia katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani msimu huu wa majira ya joto na kipengele cha kuachiliwa cha pauni milioni 110 kitaanza kutumika katika mkataba wake mwaka 2024. ***(Sky Sports)***

### MUDRYK ANUKIA ARSENAL

KLABU ya Arsenal imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21 wakati wa dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa Januari, mwakani kwa mujibu wa mkurugenzi wa michezo wa klabu yake ya sasa ya Shakhtar Donetsk. ***(Football 365)***

### OCHOA KUTUA ITALIA

GOLIKIPA wa Mexico, Guillermo Ochoa, mwenye umri wa miaka 37, anatazamiwa kujiunga na Klabu ya Serie A ya Italia, Salernitana, kwa uhamisho wa bure baada ya mkataba wake katika Club America kumalizika. ***(Sky Sports Italia)***

### BASTONI MKATABA MPYA

KLABU ya Inter Milan imeanza mazungumzo ya mkataba mpya na beki wa Italia, Alessandro Bastoni kuhusu mkataba mpya, huku Manchester City na Tottenham Hotspur zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(La Gazzetta Dello Sport)***

### DE PAUL ALIKARIBIA LEEDS

KIUNGO wa kati wa Argentina, Rodrigo De Paul, mwenye umri wa miaka 28, alikaribia kujiunga na Leeds United kutoka Udinese kabla ya kuhamia Atletico Madrid. ***(TalkSPORT)***

### DIAZ HAONDOKI BLACKBURN

MSHAMBULIAJI wa Blackburn na Chile, Ben Brereton Diaz, mwenye umri wa miaka 23, huenda akasalia Ewood Park Januari na kuweka chaguo lake wazi kwa uhamisho wa bila malipo msimu wa majira ya joto. ***(Football League World)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA WAKARIBIA KUMNASA RASMI KANTE

**Majeraha ya hivi karibuni yalimfanya asishiriki Kombe la Dunia, lakini hilo halijamzuia...**

**BARCELONA, Hispania**

MCHEZAJI N'Golo Kante anaripotiwa kukaribia kusaini mkataba wa awali na Barcelona, Januari mwakani, wakati kocha Xavi anatazamia kumsajili Mfaransa huyo ili kuimarisha safu yake ya kiungo msimu ujao.

Kwa mujibu wa Jarida la Sport la Hispania, kiungo huyo wa kati wa Chelsea anakaribia kufikia makubaliano na wababe hao wa Katalunya, huku mkataba wake wa sasa huko Stamford Bridge ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Majeraha ya hivi karibuni zaidi ya Kante yalimfanya asishiriki Kombe la Dunia, lakini hilo halijamzuia kuhusishwa na Barca.

Huku ikiwa imesalia zaidi ya miezi sita katika mkataba wake, Kante anafikiriwa kuwa na nia ya kutatua mustakabali wake haraka iwezekanavyo, na kwa hivyo atataka kufikia makubaliano na 'Blaugrana' hao Januari.

Chelsea wanaripotiwa kuongeza mkataba wa miaka miwili Stamford Bridge, ingawa anatafuta mwaka wa tatu ambao haujafika.

Mazungumzo na wababe hao wa Katalunya yameendelea vema, kwa mujibu wa Sport, huku mkurugenzi wa soka, Mateu Alemany akishughulikia majadiliano ya moja kwa moja na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

Hakuna ada ambayo ingehitajika kutokana na kwamba mkataba wa mchezaji huyo unamalizika msimu wa majira ya joto, na atatoa msaada kamili kwa safu ya kati katika kipindi cha mpito.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 1.99
X | 3.51
2 | 3.46

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KIPA WA ARGENTINA AWINDWA BAYERN



**MUNICH, Ujerumani**

GOLIKIPA wa Aston Villa aliyeshinda Kombe la Dunia akiwa na Argentina, Emiliano Martinez, anasakwa na wababe wa Ujerumani, Bayern Munich iliyopo chini ya Kocha Mkuu, Julian Nagelsmann.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye alikuwa kwa muda wa mkopo na timu kama Oxford, Sheffield Wednesday na Rotherham wakati wa siku zake za Arsenal, alitwaa tuzo ya golikipa bora wa michuano hiyo.

Kando na hayo, golikipa huyo katika dakika za lala salama dhidi ya Australia na Ufaransa, Martinez alikuwa shujaa wa mikwaju miwili ya penalti dhidi ya Uholanzi na Ufaransa.

Bayern wanatamani sana kuimarisha safu yao ya walinda mlango msimu huu wa baridi baada ya Manuel Neuer kuvunjika mguu katika safari ya baada ya Kombe la Dunia kufanya vibaya.

Ingawa itakuwa ngumu kwa Muargentina huyo kukataa soka ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Villa hawana shinikizo la kumuuza na amepewa mkataba hadi msimu wa majira ya joto wa 2027.

Bado wakala wa mchezaji huyo, Gustavo Goni, amebatilisha uvumi huo na baadhi ya maoni ya kutiliwa shaka kwa vyombo vya habari vya Italia mwishoni mwa wiki.

Alipoulizwa kama mteja wake atafikiria kuhamia Serie A, Goni alijibu: "Leo kuna timu chache ambazo zinaweza kumudu kipa kama yeye."

# Mbappe: Tutarudi tena

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe ameahidi Ufaransa itarejea katika hatua kubwa zaidi baada ya hat-trick yake ya fainali ya Kombe la Dunia kutotosha kuwanyima Lionel Messi na Argentina kutwaa taji hilo huko nchini Qatar.

Bao la tatu la Mbappe katika fainali ya Kombe la Dunia kwa vijana hao wa Kocha Didier Deschamps liliihakikisha Ufaransa kuingia kwenye mikwaju ya penalti katika Uwanja wa Lusail.

Kisha akafunga penalti ya kwanza, lakini akanyimwa ushindi wa pili wa Kombe la Dunia kwani Kingsley Coman na Aurelien Tchouameni walishindwa kufunga, na kuwapa 'Albiceleste' taji lao la tatu.

Mbappe, ambaye juzi alitimiza umri wa miaka 24, ameandika katika chapisho lake la kwanza la mtandao wa kijamii baada ya kushindwa kwa 'Les Bleus' kwa "tutarudi" akiandika katika Instagram.

Mshindi mara tatu wa Kombe la Dunia, Pele alikuwa miongoni mwa waliojibu chapisho la Mbappe, kwa kuandika tu: "Pole".



Idadi ya mabao manne ya mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain katika fainali za Kombe la Dunia hailinganishwi na mchezaji yeyote, huku akiwa miongoni mwa wachezaji watano kufunga mabao katika mechi mbili za michuano hiyo pamoja na Vava, Pele, Paul Breitner na Zinedine Zidane.

Mshambuliaji wa zamani wa Ufaransa, Louis Saha, alisifu uchezaji wa Mbappe alipozungumza na Sky Sports na kueleza kuwa jambo hilo halijawahi kutokea kwa mchezaji wa umri wake.

"Yalikuwa ni mafanikio ya ajabu kwa kijana kama yeye kufanya hivyo kwenye hatua hiyo," alisema Saha.

"Inasikitisha kwake kwa sababu kwa umri mdogo, angeandika historia yake ya kipekee. Hakuna mtu aliyefanya hivi.

"Kwa heshima zote kwa wachezaji wengine, historia za mchezo, uchezaji wa kijana huyu kudumisha ndoto ya Ufaransa, ubora wa mtazamo wake kupitia mashindano, ulikuwa wa kuvutia kabisa," alisema.

344,733/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 22/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1439 | Kayserispor vs Genclerbirligi | 1.30 | 5.04 | 7.56 |
| 14:00 | 4534 | KMC vs Polisi Tanzania | 1.75 | 3.20 | 4.66 |
| 14:00 | 5154 | Kenkre FC vs Real Kashmir | 4.59 | 3.41 | 1.70 |
| 15:00 | 1397 | KS Kastrioti Kruje vs Egnatia Rrogozhine | 3.05 | 2.95 | 2.47 |
| 15:00 | 1526 | KF Erzeni vs Bylis Ballsh | 2.19 | 2.92 | 3.31 |
| 15:00 | 1799 | Mathare United vs Nzoia United | 5.60 | 3.25 | 1.71 |
| 15:00 | 1982 | Kenya Commercial Bank vs Tusker | 3.66 | 2.68 | 2.20 |
| 15:00 | 5420 | Konyaspor vs Bodrumspor | 1.63 | 3.88 | 4.37 |
| 15:30 | 1072 | AL Baten vs Al Raed Club | 5.65 | 3.90 | 1.50 |
| 15:30 | 1292 | Othellos Athienou vs PO Xylotymbou | 1.84 | 3.50 | 3.70 |
| 15:30 | 2421 | Als Omonia vs Anagennisi Derynia FC | 1.96 | 3.35 | 3.80 |
| 15:30 | 2983 | Ermis Aradippou vs M E A P Nisou | 2.33 | 3.10 | 3.15 |
| 15:30 | 3487 | Paeek vs AEZ Zakakiou | 3.35 | 3.20 | 2.16 |
| 15:30 | 3730 | Achyronas Onisilos vs Alki Oroklini | 1.70 | 3.52 | 4.40 |
| 15:45 | 1934 | Kalamata FC vs GS Ilioupoli | 1.44 | 3.75 | 7.20 |
| 15:45 | 4557 | Panachaiki vs Kallithea FC | 2.25 | 2.92 | 3.21 |
| 15:45 | 5532 | Olympiacos Piraeus B vs Proodeftiki FC | 2.06 | 3.07 | 3.46 |
| 16:00 | 3074 | Legetafo Legedadi vs Saint George FC | 10.71 | 5.06 | 1.24 |
| 16:00 | 5379 | Etincelles vs APR FC | 5.65 | 3.36 | 1.60 |
| 16:00 | 5807 | Mbeya City vs Singida BS FC | 2.37 | 2.66 | 3.29 |
| 16:30 | 5524 | Pordenone vs Triestina | 1.93 | 3.34 | 3.94 |
| 16:30 | 5554 | Extension Gunners vs Nico United | 2.33 | 3.30 | 2.95 |
| 17:00 | 3246 | Jamshedpur vs FC Goa | 3.06 | 3.35 | 2.11 |
| 17:00 | 5679 | Gaziantep BB vs Boluspor | 1.85 | 3.55 | 3.60 |
| 18:00 | 2443 | OFI Crete vs Atromitos | 2.19 | 3.19 | 3.28 |
| 18:00 | 3866 | Al Fateh (KSA) vs AL Tai | 2.26 | 3.17 | 2.92 |
| 19:00 | 3122 | MS Kiryat Gat W vs Maccabi Kishronot Hadera W | 1.50 | 4.70 | 5.20 |
| 19:00 | 3531 | Arba Minch Kenema vs Sidama Bunna SC | 2.30 | 2.87 | 3.16 |
| 19:00 | 4134 | Adana Demirspor vs Caykur Rizespor | 1.49 | 4.17 | 5.24 |
| 20:00 | 1924 | Ethnikos Achnas vs Omonia Aradippou | 2.28 | 3.15 | 3.20 |
| 20:00 | 2167 | Omonia Nicosia vs Apollon Limassol | 2.47 | 3.19 | 2.85 |
| 20:00 | 2845 | Aris Limassol vs Apoel Nicosia | 2.85 | 3.20 | 2.45 |
| 20:30 | 3670 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.66 | 4.40 | 4.20 |
| 20:30 | 4001 | Panetolikos vs PAOK | 4.79 | 3.49 | 1.73 |
| 21:00 | 1094 | Al Ittihad Jeddah vs Al Shabab Riyadh | 2.21 | 3.11 | 3.07 |
| 21:00 | 2027 | SD Gernika vs Celta Vigo | 13.95 | 5.98 | 1.20 |
| 21:00 | 2131 | Galatasaray vs Keciorengucu | 1.22 | 5.84 | 9.35 |
| 21:00 | 3494 | CD Linares vs Racing Santander | 2.94 | 3.14 | 2.40 |
| 21:00 | 4006 | CD Eldense vs Burgos | 2.64 | 3.09 | 2.69 |
| 21:00 | 4343 | CP Cacereno vs Girona | 10.91 | 4.96 | 1.28 |
| 21:30 | 4233 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Hapoel Katamon Jerusalem W | 3.60 | 4.20 | 1.80 |
| 21:30 | 5833 | Hapoel Petach-Tikva W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 3.80 | 4.40 | 1.73 |
| 22:45 | 4727 | Cardiff Met Uni. vs Newtown AFC | 1.97 | 3.46 | 3.31 |
| 23:00 | 1197 | CD Arenteiro vs Atletico Madrid | 12.90 | 6.35 | 1.19 |
| 23:00 | 1331 | Chelsea W vs Paris Saint Germain W | 2.04 | 3.40 | 3.16 |
| 23:00 | 1803 | Gimnastic Tarragona vs Malaga | 2.89 | 3.14 | 2.43 |
| 23:00 | 2517 | Manchester City vs Liverpool | 1.99 | 3.51 | 3.46 |
| 23:00 | 3480 | Real Oviedo vs Granada | 2.88 | 2.93 | 2.58 |
| 23:00 | 4300 | CF La Nucia vs Las Palmas UD | 3.73 | 3.28 | 1.99 |
| 23:15 | 2812 | Moreirense vs FC Arouca | 2.07 | 3.26 | 3.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# GEITA YAWAITA SIMBA KUMALIZANA NA SAIDO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Geita Gold, imesema inakaribisha mazungumzo kati yake na Klabu ya Simba kama inamhitaji kiungo wake mshambuliaji, Saido Ntibazonkiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo, Zahara Michuzi, amesema mpaka sasa mchezaji huyo ni mali yao kwa sababu ana mkataba, lakini Klabu ya Simba kama imeonyesha nia ya kutaka kumchukua, basi wanawakaribisha kukaa meza moja kwa ajili ya kufanikiwa usajili huo.

"Makubaliano yetu na utamaduni wetu Geita Gold ni kwamba mchezaji anapoona kuna maslahi anaruhusiwa kwenda, lakini tunahakikisha na sisi tuliomuonyesha na kuwa jukwaa la watu kumuona, tunanufaika na uondokaji wake, unajua klabu yetu ni tanuri ya kupika wachezaji wazuri, wengine mnawafamu walikuwapo wameondoka na wengine hamuwafahamu, wako kwenye kikosi chetu cha chini ya miaka 20, ni wachezaji wazuri tu.

"Kikosi unachokiona kina wachezaji watatu ambao wametoka chini ya miaka 20 kwa hiyo tuna uwezo wa kuziba mapengo ya wachezaji wanaoondoka, mara zote kuondoka kwa mmoja ni kuonekana kwa mchezaji mwingine, kwa hiyo tunatoa nafasi kwa klabu inayomhitaji milango iko wazi, lakini Geita Gold malengo yake yatatekelezeka na tutafika tunakotaka," alisema Zahara. Naye Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Felix Minziro, alisema hata yeye anazisikia taarifa za mchezaji wake, Saido kutakiwa na Klabu ya Simba, lakini kuondoka kwake itategemea na maamuzi ya uongozi.

"Dirisha dogo limefunguliwa, najua kuna wachezaji wataondoka na wengine wataingia, kuhusu Saido alisema hata mimi taarifa hizo nimezisikia kwenye mtandao, lakini hivi karibuni alisaini mkataba na klabu yetu, kwa hiyo kuondoka au kubaki itategemea na uongozi, siku zote mchezaji yeye anaangalia maslahi na klabu pia inaangalia itaingiza nini kama itamuuza," alisema.

Hivi majuzi Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alifunguka kuhusu usajili, akisema watafanya wa maana kipindi hiki cha dirisha dogo, lakini hakusita kumwagia sifa Saido akisema ni mchezaji mzuri mno, lakini hakutaka kwenda mbali sana akidai bado ana mkataba na Geita Gold.

KIJIJI...



Mchezaji wa timu ya Mtibwa Sugar, Ismail Muhesa (kulia), akimiliki mpira dhidi ya wachezaji wa Ruvu Shooting, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NAMUNGO YAIFUATA RUVU SHOOTING

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuichapa mabao 2-0 Ihefu FC katika mchezo Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanjwa Majaliwa mkoani Lindi, Kikosi cha timu ya Namungo kimeanza safari leo kuifuata timu Ruvu Shooting, kuelekea mchezo utakaopigwa Jumamosi wiki katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, jana kutoka mkoani Lindi, Kaimu Kocha Mkuu wa Namungo FC, Denis Kitambi, alisema wachezaji wanaendelea vema na mazoezi kwa ajili ya nchezo huo.

"Mungu akipenda kesho asubuhi (leo), tutaanza safari kuelekea Dar es Salaam kukutana na Ruvu Shooting, malengo yetu ni kupata pointi tatu," alisema Kitambi.

Alisema wachezaji wote wana morali ya juu kuelekea mchezo huo wakitaka kuendeleza ushindani.

Alisema mchezo wao uliopita wachezaji wake walionyesha kiwango kizuri jambo ambalo linatia moyo kuendelea kukinoa kikosi hicho.

Naye Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Mkadeba, alisema wanatarajia kufanya usajili wa kutisha msimu huu kwa ajili ya kuziba sehemu zenye mapungufu.

Alisema wiki hii wanatarajia kupokea ripoti ya kocha wao ambayo itaonyesha idadi na aina ya wachezaji watakaowaacha na wale anaotaka kuendelea nao.

Simba yaitwa mezani kwa Saido UKURASA 31

Michezo
Alhamisi Des
Nipa






# NABI NA MTIHANI KWA KAMBOLE, YACOUBA

## ●●●Wakigeni wengine wawili kutolewa kwa mkopo kupisha...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umempa jukumu Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, kuamua nani anataka abaki katika kikosi chake kati ya straika Lazarous Kambole na Yacouba Songne ambao wamepona baada ya kuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu kutokana na majeraha yaliyokuwa yakiwakabili.

Yanga wanataka kumtema mchezaji mmoja kati ya hao wawili na sasa wameamua jukumu hilo kumuachia Nabi kwa sababu yeye ndiye anayejua nani atafiti kwenye kikosi chake hasa wakati huu ambao timu inakabiliwa na michuano mbalimbali ikiwamo Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema Kambole na Yacouba walikuwa majeruhi na wamepona na kuhusu nani abaki hilo ni jukumu la kocha kulingana na mahitaji ya kikosi chake kuelekea katika mashindano yaliyoko mbele yao.

Alisema kulingana na idadi ya wachezaji 12 wa kigeni wanaotakiwa kusajili kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), wanalazimika mmoja kuondoka kwa sababu wataongeza nyota wawili wengine wawili wa kigeni katika dirisha hili dogo la usajili lililofunguliwa Desemba 16, mwaka huu.

Hata hivyo, tayari Yanga ina wachezaji 12 wakigeni kwa mujibu wa kanuni, ambao ni Djigui Diarra, Joyce Lomalisa, Djuma Shaban, Yannick Bangala, Khalid Aucho, Jesus Moloko, Bernard Morrison, Stephane Aziz Ki, Heritier Makambo, Fiston Mayele, Gael Bigirimana na Tuisila Kisinda.

"Kulingana na idadi ya wachezaji wa kigeni, tunalazimika mmoja kuondolewa hilo tumemuachia Nabi, kati ya Yacouba na Kambole nani atabaki, pia tumepokea maombi ya mikopo kwa baadhi ya wachezaji wetu kutoka klabu zingine na tutawaruhusu kwenye dirisha hili dogo.

"Huu ni wakati wetu Yanga kuweka alama kwenye mashindano ya kimataifa, mfumo wetu ni uleule mchezaji tunayemsajili lazima awe bora sana au zaidi ya yule ambaye tunaye," alisema Hersi.

Hata hivyo, taarifa zilizolifikia gazeti hili kutoka moja ya chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo, kati ya maombi yaliyowasilishwa mezani Yanga ni kutoka

INAENDELEA UK. 28

## Simba Queens, Yanga vita leo

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba Queens na Yanga Princess wakitarajia kumaliza ubishi wa nani zaidi katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu, vita kubwa kati ya makocha wa timu hizo mbili, Charles Lukulu ambaye anahitaji kuweka heshima kubwa mbele ya Sebastian Nkoma, aliyewahi kuwa kocha wa Malkia wa Simba hao.

Simba Queens na Yanga Princess zitashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kumenyana kwenye mechi ya Ligi Kuu raundi ya tatu, zote zikiwa na alama tatu katika nafasi ya tano na sita baada ya kupoteza michezo yao ya ufunguzi ya ligi hiyo.

Vita vya makocha hao ni baada ya Kocha wa Simba, Lukulu kutaka kulipa kisasi kwa kumfunga Kocha wa Yanga Princess, Nkoma katika mchezo wa leo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania utakaopigwa saa 11: 00 jioni.

Makocha hao walikutana katika michuano ya CECAFA huku Lukulu akiwa

INAENDELEA UK. 28

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >